

Ripoti Maalum

# Upatikanaji wa Silaha Ndogo ndogo na Hisia za Usalama nchini Kenya: Ukadiriaji

*Manasseh Wepundi, Eliud Nthiga, Eliud Kabuu, Ryan Murray, na Anna Alvazzi del Frate*

small arms survey

HARAMBEE

Kenya National Focal Point On Small Arms & Light Weapons

Ministry of Foreign Affairs of Denmark

Ripoti Maalum

Juni 2012

# Upatikanaji wa Silaha Ndogo Ndogo na Hisia za Usalama nchini Kenya: Ukadiriaji

*Manasseh Wepundi, Eliud Nthiga, Eliud Kabuu, Ryan Murray, na Anna Alvazzi del Frate*

Uchunguzi uliofanywa na Shirika la Uchunguzi wa Silaha Ndogo Ndogo, Small Arms Survey, na Shirika la Kitaifa la Kushughulikia silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi, Kenya National Focus Point on Small Arms and Light Weapons, kwa usaidizi kutoka kwa Wizara ya Mashauri ya Kigeni ya Denmark

small arms survey

HARAMBEE

Kenya National Focal Point On Small Arms & Light Weapons

Ministry of Foreign Affairs of Denmark

# Haki Miliki

Kimechapishwa nchini Switzerland na shirika la Small Arms Survey

© Shirika la Small Arms Survey, Taasisi ya Masomo ya Juu ya Kimataifa na Maendeleo, Geneva 2012

Chapisho la kwanza Juni 2012

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki au visehemu vyake vyovyote havipaswi kutolewa kwa namna yoyote ile, au kuhifadhiwa kwa mtambo wowote ule utakaovitoa, au kurushwa hewani kwa namna au njia yoyote ile bila ya kuwa na idhini iliyoandikwa kutoka kwa shirika la Small Arms Survey, au ilivyobainishwa kisheria, au chini ya masharti yaliyokubaliwa na shirika linalohusika na haki za utoleshaji. Maswali yanayohusu utoaji ulio nje ya upeo ulioshughulikiwa hapo juu yanapaswa kutumwa kwa Meneja wa Uchapishaji, Small Arms Survey, katika anwani iliyopo hapo chini.

Small Arms Survey
Graduate Institute of International and Development Studies
47 Avenue Blanc, 1202 Geneva, Switzerland

Kimetafsiriwa na Joan Simba
Kimehaririwa na Esther Munguti

Usanifu wa ramani umefanywa na Jillian Luff, MAP*grafix*
Utayarishaji chapa umefanywa na Frank Benno Junghanns

Kimepigwa chapa na GPS mjini France

ISBN 978-2-9700771-8-3
ISSN 1661-4453

# Shirika la Small Arms Survey

Shirika la Small Arms Survey ni mradi huru wa utafiti uliyoko kwenye Taasisi ya Masomo ya juu ya Kimataifa na Maendeleo, Graduate Institute of International and Development Studies, huko Geneva Switzerland. Mradi huo, ulioanzishwa 1999, unafadhiliwa na Idara ya Jamhuri ya Switzerland ya Mashauri ya Kigeni, pamoja na michango kutoka kwa serikali za Australia, Ubelgiji, Canada, Denmark, Finland, Ujerumani, Uholanzi, Norway, Sweden, Uingereza na Marekani. Shirika hilo linatoa shukurani kwa usaidizi wa hapo awali uliopokelewa kutoka kwa serikali za Ufaransa, New Zealand na Uhispania. Shirika hili pia lingependa kutoa shukurani kwa usaidizi wa kifedha ambao limepokea kwa muda wa miaka kadhaa kutoka kwa mashirika, programu na taasisi za Umoja wa Mataifa.

Madhumuni ya shirika la Small Arms Survey ni kuwa watoaji wakuu wa habari kwa umma kuhusu masuala yote ya silaha ndogo ndogo na ghasia kunakotumika silaha; kuhudumu kama kituo cha rasilimali kwa serikali kadhaa, waundaji sera, watafiti, na wanaharakati; kuchunguza mipango na juhudi za kitaifa na za kimataifa (za serikali na zisizo za serikali) kuhusu silaha ndogo ndogo; kuunga mkono juhudi za kushughulikia athari za ueneaji na utumiaji mbaya wa silaha ndogo ndogo; na kuwa ofisi au eneo la kubadilishana habari na kusambaza kanuni bora. Shirika hilo hali kadhalika hufadhili utafiti wa nyanjani na juhudi za kukusanya habari, hususan katika mataifa na maeneo yaliyoathiriwa. Shirika hilo lina wafanyakazi wa kimataifa wenye ujuzi katika masomo ya kiusalama, sayansi ya kisiasa, sheria, uchumi, masomo ya maendeleo, elimu-jamii au sosiolojia na elimu-jinai, na hushirikiana na mtandao wa watafiti, taasisi washirika, mashirika yasiyo ya kiserikali na serikali katika zaidi ya nchi 50.

Shirika la Small Arms Survey
Graduate Institute of International and Development Studies
47 Avenue Blanc, 1202 Geneva, Switzerland

**p** +41 22 908 5777 **f** +41 22 732 2738
**e** sas@smallarmssurvey.org **w** www.smallarmssurvey.org

# Shirika la Kitaifa la Kenya kuhusu Silaha Ndogo Ndogo (KNFP)

Shirika la Kitaifa la Kenya la Kushughulikia Silaha Ndogo Ndogo (KNFP) ni juhudi za mashirika mbalimbali na Idara katika Wizara ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Ndani katika Afisi ya Rais. Shirika la KNFP lilibuniwa mnamo mwaka wa 2002 na kuanza kutekeleza shughuli zake mwaka wa 2003, kwa kuleta pamoja wizara mbalimbali za serikali, idara na mashirika yasiyo ya kiserikali katika usimamizi na udhibiti wa silaha ndogo ndogo nchini Kenya.

Shirika la KNFP lina maono ya kuwa na jamii yenye amani, iliyo salama, yenye ufanisi na isiyokuwa na silaha haramu, ili kuhakikisha maendeleo endelevu. Wito au lengo la shirika hili ni kusimamia na kushirikisha hatua zote katika kushughulikia tatizo la kuenea kwa wingi wa silaha ndogo ndogo katika nyanja zote nchini Kenya.

Shirika la KNFP limepata kibali chake kutokana na hati za kisheria za kimataifa, kieneo na kanda ambazo Kenya imetia sahihi na lina jukumu la kushirikiana na mataifa mengine katika kiwango cha kanda, eneo na kimataifa, pamoja na mashirika mengine husika, katika masuala yote yanayohusu utekelezaji wake.Hii inajumuisha uundaji wa mwongozo wa sera na utafiti; juhudi za uchunguzi ili kupambana, kuzuia na kuangamiza biashara haramu ya silaha ndogo ndogo katika nyanja zote; na kushirikisha ukusanyaji na uangamizaji wa silaha ndogo ndogo.

Kwa kutilia maanani kuenea kijiografia kwa tatizo la silaha ndogo ndogo nchini, Shirika la KNFP limebuni majopo kazi ya mikoa na wilaya (DTF) ili kuzingatia kushughulikia tatizo hili kote nchini Kenya. Jukumu la DTF's ni kurahisisha utekelezaji wa Mpango Tekelezi wa Taifa la Kenya wa kudhibiti na Kusimamia Silaha katika viwango vya wilaya na mashinani, kwa kushirikiana na kamati za amani wilayani na mashirika ya kijamii ya kutetea haki za raia, ili kuafikia mfumo jumuishi wa kuzuia, kutatua na kusimamia mizozo. Hii ni kuambatana na maadili muhimu ya shirika

la KNFP ya kujibu au kuitikia wito, ushirikiano, ujumuishaji, uongozi na uadilifu.

Shirika la Kitaifa la Kenya kuhusu Silaha Ndogo Ndogo

Jengo la Bruce House, Orofa ya 14
(Upande wa Kusini, South Wing)
Barabara ya Standard
S.L.P 30510 – 00100
Nairobi, Kenya

**p** +254 20 343 462/8
**f** +254 20 31 33 35 (kipepesi/simu ya moja kwa moja)
**e** knfp.info@gmail.com
**w** www.knfparms.go.ke

# Yaliyomo


**Shukurani** ........ **14**

**Dibaji** ........ **15**

**Utangulizi** ........ **16**

**Vifupisho na akronimi** ........ **17**

**Muhtasari wa yaliyoangaziwa** ........ **19**

**I. Utangulizi** ........ **22**

Tatizo la silaha ndogo ndogo nchini Kenya ........ 22

Matukio ya Kihistoria na Kieneo ........ 24

Sababu za kindani za kuenea kwa silaha ndogo ndogo ........ 27

Athari za silaha ndogo ndogo ........ 28

Mikakati ya usalama na usalimishaji silaha ........ 32

Mafanikio na Changamoto ........ 35

Madhumuni ya Mradi wa Kitaifa wa Uratibu wa Silaha ........ 38

Utaratibu na Upeo ........ 40

**II. Silaha ndogo ndogo na hisia kuhusu usalama** ........ **42**

Utangulizi ........ 42

Kuenea kwa silaha ndogo ndogo na namna zinavyotumika ........ 43

*Hisia kuhusu sababu za kuhitajika kwa silaha ndogo ndogo* ........ 43

*Makadirio ya umiliki wa bunduki nyumbani* ........ 47

*Hisia za umma* ........ 49

*Ufahamu kuhusu namna silaha zinapatikana* ........ 54

Viashirio vya hisia kuhusu athari za silaha ndogo ndogo ........ 60

*Vifo kutokana na kupigwa risasi na/au majeraha* ........ 60

*Athari za silaha ndogo ndogo* ........ 60

Mahali silaha ndogo ndogo zitokako na ziendako ........ 61

Gharama ya silaha ndogo ndogo ........ 66

Silaha ndogo ndogo, uhalifu na ghasia: uchunguzi wa masaibu ya waathiriwa . . . 66
*Maoni ya jumla* . . . 66
*Masaibu ya waathiriwa* . . . 68

**III. Uwezo wa Kenya kudhibiti silaha ndogo ndogo** . . . **73**
Utangulizi . . . 73
Mafanikio kwa ujumla ya kudhibiti silaha haramu . . . 73
Taratibu za kudhibiti mipaka . . . 77
Kupunguza changamoto kuhusu silaha haramu . . . 79
*Usalimishaji silaha* . . . 79
*Kukuza ufahamu kuhusu silaha ndogo ndogo* . . . 84
*Kukamatwa na kufikishwa mahakamani* . . . 86
*Kitengo maalum cha polisi* . . . 91
*Mfumo wa kutoa tahadhari ya mapema* . . . 93
Changamoto zinazokabiliwa katika kupambana na silaha haramu . 94
Fikra za umma kuhusu mafanikio ya juhudi za kudhibiti silaha ndogo ndogo . . . 96

**IV. Maamuzi na Mapendekezo** . . . **98**
Maamuzi . . . 98
Mapendekezo . . . 104
*Kufuatilia na kuelewa hali halisi ya tatizo* . . . 104
*Mazingira ya kitaasisi* . . . 105
*Hatua za kupunguza kupatikana kwa bunduki* . . . 107
*Hatua za kuwashughululikia wahasiriwa* . . . 108
*Hatua zenye misingi ya utaratibu wa kimaendeleo* . . . 109

**V. Utaratibu au Methodolojia** . . . **111**
Utangulizi . . . 111
Utaratibu wa Sampuli . . . 112
*Mfumo wa sampuli kwa uchunguzi wa nyumba* . . . 112
*Sampuli kwa mahojiano ya CSO na LEA* . . . 113
*Mfumo wa Sampuli kwa FGDs* . . . 113
*Eneo-lengwa* . . . 113
Kukagua, kuthibitisha na kupima takwimu . . . 116
Vifaa au njia zilizotumika . . . 117

Mafunzo na ukusanyaji takwimu . . . . . 118
*Namna mahojiano yalivyofanywa* . . . . . 118
*Uingizaji takwimu kwenye tarakilishi na ukaguzi* . . . . . 119
Matokeo ya demografia . . . . . 119
*Uwakilishi wa jinsia* . . . . . 119
*Umri wa wahojiwa* . . . . . 120
*Elimu* . . . . . 121

**Kiambatisho 1: Sampuli ya ugawaji kwa kaunti** . . . . . **122**

**Kiambatisho 2: Utaratibu au methodolojia ya makadirio ya umiliki bunduki katika Jedwali 2.3** . . . . . **123**
Mkokotoo au kufanywa kwa hesabu . . . . . 124
*Kaunti ambazo Hazikuchunguzwa* . . . . . 124

**Kiambatisho 3: Silaha zilizopatikana mwaka 2010** . . . . . **126**

**Tanbihi** . . . . . **127**

**Bibliografia** . . . . . **132**

# Orodha ya ramani, michoro na jedwali


Ramani 1.1 Mikoa ya Kenya, 2004 .......... 26

Ramani 1.2 Kaunti kwa kiwango cha uathirikaji .......... 44

Mchoro 2.1 Hisia kuhusu umiliki wa bunduki kwa ulinzi wa jamii, uwezekano wa kuathirika, kwa kaunti na makundi (LEAs na CSOs) .......... 45

Mchoro 2.2 Hisia kuhusu umiliki wa bunduki nchini, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 50

Mchoro 2.3 Hisia kuhusu urahisi wa upatikanaji wa bunduki, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 56

Mchoro 2.4 Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba silaha zenye bapa ni kawaida katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 57

Mchoro 2.5 Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba bastola ndogo ni nyingi katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 57

Mchoro 2.6 Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba bunduki za marisaa ni nyingi katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 57

Mchoro 2.7 Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba bunduki za rashasha ni nyingi katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 58

Mchoro 2.8 Asilimia ya wahojiwa inayoonyesha nchi jirani kama chanzo cha silaha na risasi haramu katika maeneo yao, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 62

Mchoro 2.9 Asilimia ya wahojiwa inayoonyesha wauzaji silaha haramu/wafanyabiashara ya silaha haramu kuwa chanzo kikuu cha silaha na risasi hizo katika maeneo yao, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) . . . 62

Mchoro 2.10 Asilimia ya wahojiwa wanaoonyesha maghala ya serikali ya silaha (polisi, jeshi) kama chanzo kikuu cha silaha na risasi haramu kwenye maeneo yao, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs,na CSOs) . . . 63

Mchoro 2.11 Hisia za wahojiwa wa HH kuhusu usalama mwaka 2011 ikilinganishwa na mwaka moja uliopita, kwa uathirikaji wa kaunti . . . 67

Mchoro 2.12 Tajriba ya kuathiriwa na uhalifu miongoni mwa wahojiwa wa HH mwaka 2011, kwa uathirikaji wa kaunti . . . 68

Mchoro 2.13 Eneo la uhalifu uliokumba wahojiwa wa HH, kwa uathirikaji wa kaunti . . . 69

Mchoro 2.14 Silaha zinazotumika katika visa vya uhalifu au ghasia . . . 70

Mchoro 3.1 Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kwamba Kenya imefanikiwa katika kudhibiti silaha ndogo ndogo katika muda wa miaka mitano iliyopita, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 74

Mchoro 3.2 Asilimia ya wahojiwa wanaoona mikakati ya kudhibiti silaha nchini Kenya ni duni au inafaa, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 76

Mchoro 3.3 Maoni ya wahojiwa kuhusu kuwa na habari kuhusu angalau mkataba mmoja wa kimataifa kuhusu udhibiti wa silaha, kwa makundi (CSOs na LEAs) . . . 76

Mchoro 3.4 Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa visa fulani vya uhalifu vimekithiri mpakani, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 78

Mchoro 3.5 Asilimia ya wahojiwa ambao wanafahamu kuhusu kampeni za eneo lao za upokonyaji silaha, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) ......... 80

Mchoro 3.6 Asilimia ya wahojiwa waliokubaliana na taarifa fulani kuhusu matokeo ya kampeni za mashinani za usalimishaji silaha, kwa makundi (LEAs na CSOs) ........ 82

Mchoro 3.7 Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa serikali huweka kumbukumbu zifaazo za silaha zake, kwa makundi (LEAs na CSOs) ................................ 83

Mchoro 3.8 Asilimia ya wahojiwa ambao wamehudhuria/kuhusishwa/kuona matangazo yoyote ya kuimarisha uhamasishaji kuhusu silaha ndogo ndogo kwa makundi (LEAs na CSOs) ........................................ 85

Mchoro 3.9 Asilimia ya wahojiwa waliotaja njia mbalimbali za uhamasishaji, kwa makundi (LEAs na CSOs) ............. 85

Mchoro 3.10 Asilimia ya wahojiwa ambao waliorodhesha baadhi ya njia za uhamasishaji kuhusu silaha ndogo ndogo na nyepesi kuwa zinafaa, kwa makundi (CSOs na LEAs) ..... 86

Mchoro 3.11 Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba uhalifu unaohusisha silaha unashtakiwa ipasavyo, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .......... 87

Mchoro 3.12 Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa tatizo linalohusu uendeshaji mashtaka wa visa vya uhalifu vinavyohusu silaha yanatokana na ukosefu wa rasilimali na siyo utendakazi, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) ......................... 89

Mchoro 3.13 Asilimia ya wahojiwa waliosema kwamba kesi zinazohusu silaha ndogo ndogo katika maeneo yao hazifikishwi mahakamani, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) .................... 89

Mchoro 3.14 Asilimia ya wahojiwa waliosema kuwa kuna haja ya kuwepo kwa kitengo maalum cha polisi cha silaha ndogo ndogo, kwa makundi (LEAs na CSOs) ............. 91

Mchoro 3.15 Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa kuna uhusiano mzuri kati ya mashirika ya kudumisha sheria na jamii, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 92

Mchoro 3.16 Asilimia ya wahojiwa wanaoonelea kwamba njia kadhaa za mawasiliano kuwa zinazofaa, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 95

Mchoro 3.17 Asilimia ya wahojiwa wanaoonelea kwamba changamoto zinazokumba mashirika ya kudumisha sheria ni za muhimu, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 95

Mchoro 3.18 Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kwamba Kenya inafaulu katika juhudi zake za kudhibiti silaha ndogo ndogo haramu, kwa makundi (LEAs na CSOs) . . . 96

Mchoro 5.1 Mgawanyo wa wahojiwa kijinsia, kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs) . . . 120

Mchoro 5.2 Kiwango cha elimu cha wahojiwa (HHs na CSOs) . . . 120

Mchoro 5.3 Mgawanyo wa sampuli ya HH, kwa umri . . . 121

Mchoro 5.4 Mgawanyo wa sampuli ya LEA, kwa umri . . . 121

Mchoro 5.5 Mgawanyo wa sampuli ya CSO, kwa umri . . . 121

Jedwali 1.1 Athari za matumizi mabaya ya silaha ndogo ndogo kwa maendeleo ya binadamu . . . 30

Jedwali 1.2 Takwimu za uhalifu kimkoa/kitengo 2009 na 2010 . . . 31

Jedwali 2.1 Sababu za kumiliki bunduki kulingana na maoni ya HHs na LEAs (%) . . . 43

Jedwali 2.2 Majibu kwa swali: 'Je, wewe ama yeyote kwa kaya yako anamiliki bunduki?' (%) . . . 49

Jedwali 2.3 Makadirio ya umiliki wa bunduki katika HH kote nchini Kenya (hesabu zimefanywa kamili kukaribia 10,000) . . . 53

Jedwali 2.4 Baadhi ya bunduki/silaha zilizotajwa katika FGDs . . . 59

Jedwali 2.5 Hisia za wahojiwa kuhusu mahala silaha zinapohifadhiwa (LEAs na CSOs) . . . 59

Jedwali 2.6 Hisia za wahojiwa zinazoonyesha ni mara ngapi vifo au majeraha hutokea kupitia mtutu wa bunduki (LEAs na CSOs) . . . 60

Jedwali 2.7 Njia za ulanguzi na namna ya usafirishaji . . . 46

Jedwali 2.8 Makadirio ya gharama ya bunduki (KES) . . . 65

Jedwali 2.9 Hisia za viwango vya usalama (maeneo na saa mbalimbali) . . . 67

Jedwali 2.10 Aina ya uhalifu au ghasia (majibu kadhaa) . . . 71

Jedwali 2.11 Wale walioambiwa kuhusu visa vya uhalifu/vya kutumia nguvu . . . 71

Jedwali 2.12 Sababu za kutoripoti visa vya vya uhalifu/vya kutumia nguvu . . . 72

Jedwali 3.1 Athari za usalimishaji silaha kwa usalama wa wakaazi . . . 81

Jedwali 3.2 Kesi zinazohusu utumiaji wa bunduki/risasi na wahalifu katika mwaka mmoja na matokeo ya kesi hizo (2010/11) . . . 90

Jedwali 5.1 Uteuzi wa viwango vya juu-, kadiri-, na chini vya uathirikaji wa kaunti kote nchini Kenya kwa uchunguzi huu . . . 114

Jedwali 5.2 Ugawaji wa sampuli ya nyumba katika matabaka na kaunti . . . 115

Jedwali 5.3 Ugawaji wa sampuli ya HHs . . . 116

Jedwali 5.4 Matokeo ya ukusanyaji takwimu kwa sampuli tatu za idadi ya watu . . . 117

Jedwali A1 Sampuli ya ugawaji kwa kaunti . . . 122

Jedwali A2 Silaha zilizopatikana mwaka 2010 . . . 126

# Shukurani

Kufanyika kwa uchunguzi huu kuliwezekana kutokana na kujitolea kwa kundi kubwa la wataalamu. Kwanza kabisa tungependa kutoa shukrani zetu kwa ofisi nzima ya KNFP—David Mwole Kimaiyo (mkurugenzi), John Patrick Ochieng (naibu mkurugenzi), Adonijah Dianga (afisa wa silaha), Esther Wamuyu Waiganjo, na Dorcus Wambui Irungu—kwa ari ya ushiriki wao wa dhati katika mradi huu na Kamati Kuu ya Uendeshaji ya Kitaifa kwa usaidizi na maoni thabiti katika awamu zote za mradi. Tungependa pia kumshukuru Profesa Kennedy Mkutu kwa kuwezesha kufanyika kwa warsha ya uthibitishaji ambayo ilichangia masuala muhimu kwenye rasimu ya kwanza ya ripoti hii.

Shukrani pia zimwendee Wilfred Odoke, ambaye alilisaidia kundi la uchunguzi kwa tekinolojia ya habari na usimamizi wa takwimu wakati wote wa kazi yao walipokuwa nyanjani, na kundi lake la wafanyakazi wa kuingiza takwimu mitamboni; kwa wasimamizi na makarani ambao walifanya zaidi ya mahojiano 2,000 katika kaunti 31, wakati mwingine wakikumbana na changamoto kubwa nyanjani; kwa madereva walioandamana na makundi hayo; na kwa watafsiri ambao walihakikisha kwamba hojaji na ripoti ya mwisho zitapatikana kwa Kiingereza na Kiswahili.

Tungependa pia kutoa shukrani kwa Savannah de Tessières na Matthias Nowak wa Small Arms Survey, kwa ushiriki wao katika sehemu mbalimbali za mafunzo na kazi nyanjani, pamoja na Jordan Shepherd, ambaye alikagua usahihi wa ripoti hii, na Alex Potter, ambaye alihariri matini. Kadhalika tungependa kumshukuru Alessandra Allen na Martin Field wa Small Arms Survey kwa kuhakikisha kiwango cha juu cha ripoti hii, na pia Joan Simba na Esther Munguti kwa kutafsiri kwa Kiswahili.

Hatimaye, na cha muhimu vilevile, tunawashukuru wote waliohusika katika shughuli ya ukusanyaji takwimu; wahojiwa kutoka kaya, mashirika ya kijamii, na mashirika ya udumishaji sheria; na watoaji habari wakuu na washiriki kwenye makundi mahususi. Ni kupitia ushiriki wao wa hiari ambapo msingi huu wa thamani wa takwimu umeweza kupatikana.

# Dibaji


Wizara ya Usimamizi wa Mikoa na Usalama wa Nchi, kupitia kwa Shirika la Kitaifa Kuhusu Silaha Ndogo Ndogo(KNFP), hivi majuzi iliandaa mpango madhubuti wa kitaifa ili kufanya uratibu na uchunguzi, kuambatana na mamlaka yake ya kutekeleza Mwafaka wa Nairobi wa Aprili 2004 na Mpango wa Utekelezaji wa Umoja wa Mataifa wa Julai 2001.

Utafiti huu wa kitaifa ulichunguza hali na hisia za watu kuhusu silaha ndogo ndogo na nchini Kenya, huku matokeo yakilipa shirika la KNFP habari muhimu zinazoweza kutumika kwa utekelezaji unaofaa wa Mpango wake wa Kitaifa wa Utekelezaji na Mpango wa Mikakati wa 2010/11 – 2014/15. Uchunguzi huu unawakilisha jitihada muhimu na unasaidia juhudi nyingine ambazo serikali na wadau wengine wamefanya hadi kufikia sasa kuafikia amani na usalama.

Mapigano mengi na ya muda mrefu ambapo silaha hutumika miongoni mwa mataifa mengi jirani na Kenya yamesababisha kuwepo kwa kiasi kikubwa cha silaha na risasi zisizodhibitiwa na serikali. Kuwepo kwa upatikanaji na utumiaji wa silaha haramu ndogo ndogo kunaendelea kutishia amani nchini. Ili kutekeleza mipango madhubuti inayohusiana na usalama, ipo haja ya kuwepo kwa takwimu sahihi na utaratibu unaohusika na suala hilo ili kukabiliana na tishio hili, katika juhudi za kupunguza ghasia zinazohusu silaha, na kuimarisha maendeleo.

Kwa hivyo ningelipenda kuishukuru taasisi ya Small Arms Survey iliyoko Geneva kwa usaidizi wa kiufundi na kifedha katika utafiti huu. Vile vile, twaishukuru Serikali ya Denmaki na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali walioshirikiana nasi katika miradi na maazimio yaliyomo katika Mpango wa Mikakati 2010/11 – 2014/15.

Hata hivyo, kuna mengi zaidi ambayo yanaweza kufanywa katika nyanja ya amani na usalama, na kwa kiasi kikubwa, kuhusu tatizo la silaha ndogo ndogo nchini Kenya. Hivyo basi, serikali inahimiza kufanywa kwa utafiti zaidi na hatua zaidi za kuingilia kati suala hili, kama inavyopendekezwa kwenye ripoti hii.



**E. Mutea Iringo, EBS**

**Kaimu Katibu – Usimamizi wa Mikoa na Usalama wa Nchi**

# Utangulizi

Uchunguzi wa kitaifa ili kuratibu silaha hutoa takwimu zenye ushahidi kwa waundaji sera na wataalamu wengine ili kuwawezesha kupanga ajenda na hatua za uingiliaji kati.

Uchunguzi wa kitaifa wa aina hii unahitaji kudumisha msimamo wake, kujitolea kisiasa, kufanywa kwa njia ya kitaalam, kheri njema na kuweko kwa kiasi kikubwa cha rasilimali (za kibinadamu na pia za kifedha). Tutawaachia waandishi wakuu wa utafiti kutoa shukurani kwa wengi waliochangia utafiti huu lakini ambao hawakutajwa hapa. Hata hivyo, tungependa kusisitiza jukumu muhimu lililotekelezwa na Kamati Kuu ya Kitaifa ya Uongozaji ya Kuendeleza Amani na Usimamizi wa Mizozo ya shirika la KNFP katika kutoa mwongozo na kuimarisha uwajibikaji, pamoja na ufadhili mkubwa kutoka kwa serikali ya Denmark ili kuhakikisha kufanikiwa kwa mradi huu. Isitoshe, tungependa kuwashukuru Manasseh Wepundi, Eliud Nthiga, Eliud Kabuu, Anna Alvazzi del Frate, na Ryan Murray kwa kufanya kazi kwa bidii na kwa kujitolea kwao. Mwishowe, tunashukuru usimamizi wa KNFP, hususan John Patrick Ochieng na makao makuu, kwa usaidizi wao nchini.

Mara nyingi, uchunguzi wa aina hii hutekelezwa kwa namna duni au bila kutumia maadili bora. Serikali ya Kenya haijachukulia juhudi hii kuwa kama tu tendo la 'kuweka alama ya usahihi' ili kutii mwongozo au masharti yaliyowekwa chini ya Mpango wa Utekelezaji wa Silaha Ndogo Ndogo wa Umoja wa Mataifa, au Azimio la Nairobi na Mwafaka wa Nairobi unaosimamiwa na Kituo cha Kanda cha Silaha Ndogo Ndogo na Nyepesi, (RECSA), lakini imejitolea kutumia taarifa na matokeo ya utafiti huu ili kuarifu sera na mipango yake katika miezi na miaka ijayo.

Tunatumaini kwamba shughuli hii ya ushirikiano itakuwa kielelezo cha uchunguzi madhubuti kitakachofaa kuigwa na kutumiwa na wengine kama mfano katika eneo la RECSA, na mbali zaidi, ikiwa ni pamoja na kwingineko barani, na hata nje ya Afrika.

**David M. Kimaiyo, CBS, DSM**
**Mkurugenzi, KNFP/SALW**

**Eric G. Berman**
**Mkurugenzi Mkuu, Small Arms Survey**

# Vifupisho na akronimi

| | |
|---|---|
| ASTU | Anti Stock Theft Unit – Kitengo cha kukabiliana na Wizi wa Mifugo |
| CID | Criminal Investigation Department – Idara ya Upepelezi wa Jinai |
| CSO | Civil society organization – Shirika la kutetea haki za jamii |
| DTF | District task force – Jopo kazi la Wilaya |
| EAC | East African Community – Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| FGD | Focus group discussion – Kundi Mahususi la Mjadala |
| HH | Household – Kaya/nyumba |
| IDP | Internally displaced person – Mtu aliyepoteza Makao Nchini |
| IED | Improvised explosive device- Kilipukaji kilichotengenezwa haraka/papo hapo/kwa ufaraguzi |
| ISS | Institute for Security Studies –Taasisi ya Mafunzo ya Usalama |
| KES | Kenyan shilling – Shilingi ya Kenya |
| KFS | Kenya Forest Service – Huduma ya Misitu Nchini Kenya |
| KII | Key informant interview – Mahojiano ya mtoa habari mkuu |
| KNFP | Kenya National Focal Point on Small Arms and Light Weapons – Shirika la Kitaifa la Kushughulikia Silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi |
| KPR | Kenya Police Reserve – Polisi wa Akiba wa Kenya |
| KPRs | Members of the KPR – Maafisa wa Polisi wa Akiba wa Kenya |
| KWS | Kenya Wildlife Service – Shirika la Huduma kwa Wanyamapori |
| LEA | Law enforcement agent –Afisa anayedumisha sheria |

| | |
|---|---|
| Nairobi Declaration | Azimio la Nairobi kuhusu tatizo la ueneaji wa silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi katika Eneo la Maziwa Makuu na Upembe wa Afrika |
| Nairobi Protocol | Mwafaka wa Nairobi wa Uzuiaji, Udhibiti na Upunguzaji wa silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi katika Eneo la Maziwa Makuu na Upembe wa Afrika. |
| National Action Plan | Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji nchini Kenya kwa Udhibiti na Usimamizi wa Silaha |

| | |
|---|---|
| National Arms Mapping | Uratibu wa Kitaifa wa silaha haramu ndogo ndogo na silaha nyepesi |
| NSC | National Steering Committee on Peace-building and Conflict Management – Kamati Kuu ya Kitaifa ya Uongozi kuhusu Uimarishaji Amani na Usimamizi wa Mizozo |
| PTF | Provincial task force – Jopo kazi la mkoa |
| Programme of Action | Mpango wa Utekelezaji wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia, Kupambana na Kuangamiza biashara haramu ya silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi kwa kila hali |
| RECSA | Regional Centre on Small Arms and Light Weapons – Kituo cha Kanda kwa Silaha Ndogo Ndogo |
| RECSA Best Practice Guidelines | Mwongozo wa Kanuni Bora kuhusu upunguzaji silaha kwa eneo la Kituo cha Kanda kwa silaha ndogo ndogo |
| SALW | Small Arms and Light Weapons sihala ndgo ndgo |
| SLDF | Sabaot Land Defence Force – Kundi la wapiganaji la Sabaot Land Defence Force |
| SRIC | Security Research and Information Centre – Kituo cha Utafiti wa Usalama na Habari |
| UNDP | United Nations Development Programme-Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| UNODC | United Nations Office on Drugs and Crime – Ofisi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Dawa za Kulevya na Uhalifu |
| WPDC | Wajir Peace and Development Committee – Kamati ya Amani na Maendeleo ya Wajir |

# Muhtasari wa yaliyoangaziwa

Kenya imekumbwa na athari za utumizi mbaya wa silaha ndogo ndogo kwa miaka mingi, lakini ghasia ambazo hazijawahi kutokea zilizoibuka baada ya uchaguzi mkuu wa Disemba 2007 ziliweka suala la upunguzaji silaha ndogo ndogo katika kiwango cha juu zaidi kwenye ajenda ya kitaifa. Serikali ya Kenya ilianzisha mipango kadhaa muhimu, kama vile kubuniwa kwa Shirika la Kitaifa la Kushugulikia Silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi (KNFP) ambalo ni kurugenzi kwenye Wizara ya Ofisi ya Rais, Wizara ya Usimamizi wa Mikoa na Usalama wa Nchi. Licha ya hatua kubwa kupigwa, juhudi za kudumisha sheria ili kudhibiti kuenea kwa silaha ndogo ndogo nchini zingali zinakabiliwa na changamoto kubwa.

Idadi ya silaha haramu na kuenea kwake nchini Kenya ilikuwa kusudi muhimu la Uratibu wa Kitaifa wa mwaka 2003 wa silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi, uliofanywa na KNFP, na ambao ulisababisha ustawishaji wa Mpango Tekelezi wa Kitaifa wa Kenya kuhusu Udhibiti na Usimamizi wa Silaha (KNFP, 2006). Hata hivyo, kwa miaka minane iliyofuata hakukuwepo na utafiti uliojumuisha taifa zima, huku utafiti uliofanywa kuhusu silaha ndogo ndogo nchini ukizingatia zaidi maeneo ya kaskazini mwa nchi (Kaskazini mwa Bonde la Ufa, Kanda ya Juu ya Mashariki, na Mkoa wa Kaskazini Mashariki).

Uchunguzi huu wa pamoja wa Serikali ya Kenya na shirika la Small Arms Survey lenye makao yake Geneva nchini Uswizi, unanuia kukadiria ueneaji wa silaha ndogo ndogo nchini Kenya (kuratibu maeneo zilizoko, zitokako, na zinavyosafirishwa), na kukadiria uwezo wa wadau mbalimbali wanaohusika na juhudi za kudhibiti silaha ndogo ndogo, na za kuendeleza amani nchini. Kwa lengo hili, uchunguzi huu ulitumia mchanganyiko wa mifumo ya taratibu bora na zenye kutumia idadi zifaazo – uliohusisha takriban mahojiano 2,500 ya wakaazi wa kaya, wawakilishi wa mashirika ya kutetea haki za jamii, maafisa wa kudumisha sheria, na watoaji habari wengine wakuu kutoka kaunti 32 kati ya kaunti 47 nchini Kenya. Kijiografia,

sampuli zilijumuisha kaunti zote zinazotambuliwa kuwa zinaathirika kwa kiwango kikubwa (zile ambako silaha ndogo ndogo zimeenea sana, zile zenye kiwango kikubwa cha jamii za kuhamahama zenye mwelekeo wa kumiliki silaha ndogo ndogo ili kulinda mifugo wao, maeneo ambapo inaonekana kuwa silaha zitaibuka, maeneo yenye watu wengi mijini ambako viwango vya visa vya uhalifu ni vya juu), pamoja na wawakilishi kutoka maeneo yanayotambuliwa kuwa yanaathirika kwa kiwango cha kadiri, na kiwango cha chini.

Matokeo makuu ya utafiti huu ni yafuatayo:

- Kati ya bunduki 530,000 na 680,000 huenda ziko mikononi mwa raia kote nchini.
- Licha ya fikra kwamba idadi ya bunduki nchini imepungua, maeneo kadhaa, yakiwemo maeneo kama Mt Elgon na Bonde la Ufa ambako mipango ya upokonyaji silaha imetekelezwa, yamethibitishwa kuwa na ongezeko kubwa la umiliki wa bunduki tangu 2003.
- Kipindi cha ghasia zilizozuka wakati wa uchaguzi mkuu wa Desemba 2007 kiliwaachia watu wengi madhara, huku wahojiwa wengi wa kaya wakisema kwamba wao huhisi ukosefu wa usalama zaidi nyakati za uchaguzi.
- Takriban asilimia 20 ya wahojiwa wa kaya waliathiriwa na visa vya uhalifu au ghasia katika kipindi cha mwaka uliotangulia kuhojiwa kwao, lakini idadi mara dufu walihisi kwamba kulikuwa na uwezekano wa wao kuwa waathiriwa wa ghasia na/au uhalifu katika mwaka utakaofuatia.
- Zaidi ya theluthi moja ya waathiriwa walivamiwa kwa kutumia bunduki
- Kuna tofauti fulani kati ya maoni ya mashirika ya kudumisha sheria na yale ya kutetea haki za jamii kuhusu matokeo ya juhudi za wakati huu za kupunguza kuenea kwa bunduki na uboreshaji usalama, huku mashirika ya kudumisha sheria yakiwa na matumaini zaidi kuliko mashirika ya kutetea haki za jamii.

Kutokana na matokeo muhimu yaliyoko hapo juu, utafiti huu unatoa mapendekezo kadhaa kuhusu ufuatiliaji na kueleweka kwa tatizo hili, mabadiliko ya mazingira ya kitaasisi, hatua za kupunguza upatikanaji wa silaha ndogo

ndogo na silaha nyepesi, na hatua za kuwashughulikia waathiriwa, na hatua za kushughulikia masuala ya maendeleo kwa kutumia mfumo wenye utaratibu mahsusi.

Uchunguzi huu unajumuisha sura tano. Ya kwanza inashughulikia usuli na inatoa taarifa tangulizi kuhusu utafiti. Ya pili na ya tatu zinajadili matokeo kutoka kwa uchunguzi wa nyumba au kaya, maafisa wa kudumisha sheria na wanachama wa mashirika ya kutetea haki za jamii, pamoja na habari stahilifu zilizotoka kwa taarifa za majadiliano ya makundi mahususi, na mahojiano ya watoa habari wakuu kuhusu mielekeo na miendendo ya silaha, vyanzo na usafirishaji wake, na juhudi zinazoendelea ambazo zinafanywa na serikali ili kupunguza ueneaji wa bunduki. Sura ya nne inajumuisha hitimisho au maamuzi na mapendekezo, nayo sura ya tano inaelezea utaratibu uliotumiwa kwenye baadhi ya vipengee vya utafiti, kwa undani.

# I. Utangulizi

## Tatizo la silaha ndogo ndogo nchini Kenya

Kenya imepambana na ukosefu wa usalama kwa muda mrefu, kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya ueneaji wa silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi.[1] Masuala ya ndani pamoja na ya nje yanachangia kukua kwa changamoto zinazohusiana na bunduki zinazoikumba nchi hii. Nchini, sababu za kijamii, kiuchumi na kisiasa zimechangia haja na kuenea kwa silaha ndogo ndogo.[2] Ukosefu wa hali thabiti ya kisiasa unaokithiri, na mapigano ambapo silaha hutumika katika nchi zilizo jirani na Kenya, kadhalika zimechangia tatizo la silaha ndogo ndogo linalokabili nchi hii, ikitiliwa maanani hali legevu ya udhibiti wa mipaka.

Madhara ya silaha ndogo ndogo na utumiaji mbaya wa silaha hizo limekuwa tatizo sugu na la muda mrefu kote nchini Kenya. Jamii za wafugaji wanaohamahama, ambapo kuna maafisa wa polisi wachache mno, pamoja na changamoto nyingi (kama vile mizozo kuhusu kupatikana kwa malisho na maji kwa mifugo wao) zimeathiriwa sana. Hali hii huzikumba haswa jamii zilizoko Kaskazini Mashariki, Kanda ya Juu ya Mashariki na eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, yanayoaminika kuwa yameathiriwa vibaya sana na kuweko kwa idadi kubwa ya bunduki haramu, na ukosefu wa usalama. (Muchai, 2005, uk. 117–19). Miji kama vile Nairobi, Mombasa, Eldoret, Thika, na Kisumu pia imeathiriwa na biashara haramu ya silaha ndogo ndogo.

Viwango ambavyo havikuwa vimeshuhudiwa awali vya ghasia ambapo silaha zilitumika na vilivyoibuka baada ya uchaguzi mkuu wa Desemba 2007 nchini Kenya vililisukuma tatizo la silaha ndogo ndogo juu zaidi kwenye ajenda ya kitaifa. Kulingana na ripoti ya Tume Iliyochunguza Ghasia za Baada ya Uchaguzi (inayofahamika pia kama Ripoti ya Waki kwa sababu ya

mwenyekiti wake Jaji Philip Waki), jumla ya watu 1,133 walifariki kutokana na ghasia hizo. Zaidi ya Wakenya 3,500 walipata majeraha, na zaidi ya mali 100,000 za kibinafsi kuharibiwa. Ripoti hiyo ya Waki ilisema kwamba 'risasi zilisababisha majeruhi 962, huku 405 kati yao wakifariki' (CIPEV, 2008, uk. 345–46). Takwimu hizi zinadhihirisha kiwango cha ukali wa ghasia hizo, ambazo zilizidi kiwango kilichoshuhudiwa kwenye ghasia za mwaka 1992 ambapo kulitokea zaidi ya vifo 779 na majeraha 654] (CIPEV, 2008, uk. 304). Ingawaje ghasia za 1992 na 1997 zilisababisha zaidi ya watu 600,000 kupoteza makao nchini (IDPs) (KHRC, 2011, uk. 12), jumla ya IDPs kutokana na ghasia za 2007/08 ni idadi hiyohiyo (IDMC, 2008, uk. 41).

Ghasia zinazohusiana na uchaguzi za 2007/08, kuachwa bila makao kwa wengi, na ukosefu wa usalama katika sehemu nyingi unaaminika ulichochea mahitaji mapya ya silaha ndogo ndogo, hasa katika eneo la kati la Mkoa wa Bonde la Ufa. Ingawaje silaha nyingi butu kama visu na mapanga zilitumiwa kuzua ghasia hizo na mauaji yaliyofuatia, kuna ripoti kwamba jamii zilitafuta– na zikafanikiwa kupata – bunduki za kisasa nyingi tu. Pamoja na haja hii kubwa ya silaha, kuna wasiwasi wa kuweko kwa uwezekano wa kuenea kwa makundi yenye silaha, na ukuaji wa makundi yaliyopo ya wahuni. Kampeni hii ya kutafuta upya silaha miongoni mwa jamii, iliyotangazwa sana sana kupitia vyombo vya habari, inathibitisha haja ya kuchukuliwa kwa hatua kabambe za udhibiti silaha, zitakazoandamana na juhudi za kuendeleza amani.[3]

Tishio la ueneaji wa silaha ndogo ndogo nchini Kenya kwa sheria na utangamano, na amani na usalama – ndani ya nchi ya Kenya na pia katika kanda hii – lilitiwa mkazo mnamo Desemba 2009 wakati polisi wa Kenya walipogundua risasi 100,000 kwenye makao ya kibinafsi huko Narok, mji ulioko takriban kilomita 142 kaskazini magharibi mwa mji mkuu, Nairobi. Zaidi ya risasi myingine 30,000[4] baadaye zilipatikana hapohapo. Kufikia wakati wa kuandika ripoti hii, maswali mengi yalikuwa hayajapata jawabu, lakini jambo moja lilikuwa wazi: risasi nyingi kati ya hizi zilitengenezewa humu humu nchini, na zilitoka kwenye kiwanda cha risasi cha Kenya Ordnance Factories Corporation, chenye makao yake huko Eldoret (*Daily Nation*, 2010b; KOFC, n.d.). Jinsi mfanyabiashara huyo wa kibinafsi alivyopata risasi hizo ni sehemu ya uchunguzi unaoendelea, na

kesi iliyoko mahakamani. Isitoshe, inaaminika na wengi kwamba maafisa wa sekta ya usalama na maafisa wa serikali walihusika katika mbinu za kugeuza mkondo wa silaha na kumwelekezea mfanyabiashara huyo, au walipuuza alichokuwa akifanya. Kulingana na ripoti za vyombo vya habari nchini Kenya, kupatikana kwa risasi hizo kuliashiria kuwepo kwa mtandao wenye visehemu vingi wa magendo ya silaha, ambao huenda unasambaza silaha katika eneo hili. (*Daily Nation*, 2010b).[5] Madokezo ya awali yaliashiria uwezekano wa kuhusika kwa maafisa wa usalama wa Kenya kwenye makundi ya ulanguzi wa silaha, ambayo masoko yalidaiwa kuwa nchi jirani, magenge ya wahalifu na jamii za wafugaji wa kuhamahama nchini Kenya (Nation TV, 2010).

Ni katika muktadha huu ambapo utafiti huu ulifanywa. Lakini kabla ya kuendelea, ni muhimu kutilia maanani muktadha wa kihistoria na kieneo wa ueneaji wa silaha ndogo ndogo.

## Matukio ya Kihistoria na Kieneo

Kuenea kwa silaha ndogo ndogo katika kanda ya Afrika Mashariki kulianzia kabla ya ukoloni wa mataifa ya Ulaya katika karne ya 19. Ulanguzi wa silaha katika maeneo ya bara yalitokana na biashara iliyokita mizizi ambayo ilichangia kuongezeka kwa visa vya uvamizi ili kunyakua watumwa, mifugo, pembe za ndovu, na kumbukumbu nyingine za uwindaji. Wavamizi hao walitoka Ethiopia, na wengine walikuwa wafanyabiashara wa Kiarabu (Wepundi, Ndung'u, na Rynn, 2011, uk. 4). Nyakati hizo, masoko ya bunduki yalipatikana huko Maji, kusini magharibi mwa Ethiopia, na risasi zilitumiwa kama sarafu nchini humo (Mburu, 2002, uk. 4–5). Waingereza walijitahidi kuyashinda na kuyatuliza makundi pinzani ya wenyeji kwenye maeneo ya mipakani nchini Kenya, Uganda, Sudan, na Ethiopia (Collins, 2006, uk. 16–22).[6]

Changamoto za sasa kuhusiana na ukosefu wa usalama mijini na ueneaji wa silaha ndogo ndogo nchini Kenya zina asili zake katika mapigano ya Mau Mau yaliyopinga ukoloni katika miaka ya 1950. Yaaminika kwamba wapiganaji wa Mau Mau walianzisha utumizi wa silaha haramu katika eneo la Nairobi na Mkoa wa Kati (Katumanga na Cliffe, 2005, uk. 5).

Kuanguka kwa utawala wa Idi Amin mnamo mwaka wa 1979 kulizua uporaji wa maghala ya silaha katika kambi za kijeshi kaskazini mwa Uganda, na kupelekea kuenea kwa silaha ndogo ndogo katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa. Vile vile kupinduliwa kwa serikali ya Mengistu Haile Mariam wa Ethiopia kulichangia ongezeko la mtiririko wa silaha ndogo ndogo katika eneo la Kaskazini mwa Kenya (Adan na Pkalya, 2005, uk. 47–48).

Ukosefu wa amani uliodumu kwa muda mrefu nchini Somalia tangu kung'olewa mamlakani kwa Rais Siad Barre mnamo mwaka wa 1991 pia umechangia tatizo la silaha ndogo ndogo nchini Kenya. Mapambano ya awali ya kudai kuunganishwa kwa Somali, ambayo pia yanafahamika kihistoria kama vita vya 'shifta' (au kiharamia) ya miaka 1963–67, yaliathiri Mkoa wa Kaskazini Mashariki nchini Kenya. Tatizo hilo la 'shifta' lilipungua taratibu mnamo miaka ya 1990, ilhali bunduki haramu zilisalia kuwa tatizo katika eneo hili (Murunga, 2005, uk. 148).

Lakini upeo wa kimataifa kuhusu kuenea kwa bunduki nchini Kenya hauwezi kupuuzwa. Kenya imeathiriwa sana na biashara haramu kupitia kwa njia zile zile zinazotumiwa kwa usafirishaji halali wa silaha, huku bandari ya Mombasa ikiwa mojawapo ya viingilio vinavyotumiwa na walanguzi (HRW, 2002, uk. 9). Silaha zinazokusudiwa kusafirishwa hadi nchi jirani zimeripotiwa kugeuzwa mkondo, na baadhi kusemekana kuwa zimetumika katika shughuli za ulanguzi wa dawa za kulevya (Sabala, 2002, uk. 38).

Miji ya mipakani iliyoorodheshwa kama vituo ambavyo silaha ndogo ndogo husambazwa hadi Nairobi ni pamoja na Mandera, Moyale, El Wak, Lokichoggio, na Isiolo, na viko katika maeneo ya kaskazini mashariki, na kanda ya juu ya eneo la mashariki nchini Kenya (Sabala, 2002, uk. 38; HRW, 2002, uk. 11). Kwa kweli, mnamo mwaka 1997, polisi wa Kenya walifunga soko moja karibu na Isiolo ambalo lilifahamika kama soko kubwa la silaha, lakini biashara haramu ya silaha ndogo ndogo iliendelea (HRW, 2002, uk. 11). Kwa hivyo, kwa ujumla, eneo la kaskazini mwa Kenya – linalokabiliwa na changamoto mbalimbali za uzorotaji wa maendeleo, mizozo ya kikabila ya kupigania rasilimali, na kuwa karibu na nchi jirani zinazokumbwa na vita vya mara kwa mara – limekuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ueneaji wa silaha ndogo ndogo, huku makisio ya juu zaidi yakiwa kuweko kwa zaidi ya silaha 100,000 mwaka wa 2003 (Wairagu na Ndung'u, 2003, uk. 3).

Ramani 1.1 **Mikoa ya Kenya, 2004**




**Marejeo:** Ramani No. 4187, rev. 1, Umoja wa Mataifa, Idara ya Operesheni za Kudumisha Amani, Kitengo cha Uchoraji Ramani, Januari 2004

## Sababu za kindani za kuenea kwa silaha ndogo ndogo

Mifumo duni ya kudhibiti usalama inayokumbwa na ufisadi wakati mwingine, pamoja na kuweko kwa taratibu legevu mipakani na polisi wachache kwenye maeneo mengi kaskazini mwa Kenya, inakuza mazingira ya kuweko kwa ulanguzi wa silaha ndogo ndogo haramu, umilikaji na utumiaji wao (Kimaiyo na Nthiga, 2009, uk. 44–46). Kenya imeorodheshwa kuwa nambari 154 duniani, na nambari 35 barani Afrika katika Orodha ya Kukadiria Kiwango cha Ufisadi ya shirika la Transparency International ya mwaka wa 2010, na inaishinda Burundi pekee katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (TI, 2010, uk. 14).[7] Ingawaje nafasi ya Kenya imeboreka kulingana na Kiwango cha Kukadiria Ufisadi katika kanda ya Afrika Mashariki cha mwaka 2011, Kenya iliorodheshwa kama nchi ya nne ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye idadi ya chini zaidi ya visa vya rushwa, huku Idara ya Polisi ikiorodheshwa kama taasisi yenye visa vya ufisadi vingi zaidi nchini, na ya nne kwa ulaji rushwa Afrika Mashariki (TI-Kenya, 2011, uk. 2–3). Hata ingawa vipimo vilivyotumika ili kudhihirisha matokeo haya havilengi tu silaha ndogo ndogo, ukweli kwamba Wakenya hawawaoni polisi wao kuwa watu wanaofanya kazi kwa uwazi ni sababu inayozua wasiwasi, hasa kwa vile kazi kubwa ya idara hii ya udumishaji sheria ni kuhakikisha usalama na kusimamia maghala ya silaha, mbali na shughuli nyingine.

Kutodumishwa kwa usalama vilivyo na maafisa wa polisi katika maeneo mengi nchini Kenya kumechangia kukua kwa utamaduni wa kutaka kumiliki bunduki, hasa katika jamii za wafugaji wa kuhamahama. Hii inamaanisha kwamba bunduki ya aina ya Kalashnikov haichukuliwi kama bunduki tu, bali ni ishara kali ya mapigano na vurugu, pamoja na nguvu za kimabavu.[8] Kaskazini mwa Kenya, utamaduni wa umilikaji bunduki— au kuthaminiwa kwa bunduki kama kifaa muhimu sana miongoni mwa makundi mbalimbali— kumejenga hisia za watu wengi kwamba umilikaji bunduki ni haki ya kimsingi, jambo linalosababisha kila kabila kujitahidi kutaka kumiliki silaha nyingi zaidi ya mwenzake (Kamenju, Singo, and Wairagu, 2003, uk. 49–50).

Kwa sababu ya hali duni ya maisha, jamii zilizoko katika sehemu za Kenya ambazo hazijaendelea hujizatiti kutafuta silaha ndogo ndogo ili kuweza kupigania rasilimali chache zilizopo. Hii, pamoja na uhasama kati ya jamii, ambazo wakati mwingine huzua vurugu – kwa mfano wanapoibiana mifugo – huzipa jamii hizi moyo zaidi kutafuta silaha ili kujilinda. Na zaidi ya hayo, kwa vile serikali imeshindwa kutoa huduma zinazostahili, na kudumisha amani na utangamano kaskazini mwa Kenya, jambo hili limezifanya jamii zote kuamua kujihami kwa bunduki.

Miundo duni ya kiutawala huathiri vibaya ukosefu wa usalama na kuenea kwa silaha ndogo ndogo. Kwa mfano, akiorodhesha sababu kadhaa mahususi zinazochangia kutakikana sana kwa silaha ndogo ndogo miongoni na jamii za wafugaji wa kuhamahama, Mkutu (2008, uk. 6–9) anatoa hoja kuwa kiini cha kimsingi cha jambo hili ni uongozi duni, ilihali viini vingine ni kama vile kuzorota kwa tawala na taasisi za kitamaduni, kupungua kwa idadi ya mifugo, ulipaji mahari, na ukosefu wa ajira. Hata hivyo kuna vichocheo vingine, kama wizi wa mifugo, ambao huchukuliwa kama tatizo la kitamaduni la jadi katika jamii za wafugaji wa kuhamahama nchini Kenya, na katika eneo la Afrika Mashariki.

## Athari za silaha ndogo ndogo

Silaha ndogo ndogo huchangia pakubwa kudhihirisha ni nani washindi na nani walioshindwa kwa mapigano, na pia katika visa vya uvunjaji sheria. Mbali na kutumika kihalali ili kudumisha amani, silaha ndogo ndogo zinazotumika kiholela au zinazosambazwa hapa na pale kwa njia isiyo halali zimeathiri vibaya jamii husika, na watu wasio na hatia. Zinaongeza makali ya vita na hata pia muda wa mapigano.

Athari mojawapo ya silaha ndogo ndogo haramu ni kusabibishwa kwa watu kuhama bila wao kukusudia. Lakini wakimbizi hawa hawapatikani tu katika maeneo yanayokumbwa na fujo nyakati za uchaguzi katika eneo la katikati mwa Bonde la Ufa. Utafiti uliofanywa kaskazini mwa Kenya unadhihirisha kuwa mapigano ya jamii za kuhamahama ambapo silaha ndogo ndogo zilitumika yaliwalazimisha zaidi ya watu 160,000 kuhama kufikia 2003 (Pkalya, Adan, na Masinde, 2003, uk. 11). Katika muda

wa miaka miwili, wakati fulani, zaidi ya watu 200,000 walilazimika kuhama kwa sababu ya mapigano yaliyohusisha silaha ndogo ndogo wakati jamii zilipokuwa zinapigania mifugo au rasilimali (Adan na Pkalya, 2005, uk. 39).

Katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, ukosefu wa usalama kutokana na kukithiri kwa matumizi ya silaha ndogo ndogo kumekuza utamaduni wa umilikaji silaha ambao umerudisha nyuma maendeleo ya kibiashara, na hata shughuli za uwekezaji, huku silaha hizi zikichangia kukua kwa visa vya ukatili wa kijinsia (Kamenju, Singo, na Wairagu, 2003, uk. 71–79).

Silaha ndogo ndogo zimechangia pakubwa kuongezeka kwa vurugu za hapa na pale, ambazo zimehusishwa na visa vingi vya kijambazi, mapigano kati ya jamii mbalimbali na wizi wa mifugo. Ukosefu huu wa usalama una athari zake kwa upande wa umasikini na kupigania rasilimali kwa sababu inayabidi makundi kuhama au kutoroka na kuelekea maeneo yenye usalama, jambo linaloshinikiza matumizi ya ardhi na rasilimali (Eavis, 2002, uk. 252–53).

Kulingana na idara ya polisi ya Kenya, kadri ya watu 1,400 waliuawa kila mwaka kati ya 2004 na 2009 (Kenya Police, 2007a; 2007b; 2008; 2010). Ingawaje kumbukumbu za takwimu hazijatoa maelezo ya idadi ya waliouawa kupitia bunduki, kati ya 1994 na 2004 utafiti ulionyesha kwamba kulikuwa na zaidi ya vifo 3,000 vilivyosababishwa na mapigano yaliyohusu silaha ndogo ndogo Kaskazini Mashariki mwa Kenya (Adan na Pkalya, 2005, uk. xii).

Utafiti uliofanywa mnamo mwaka 2002 ulionyesha kwamba asilimia 83.7 ya wakaazi wa Nairobi walidhani kuwa idadi ya bunduki ilikuwa imeongezeka (Eavis, 2002, uk. 253). Uchunguzi mwingine wa mwaka 2002 wa waathiriwa ulionyesha kwamba asilimia 37 ya wakaazi wa Nairobi walikuwa waathiriwa wa visa vya wizi katika mwaka uliokuwa umepita (Stavrou, 2002, uk. 4). Katika mwaka wa 2010, idara ya polisi ya Kenya ilipata bunduki kubwa 128, bastola 60, bastola bandia 10, na risasi 36,458, katika operesheni za kawaida za polisi, na bunduki 1,064 na risasi 3,078 katika operesheni ya upokonyaji silaha (Kenya Police, 2010). Ingawaje katika kipindi hiki Kenya ilikuwa inatingishwa na ghasia za baada ya uchaguzi, nyingi za silaha hizi zilitumika katika visa vya uhalifu wa aina nyingine. Hata hivyo, hakujapatikana matokeo ya uchunguzi wowote wa kina kuhusu waathiriwa,

**Jedwali 1.1** Athari za matumizi mabaya ya silaha ndogo ndogo kwa maendeleo ya binadamu

| Athari | Athari kwa maendeleo | Viashiria |
|---|---|---|
| **Athari za moja kwa moja** | Majeraha yaliyo-sababisha vifo na yale ambayo haya-kusababisha kifo | • Kupotea kwa uwezo wa uzalishaji<br>• Gharama za kibanafsi za kutibiwa na kuuguza majeraha<br>• Mahitaji ya kifedha nyumbani, katika jamii, manispaa, na kitaifa<br>• Gharama za kisaikolojia na kijamii |
| **Athari zisizo za moja kwa moja** | Uhalifu unaotumia silaha | • Viwango vya visa vya uhalifu vilivyoripotiwa (mauaji)<br>• Ishara za kijamii za uhalifu<br>• Malipo ya bima<br>• Idadi na aina ya vifaa vya kibinafsi vya usalama |
| | Upatikanaji na ubora wa huduma za jamii | • Visa vya kuvamiwa kwa maafisa wa afya/elimu<br>• Visa vya kuvamiwa na kufungwa kwa zahanati za afya/elimu<br>• Upeo wa utoaji chanjo<br>• Matarajio ya muda anaoishi mtu na vifo vya watoto wachanga<br>• Viwango vya usajili wa watoto shuleni |
| | Shughuli za kiuchumi | • Gharama ya usafirishaji nchi kavu na usafirishaji kwa meli<br>• Kuharibiwa kabisa kwa miundomsingi<br>• Bei ya bidhaa katika eneo husika na masharti ya kibiashara<br>• Uzalishaji wa kilimo na kujitosheleza kwa chakula |
| | Uwekezaji, akiba, ukusanyaji mapato | • Maelekeo ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini na wa kigeni<br>• Mitindo ya uwekezaji wa sekta ya ndani<br>• Mielekeo ya ukusanyaji mapato nchini<br>• Kiwango cha matumizi nchini, na akiba |
| | Mtaji wa jamii | • Idadi ya wanajeshi watoto, walioandikwa na wanaohudumu<br>• Idadi ya wanachama wa vikundi vyenye silaha na uhalifu wenye mipango<br>• Watoto wanaorudiarudia uhalifu wa kutumia silaha<br>• Visa vya dhuluma za kinyumbani zinazohusu bunduki au vitisho vya kutumika kwa silaha<br>• Heshima kwa uongozi wa kitamaduni au kimila |
| | Hatua za kimaendeleo | • Visa vya vitisho<br>• Gharama ya utaratibu wa ugavi na usafirishaji<br>• Gharama ya kusimamia usalama<br>• Gharama zinazohusiana na mazingira yasiyokuwa salama na/au kuharibiwa kwa rasilimali zilizowekezwa |

**Marejeo:** Small Arms Survey (2003, uk. 131)

mbali na huo wa Nairobi uliotajwa hapo awali (Stavrou, 2002), na mwingine wa kitaifa uliofanywa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa Inayochunguza Dawa za Kulevya na Jinai (UNODC, 2010).

Uchunguzi wa UNODC uligundua kwamba waathiriwa wa uhalifu waliripoti kwa polisi zaidi visa vilivyohusisha magari. Kwa hivyo, visa vya juu vitatu vya uhalifu vilivyoripotiwa kwa polisi mnamo 2010 vilikuwa vya wizi wa magari (asilimia 93.8), wizi wa pikipiki (asilimia 77.8), na utekeji nyara wa magari (asilimia 64.7). Visa vya wizi wa mali nyingine havikuripotiwa sana (kwa mfano asilimia 45.5 ya waathiriwa waliripoti kuibwa kwa baisikeli zao, na asilimia 21.7 waliripoti kuibwa kwa mifugo). Hata hivyo, visa hivi viliripotiwa kwa wingi zaidi kuliko vile vya kushambuliwa na visa vingine vya jinai na vya kibinafsi. Kwa mfano, ni mtu mmoja tu kati ya waathiriwa watano wa mashambulizi au dhuluma ya ubakaji waliokiri kuwa waliviripoti kwa polisi. Kwa kiwango cha asilimia 0.9, kosa la ufisadi ndilo lililorekodi visa vichache kuliko vyote (UNODC, 2010, uk. 4, Jedwali 2).

Matokeo ya uchunguzi wa UNODC yanaashiria kuwa idadi ya visa vya uhalifu na ghasia vilivyoripitwa ni vya chini mno, na kwamba kuna uwezekano kwamba polisi hawana habari kuhusu kiwango halisi cha uhalifu

**Jedwali 1.2** Takwimu za uhalifu kimkoa/kitengo 2009 na 2010

| Mkoa/kitengo | 2009 | 2010 |
|---|---|---|
| Bonde la Ufa | 16,887 | 15,790 |
| Mashariki | 8,431 | 7,625 |
| Kati | 8,331 | 7,584 |
| Pwani | 7,805 | 7,357 |
| Magharibi | 7,234 | 6,731 |
| Nyanza | 7,358 | 6,354 |
| Nairobi | 3,984 | 5,097 |
| Kaskazini Mashariki | 872 | 1,003 |
| Reli | 129 | 180 |
| Kitengo cha Polisi cha Viwanja vya Ndege | 89 | 106 |
| **Jumla** | **61,120** | **57,827** |

**Marejeo:** Idara ya Polisi ya Kenya (2010, uk. 16)

na ghasia. Takwimu za polisi za miaka 2009 na 2010 zinaonyesha kwamba kiasi kikubwa cha visa vya uhalifu vilivyoripotiwa vilikuwa katika mikoa ya Bonde la Ufa, Mashariki, na Kati (angalia Jedwali 1.2). Takwimu hizi, pamoja na ripoti kuhusu mienendo ya silaha ndogo ndogo nchini,[9] ndizo zilizopelekea kutajwa kwa sehemu fulani za kaskazini mwa Kenya kuwa maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kutokea kwa fujo, na nyingine kama maeneo yenye uathirikaji wa kadiri na wa chini.

## Mikakati ya usalama na usalimishaji silaha

Serikali ya Kenya ina jukumu la kimsingi la kuhakikisha kuwepo kwa usalama kupitia udumishaji sheria na utangamano. Ili kufanya hivyo, serikali imechanganya taratibu za kuwashurutisha watu wasalimishe silaha, pamoja na kuwaambia wafanye hivyo kwa hiari yao, ili kujaribu kukusanya silaha haramu, hususan huko kaskazini mwa Kenya. Kenya imetekeleza zaidi ya operesheni 50 za usalimishaji silaha katika miaka 100 iliyopita. Inaaminika kuwa wakati wa utawala wa miaka 24 wa Rais Moi, kiongozi huyo wa taifa aliamuru kutekelezwa kwa operesheni 20 kwenye eneo wanamoishi Wapokot pekee (SIKOM Mtandao wa Amani kwa Ajili ya Maendeleo, 2010, uk. 3).

Hata hivyo, hatua za kuwashurutisha watu huzua wasiwasi kuhusu ukiukaji wa haki za kibinadamu, huku jamii na mashirika yakutetea haki za jamii yakikashifu utumiaji wa nguvu zaidi na mateso yanayokithiri mipaka. Juhudi nyingine za kusalimisha silaha, kama zile zilizofanywa mwaka 1984 za Operesheni Wajir, zinasemekana kuishia kuwa mauaji ya halaiki kwa sababu ya idadi kubwa ya watu waliofariki (Wepundi, Ndung'u, na Rynn, 2011, uk. 7).[10]

Serikali ilibadilisha utaratibu wake wa usalimishaji silaha ili kujumuisha hisia hizi kuhusu haki za kibinadamu, pamoja na kutoa njia mbadala za kujikimu kwa jamii zilizolengwa kupitia kuundwa kwa mkakati wa kusalimisha silaha na maendeleo uliojulikana kama Operesheni Dumisha Amani. Utaratibu huu unajumuisha juhudi za maendeleo – kama kujengwa upya kwa miundo msingi – na unajumuisha mkakati madhubuti unaohusisha vikundi na watu mbalimbali, kama viongozi wa mashinani,

mashirika ya kutetea haki za jamii, na vyombo vya habari ili kukuza imani ya watu kuhusu usalimishaji silaha. Awamu ya kwanza ya juhudi hizi ilianza mnamo 2005, na ilipofikia 2006, bunduki 2,298 na risasi 4,418 zilikuwa zimeshapatikana (KNFP, 2010a). Awamu hii ya kwanza haikufikia lengo lililokuwa limewekwa la bunduki 50,000, na kwa hivyo awamu ya pili ikaanza mnamo mwaka 2010, huku kukiwa na awamu ya usalimishaji wa hiari mwezi wa Februari wa mwaka huo (Wepundi, Ndung'u, na Rynn, 2011, uk. 10–11).

Kati ya Februari na Agosti 2010 operesheni hiyo iliweza kukusanya bunduki 1,201, risasi 1,665, na mifugo 201 (KNFP, 2010a). Wasiwasi wa jamii husika kuhusu usalama wao na maendeleo duni umewafanya wasitake kusalimisha silaha zao zote.

Ingawaje serikali iliukubali mtazamo huu wa usalimishaji silaha kwa hiari na taratibu za maendeleo zilizoambatana nao, ilitekeleza mazoezi mawili ya lazima ya kusalimisha silaha wilayani Mt Elgon, na katika kaunti za Bungoma na Mandera. Zoezi lililotekelezwa Mt Elgon lilipewa jina Operesheni Okoa Maisha, ilhali lile la Mandera liliitwa Operesheni Chunga Mpaka. Operesheni ya Mt. Elgon ilikusanya bunduki za aina mbalimbali 103 na risasi 1,155, huku ile ya Mandera ikipata silaha 48 na risasi 1,200. Mazoezi haya mawili yalikumbwa na madai kwamba maafisa wa usalama walikiuka haki za kibinadamu (Wepundi, Ndung'u, na Rynn, 2011, uk. 10–11; HRW, 2008; 2009[11]). Hata hivyo, operesheni hizo zilichukuliwa kuwa zilifaulu kwa kuweza kuwasambaratisha wapiganaji wa Mt Elgon wa Sabaot Land Defence Force (SLDF), na kurudisha amani na utulivu katika maeneo hayo mawili.[12]

Habari zilizotolewa na Kitengo cha Kukabiliana na Wizi wa Mifugo (ASTU) zinaonyesha mfano wa juhudi za pamoja za Serikali ya Kenya kukusanya bunduki na risasi.[13] Kati ya 1 Januari 2010 na 31 Julai 2011, ASTU ilikusanya bunduki 10 na takriban risasi 75. AK-47 sita (mbili zikiwa hazina risasi), G3 tatu (mbili zikiwa hazina nambari za usajili), na SAR-80 moja zilitaifishwa. Nyingi ya risasi zilikuwa za 7.6 mm (risasi 54), huku 20 zilizobakia zikiwa za 5.56 mm.

Juhudi za kudumisha sheria ili kudhibiti kuenea kwa silaha ndogo ndogo zimekumbwa na changamoto kadhaa, hususan kuweko kwa idadi ndogo ya walinda usalama, miundomsingi duni, ufisadi, rasilimali chache, na

ugumu wa hali ya nchi katika maeneo ya mapigano kunakopatikana silaha ndogo ndogo. Juhudi nyingine za polisi za kudumisha usalama zimegonga mwamba na kuzua changamoto nyingine. Kwa mfano, Bevan (2008, uk. 17) anonelea kwamba Idara ya Polisi ya Kenya ndiyo inayotoa takriban asilimia 50 ya risasi zinazozunguka kinyume cha sheria huko Turkana Kaskazini ili Waturkana waweze kujihami dhidi ya makundi pinzani kutoka Sudan na Uganda.

Operation Dumisha Amani ilikuwa imetumaini kuwa kungekuwa na programu ya pamoja na nchi za Uganda na Ethiopia. Mashauriano na mikakati ya pamoja ilianza kufanywa na Uganda, lakini ikakatizwa na chaguzi kuu za Uganda na Kenya katika mwaka wa 2006 na 2007, mtawalia. Mazumgumzo yangali yanaendelea, huku juhudi za hivi majuzi zikilenga kampeni za kusalimisha silaha za pamoja kati ya Kenya na Ethiopia.

Juhudi nyingine ya serikali inayolenga kupambana na changamoto za kiusalama imekuwa kuundwa kwa Kitengo cha Polisi wa Akiba (KPRs), na kutumwa kwa maafisa katika maeneo mbalimbali. Jamii husika zinawachukulia KPRs kuwa muhimu sana, ingawaje kuandikwa kwao kazi na usimamizi wao unasemekana kuwa na kasoro. KPRs ni maafisa wa kujitolea wanaofanya kazi pamoja na polisi wa kawaida. Wao huitwa wakati tu wanapohitajika ili kukabiliana na kutatua matukio fulani ya kiusalama yanoyozua matatizo. Ingawaje wanatekeleza jukumu muhimu, inadaiwa kuwa baadhi yao hutumia silaha walizopewa na serikali ili kutenda vitendo vya uvunjaji sheria (Ndung'u, 2010, uk. 6–7).

Wananchi wanahisi kuwa kuajiriwa na kutumwa kazini kwa KPRs kumeingiliwa kisiasa, kunafanywa kiholela bila ushirikishi, na kunakumbwa na utata mkali. Katika baadhi ya visa, imesemekana kuwa polisi wa kawaida na wale wa utawala wamekuwa wakishindana, na hivyo taratibu kwenye wilaya kadhaa zimekuwa na misukosuko. Hii imehatarisha usalama na kurudisha nyuma hatua za udumishaji usalama za pamoja kati ya polisi na wananchi, na kupunguza kwa kiasi kikubwa wajibu wa KPRs (Ndung'u, 2010, uk. 14–16). Pingamizi hizi zinazua vikwazo vikubwa dhidi ya utekelezaji kikamilifu wa Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji kwa Udhibiti na Usimamizi wa Silaha, (Mpango Tekelezi wa Kitaifa), pamoja na mikataba ya kieneo na kimataifa kama Mwafaka wa Nairobi wa Uzuiaji, Udhibiti na

Upunguzaji wa silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi katika Eneo la Maziwa Makuu na Upembe wa Afrika (Protokali ya Nairobi); Mpango wa Utendaji wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia, Kupambana, na Kuangamiza Biashara Haramu ya Silaha Ndogo Ndogo na Nyepesi katika kila Nyanja (Mpango wa Utekelezaji); na Mwafaka wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Utengenezaji Haramu na Ulanguzi wa Bunduki, Vipuri, Sehemu zake na Risasi.

## Mafanikio na Changamoto

Serikali ya Kenya imepiga hatua kubwa ili kushughulikia changamoto sugu ya silaha ndogo ndogo haramu. Kuundwa kwa Shirika la Kitaifa la Kushughulikia Silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi (KNFP) kama kurugenzi mojawapo kwenye Ofisi ya Rais, Wizara ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Nchi, kumehakikisha kuwepo kwa mfumo jumuishi unaohusisha washika dau wote, kwa namna zote, ili kudhitibi silaha ndogo ndogo. KNFP imepewa jukumu la kushirikisha juhudi zote ili kushughulikia maswala yote yanayohusu silaha ndogo ndogo nchini Kenya.

Katika Mpango wa sasa wa Mkakati wa 2010/11–2014/15, KNFP imejitolea kutimiza matarajio au maono yake ya kuhakikisha kuwepo kwa 'jamii tulivu, yenye usalama thabiti, endelevu, na ambayo haina silaha ndogo ndogo haramu, ili kuweko na maendeleo thabiti' (KNFP, n.d.). Itaweza kufanya hivyo kupitia usimamizi ufaao wa maghala ya silaha, utoaji mafunzo zaidi kwa maafisa wa usalama na wahusika wengine kuhusu usimamizi wa silaha ndogo ndogo, kuimarisha uhamasishaji kuhusu hatari za silaha ndogo ndogo haramu, na kukuza uwezo wa taasisi mbalimbali ili ziweze kukabiliana na kudhibiti changamoto za silaha ndogo ndogo.

Mamlaka ya KNFP yametoka kwa Azimio la Nairobi la tarehe 15 Machi 2000 kuhusu Tatizo la Kuenea kwa Silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi haramu katika Eneo la Maziwa Makuu na Upembe wa Afrika (Azimio la Nairobi), lililotoa wito kwa nchi za Eneo la Maziwa Makuu na Upembe wa Afrika kuimarisha au kuanzisha taratibu za kitaifa za kukabiliana na tatizo la silaha ndogo ndogo haramu, na kutekeleza azimio hilo. Mwafaka wa Nairobi (2004) ulizifunga nchi husika kisheria chini ya Kifungu cha 16 kuhusu uwazi, ubadilishanaji habari, na uwiano. Ushirikiano kati ya serikali

na mashirika ya kutetea haki za jamii pia umehakikishwa, sio tu na Azimio la Nairobi bali pia na Mwafaka wa Nairobi (Kifungu 2c).

Kama taasisi ya kitaifa, KNFP pia inaelekezwa na hati nyingine rasmi za kimataifa na kibara, hususan Mpango wa Utekelezaji na Azimio la Bamako juu ya Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Kuenea kwa Silaha Haramu, kusambaa na Ulanguzi wa Silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi (2010).

Mara tu baada ya kuundwa, mnamo mwaka 2003 KNFP ilianza kuratibu silaha zilizomo nchini, jambo lililochangia ustawishaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa kupambana na silaha haramu nchini. Mkakati wa mpango huo ulibainishwa kwenye mada kumi; mifumo ya kitaasisi, sera na sheria, usimamizi wa maghala ya silaha, elimu ya umma na uhamasishaji, ushirikiano wa kimataifa na kieneo na ubadilishanaji habari, udhibiti mipaka na wakimbizi, mipango ya maendeleo ya binadamu, mafunzo na uimarishaji uwezo, utafiti, na maeneo mengine yanayohitaji usaidizi mkubwa (KNFP, 2006, uk. 40–55). Mada hizi ziliongoza na kuelekeza shughuli za KNFP kwa miaka sita. Hata hivyo, kuna baadhi ya masharti ambayo hayakutimizwa au kutekelezwa kikamilifu kwa sababu za kubanwa, na ukosefu hasa wa rasilmali.

Kitaasisi, kuanzishwa kwa kurugenzi inayofanya kazi, na kuundwa kwa Kamati Kuu ya Kitaifa ya Uongozi kuhusu Usimamizi wa Mizozo na Uimarishaji Amani, kunaweza kuchukuliwa kama mafanikio muhimu ya KNFP. Imetayarisha Mkakati wa Miaka Mitano 2010/11–2014/15, pamoja na mkakati utakaofuatilia na kutathmini. Kwenye viwango vya chini, KNFP imeunda na kufunza majopo-kazi nane ya mikoa (PTFs) na ya wilaya (DTFs) katika wilaya 53, kati ya zaidi ya wilaya 200 nchini. Lakini kufaulu kwa PTFs na DTFs kumetatizwa na ufuatilizi duni, ukosefu wa rasilimali za kutekeleza mipango inayohusu silaha ndogo ndogo, na kuhamishwahamishwa kwa wasimamizi.[14]

KNFP pia imerahisisha kuandikwa kwa Sera ya Kitaifa ya Silaha Ndogo Ndogo, iliyokamilishwa na kukabidhiwa waziri wa utawala wa mikoa na usalama wa nchi mnamo Desemba 2009.

Katika usimamizi wa ghala za silaha, ingawaje operesheni za usalimishaji silaha kama Okoa Maisha and Dumisha Amani zinasimamiwa kikamilifu na makundi huru, KNFP inashirikisha juhudi kuangamiza silaha

zilizorudishwa au kupatikana hadharani. Kufikia Machi 2010, Kenya ilikuwa imeshaangamiza zaidi ya silaha haramu 25,000 na risasi 50,000 (KNFP, 2010b, uk. 9). KNFP imepata mashine tano zinazoweka silaha alama[15], na kufikia mwisho wa Mei 2011 ilikuwa imeweka alama zaidi ya bunduki 60,000 (KNFP, 2011, uk. 2). KNFP pia imesimamia kuboreshwa kwa kumbukumbu za takwimu, kuwekwa kwa programu ya kompyuta kufuatilia udalali na biashara ya silaha. Kutiwa alama kwa bunduki za serikali kumeimarisha utambulishaji na ufuatiliaji, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa kutumika visivyo kwa bunduki hizo.

Kwa upande wa utafiti, Uratibu wa Kitaifa wa Silaha Ndogo Ndogo na Silaha Nyepesi Haramu (Uratibu wa Kitaifa wa Silaha) wa mwaka wa 2003 ndiyo umekuwa mradi mkuu wa utafiti wa KNFP uliosaidia kukuzwa kwa Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji nchini Kenya (KNFP, 2006). Hata hivyo, hakujawa na utafiti mwingine wowote kama huo katika miaka minane iliyofuata. Lakini, chunguzi kadhaa zimefanywa kwa kiwango cha maeneo, kwa mfano Uchunguzi wa mwaka 2010 kuhusu Upokonyaji Silaha Katika Eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, na uchunguzi kuhusu Namna Mbadala za Kujikimu, zilizoanzishwa na Taasisi ya Mafunzo ya Usalama (ISS).[16]

Kimataifa na kieneo, mbali na kuhudhuria kongamano za kimataifa za Mpango wa Utekelezaji na za kieneo za RECSA, KNFP imechangia pakubwa kushinikiza kuwepo kwa udhibiti mkali kimataifa wa ulanguzi wa silaha, kwa kuungana na wengine ili kudhamini na kupigia debe kukubalika kwa Mkataba wa Biashara ya Silaha, ikisaidiwa na nchi nyingine sita zenye mwelekeo na maono hayohayo (Argentina, Australia, Costa Rica, Finland, Japani, na Uingereza) (Saferworld, 2011, uk. 11).

Hata hivyo, licha ya kutambua na kushukuru usaidizi unaotoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo,[17] KNFP inatatizwa na ukosefu wa fedha, taasisi, na watendakazi. Hii ndiyo sababu yake kubwa kushindwa kutekeleza kikamilifu Mpango wake wa Kitaifa wa Utekelezaji (uliokusudiwa kuanza 2004 hadi 2009) (Saferworld, 2011, uk. 15).

Uwezo wa PTFs na DTFs nao pia ni mdogo kwani hawawezi kuziba ipasavyo pengo lililopo kati ya hatua za eneo-husika na za kitaifa. Mbali na hayo, KNFP inakabiliwa na changamoto za urasimu na vipaumbele vya kitaifa vinavyoshindana. Na inapofikia maswala ya silaha ndogo ndogo,

operesheni za usalimishaji silaha wakati mwingine zinachochewa na sababu za kisiasa na kiusalama ambazo ni kubwa zaidi kuliko uwezo na/au udhibiti wa KNFP (Saferworld, 2011, uk. 15–16). Utatuzi mwafaka unaofaa kwa KNFP ni kutoa ushawishi mkali ili Sera ya Kitaifa ya Silaha Ndogo Ndogo ipitishwe na kukubalika, na Mfumo wa Sera ya Maendeleo na Usalimishaji silaha umalizwe na utekelezwe. Haya yakifanyika, hata kama kutakuwa na vishawishi kuhusu udhibiti silaha vya kisiasa na vya kuisalama vyenye nguvu, basi vitakuwa tayari viko ndani ya sera zilizopo.

## Madhumuni ya Mradi wa Kitaifa wa Uratibu wa Silaha

Utafiti mwingi kuhusu silaha ndogo ndogo nchini Kenya kwa ujumla hulenga kaskazini mwa Kenya (ambayo inabainishwa kama Kaskazini mwa Bonde la Ufa, Kanda ya Juu ya Mashariki na Mkoa wa Kaskazini Mashariki).[18] Mradi wa KNFP wa mwaka 2003 wa Uratibu wa Kitaifa wa Silaha ndiyo uliokuwa utafiti wa kitaifa wa kwanza na wa kina uliofanyika nchini.

Kati ya mwaka 2003 na sasa, hakujakuwa na utafiti mwingine kama huu, mbali na ule uliofanywa na RECSA/ISS kuhusu shughuli ya usalimishaji silaha.[19]) Kwa kifupi, kumekuwa na mwanya mkubwa katika utafiti jarabati wa kawaida kuhusu silaha ndogo ndogo na mienendo ya kiusalama nchini Kenya kwa ujumla.[20]

Hii inamaanisha kwamba, hata katika mikakati ya udhibiti silaha, ni kiwango cha chini mno kilichopo cha utafiti uliofanyiwa majaribio ambao una makadirio yanayoweza kuthibitishwa kuhusu idadi ya silaha haramu zilizoko mikononi mwa raia humu nchini. Uchunguzi uilofanywa na Kituo cha Utafiti na Habari (SRIC) ulikadiria kuwa wanaume 127,519 wenye umri wa miaka 15 na zaidi katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa ilidhaniwa walikuwa wanamiliki silaha, kila mmoja akiwa na angalau bunduki moja (Kamenju, Singo, na Wairagu, 2003, uk. 68–69). Shirika la Utendaji Thabiti lilikadiria kuwa idadi ya silaha katika baadhi ya wilaya wanamoishi wafugaji wa kuhamahama nchini Kenya[21] ilikuwa 172,995, huku wakati huohuo ikisema kuwa makadirio ya SRIC yalikuwa ya chini (Adan na Pkalya, 2005, uk. 50–51).[22] Makadirio kuhusu idadi ya silaha katika sehemu nyingine nchini hayapatikani kwa urahisi, ila yale ya Mkutu (2008, uk. 4)

aliyekadiria kuwa idadi ya silaha ndogo ndogo zilizokuwa zinazunguka mjini Nairobi mnamo mwaka 2000 zilikuwa milioni 5. Utafiti mwingine ulisema idadi ya bunduki haramu mjini Nairobi ilikuwa 5,000, ikimaanisha kuwa kwa kila wakaazi 560 wa Nairobi, mmoja humiliki bunduki (Sabala, 2002, uk. 36).[23] Yote haya ni makadirio ya silaha ndogo ndogo katika maeneo kadhaa tu, na wala siyo kote nchini.

Utafiti wa KNFP uliofanywa mwaka 2003 uligundua kwamba asilimia 6 ya kila kaya ilikuwa ina silaha ndogo. Kimkoa, hii iliwakilisha asilimia 6 katika Mkoa wa Kati, asilimia 4 Pwani, asilimia 7 Mashariki, asilimia 6 Nairobi, asilimia 5 Kaskazini Mashariki, asilimia 6 Nyanza, asilimia 5 Bonde la Ufa na asilimia 7 Magharibi (KNFP, 2006, uk. 16). Lakini maswali ya mzunguko yaliyoulizwa na yaliyohusu viashiria kuhusu silaha ndogo ndogo, kama kujulikana kwa anayemiliki bunduki, au kusikika mara kwa mara kwa milio ya risasi aishipo mtu fulani, kulibainisha kuwa asilimia kubwa zaidi ya wananchi kote nchini (asilimia 8) walikuwa wameshakumbana na athari za silaha ndogo ndogo walimoishi (KNFP, 2006, uk. 17).

Sehemu muhimu ya usimamizi wa maghala ya silaha, iliyoelezewa wazi katika Mpango wa Mkakati wa KNFP wa 2010/11–2014/15, ni kufanywa kwa chunguzi mpya na kamili, na kuratibu maeneo yote kote nchini Kenya yenye silaha ndogo ndogo, ili kukadiria idadi ya silaha haramu nchini, namna zinavyotumika au kuhamishwa, na kukusanya habari zitakazotumika baadaye katika hatua za kitaifa na kieneo zitakazojumuisha juhudi za kusalimisha silaha, miongoni mwa nyingine.

Uchunguzi huu ni wa pamoja, kati ya Serikali ya Kenya na Small Arms Survey ya Geneva. Madhumuni makuu ya kufanywa kwa utafiti huu ni:

i. kukadiria idadi ya silaha ndogo ndogo nchini Kenya;
ii. kutambua kunakotoka silaha hizi, maeneo zinakopatikana, na zinavyo-safirishwa kutoka Kenya na zinavyoingizwa nchini;
iii. kutathmini uwezo wa wahusika wote wa juhudi za kudhibiti silaha ndogo ndogo, na uimarishaji amani;
iv. kukadiria wajibu na zinavyotumika habari kuhusu silaha ndogo ndogo haramu, na uhusiano uliopo baina ya tahadhari za mapema na mbinu za kujibu au kuchukua hatua nyakati za mapigano;

v. kukadiria athari za ukosefu wa usalama kutokana na utumizi wa silaha ndogo ndogo haramu, hususan katika jamii za wafugaji wa kuhamahama, athari za ukosefu wa chakula, za umasikini, na zinazoathiri njia za kutafuta ajira, mbali na masuala mengine yanayozua hofu; na
vi. kuangazia mafunzo yaliyoibuka kutoka kwa uchunguzi wa awali ambayo yatachangia juhudi za baadaye za kutatua tatizo la silaha ndogo ndogo haramu.

## Utaratibu na Upeo

KNFP na Small Arms Survey ziliunda jopo la uchunguzi lililopewa jukumu la kutayarisha mfumo madhubuti wa uchunguzi wa kitaifa. Kaunti zilizopo nchini Kenya ziliorodheshwa katika mojawapo ya viwango vitatu vinavyopima viwango vya uwezekano wa kuzuka kwa vurugu au uathirikaji: sehemu zenye vurugu kali za kisiasa au uathirikaji wa kiwango cha juu, zenye vurugu za wastani, na zenye kiwango cha chini (nyingine). Kwa minajili ya uchunguzi huu, kaunti zenye misukosuko na vurugu za mara kwa mara ziliainishwa kama ambazo zilikuwa na hatari ya kutokea kwa vita baadaye, maeneo ambayo visa vya uhalifu vilikuwa vingi, na ukosefu wa usalama ulikuwa unakithiri. Hali ya uwezekano wa kuzuka kwa vurugu nchini ilipimwa na kudhihirishwa kupitia duru na marejeleo kadhaa, mbali na ufahamu unaobainika nchini.Uainishaji wa kaunti kulingana na viwango vya uwezekano wa kuathirika uliarifu utaratibu wa sampuli, na ulitumika kama kiashirio huru wakati wa uchambuzi wa takwimu (angalia Ramani 1.2 na sehemu V).

Mfumo wa sampuli wenye matabaka na uliochagua wahojiwa bila kufuata mpangilio wowote maalum uliohusisha kaunti 31 kati ya 47 ulitumiwa. Kaunti zilizodhaniwa kuwa na tatizo kubwa la silaha ndogo ndogo zilikuwemo, pamoja na zile ambazo zilihofiwa kuwa na uwezekano wa kukua kwa tatizo hilo, pamoja na sehemu za mijini zanazokuwa na visa vingi vya uhalifu. Aidha, kaunti kunakoishi kiasi kikubwa cha jamii za wafugaji wa kuhamahama wanaomiliki silaha ili kujihami na kulinda mifugo wao pia zilihusishwa, kama maeneo ya Tana River, Marsabit, Isiolo, Garissa, Wajir, Mandera, Turkana, Pokot Magharibi, Baringo, Samburu,

Laikipia, Elgeyo-Marakwet, na Trans-Nzoia. Nairobi nayo iliorodheshwa kama mojawapo ya kaunti zenye misukosuko ya hali ya juu ya mara kwa mara.

Aina tatu za hojaji zilitumika katika kufanya uchunguzi huu: moja ikilenga kaya (HHs), nyingine ikilenga maafisa wa udumishaji usalama (LEAs), na ya tatu ikilenga mashirika ya kutetea haki za jamii (CSOs). Pamoja na uchunguzi wa kaya 1,873, takwimu zilizopatikana ziliongezewa nguvu na habari kutoka kwa takriban LEAs 336, CSOs 178, FGDs 18 na mahojiano ya watoa habari wakuu, KIIs. Njia za ukusanyaji takwimu au data kwa uchunguzi wa HH, LEA, na CSO zilifanana sana, ilihali makundi ya FGDs yalitegemea miongozo iliyojikita kwenye maudhui yayo hayo. Kama ilivyotajwa hapo awali, mijadala ya FGDs iliendeshwa kwa makini zaidi katika maeneo yanayojulikana kuwa na tatizo la utumiaji wa silaha haramu, kama maeneo fulani ya Magharibi mwa Kenya, Kati, na Kaskazini mwa Bonde la Ufa; Kanda ya Juu ya Mashariki; Mkoa wa Kaskazini Mashariki, na miji mikuu mitatu ya Nairobi, Mombasa, na Nakuru.

Utafiti wa nyanjani ulifanywa kati ya Aprili na Julai 2011. Maelezo zaidi kuhusu sifa bainifu za sampuli, pamoja na ugawaji kwa kikaunti, kijinsia na umri, yako katika Sehemu V ya ripoti hii.

# II. Silaha ndogo ndogo na hisia kuhusu usalama

## Utangulizi

Ukadiriaji wa hali iliyopo kwa wakati huu kuhusu silaha ndogo ndogo nchini Kenya unadhihirisha wazi kuwepo kwa udhaifu fulani kuhusu tatizo sugu la silaha ndogo ndogo. Matokeo yanaonyesha kuwa mipaka ya Kenya ingali haijadhibitiwa vilivyo, huku mapigano ya wenyewe kwa wenyewe huko Somalia yakivuka mipaka hadi ndani ya Kenya. Mashambulizi ya sasa ya jeshi la Kenya dhidi ya al-Shabaab yameyafanya maeneo yanayopakana na nchi hiyo, kama Mandera na Garissa, kuwa katika hatari ya kushambuliwa. Hivi karibuni kumekuwa na ripoti za mashambulizi kwa kutumia maguruneti, mabomu ya kutegwa ardhini, na mabomu yaliyotengezwa kwa ufaraguzi (IED) katika maeneo hayo.[24] Wasiwasi wa wahojiwa kwamba kulikuwa na uwezekano kuwa baadhi ya Wasomali wanaotafuta hifadhi nchini Kenya ndio wanaohusika katika ulanguzi wa silaha haramu,[25] pamoja na shauku kuhusu udhibiti wa mipaka ya Kenya, unaipa nguvu haja ya kuwepo kwa mikakati zaidi ili kuziba mianya iliyoko mipakani, na pia kuwapa polisi na maafisa wengine wa usalama mafunzo muafaka na yanayostahili kuhusu njia za kupambana na uhalifu.[26]

Utafiti huu unaonyesha jinsi hali hii ya umilikaji silaha ilivyo tata na ilivyo na vipengee vingi na vizito—kwa mfano, katika maeneo fulani umilikaji silaha unaenda sambamba na usalama wa jamii na njia za kujipatia riziki; ilhali katika maeneo ya mijini mara nyingi umilikaji bunduki haramu unahusishwa na uhalifu.[27]

Sehemu hii inaangalia mielekeo au namna silaha zinavyotumika (ukiwemo utambuzi wa kiwango cha ueneaji wa silaha ndogo ndogo nchini Kenya), na mahali zitokako na ziendako.

Matokeo yaliyopo hapa yanahusu tafiti zilizohusu HHs, LEAs, na CSOs. Mbali na hayo, sehemu hii ya ripoti inajumuisha habari stahilifu zilizotokana na taarifa kutoka kwa FGDs na KIIs, ambazo zimerejelewa ipasavyo.

## Kuenea kwa silaha ndogo ndogo na namna zinavyotumika

### *Hisia kuhusu sababu za kuhitajika kwa silaha ndogo ndogo*[28]

Kusudi kubwa la wengi la kutaka kumiliki bunduki ni ili kujihami—huku wahojiwa wengi wa HH wakisema walitaka kujihami dhidi ya hatari mbalimbali ambazo zingeweza kutokea. Haja ya kulinda mali, hususan mifugo, katika maeneo ya wafugaji wa kuhamahama, iliorodheshwa kama sababu muhimu zaidi ya kutaka kumiliki bunduki, kama ionekanavyo katika Jedwali 2.1. Aidha, ulinzi wa jamii dhidi ya jamii au koo nyingine, na ulinzi wa kijiji, ndiyo yaliyokuwa masuala mengine yaliyopewa uzito na wahojiwa. Sababu nyingine muhimu zilizotajwa za umuhimu wa kumiliki bunduki zilikuwa woga na wasiwasi kuhusu kuzuka kwa mapigano hapo baadaye, na ulinzi wao wa kibinafsi (hususan kwa wahojiwa wa HH). Aidha, sehemu kubwa ya wahojiwa wa LEA (asilimia14.7) walisema kuwa kwa mujibu wa maoni yao, mtu anaweza kumiliki bunduki kwa sababu za kitamaduni, au za kutaka kufanya uhalifu.

**Jedwali 2.1** Sababu za kumiliki bunduki kulingana na maoni ya HHs na LEAs (%)

| Sababu | HHs | LEAs |
|---|---|---|
| Ulinzi wa mali | 29.5 | 18.5 |
| Ulinzi wa kibanafsi dhidi ya koo nyingine | 16.2 | 8.2 |
| Ulinzi wa kibanafsi dhidi ya makundi haramu na majambazi | 14.5 | 19.8 |
| Ulinzi wa kijiji | 10.4 | 12.0 |
| Wasiwasi kuhusu kuzuka siku zijazo kwa vurugu/ msukosuko/ vita | 10.4 | 11.7 |
| Ulinzi wa kibanafsi dhidi ya wanyama pori | 8.7 | 2.6 |
| Silaha zikiwa kama sehemu ya ala za kufanyia kazi | 3.5 | 5.6 |
| Ulinzi kazini | 1.7 | 4.5 |
| Silaha zikiwa kama sehemu ya tamaduni/visa vya uhalifu | 1.7 | 14.7 |
| Uwindaji | 1.7 | 1.6 |
| Mali yenye thamani kwa familia | 1.7 | 1.0 |


**Kumbuka:** safu zinaweza zisijumuilike kufikia asilimia 100 kwa sababu zimewekwa katika nambari kamili.
**Marejeo:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Ramani 1.2 Uwezekano wa kukumbwa na fujo, kwa kaunti, Kenya**




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 2.1** Hisia kuhusu umiliki wa bunduki kwa ulinzi wa jamii, uwezekano wa kuathirika, kwa kaunti na makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Mchoro 2.1 unaonyesha kuwa katika maeneo yaliyofanyiwa sampuli yenye uathirikaji wa juu,[29] haja ya kutaka kumiliki bunduki kwa minajili ya kuilinda jamii iliorodheshwa juu zaidi na wahojiwa wa CSOs na LEAs, ikilinganishwa na wahojiwa wengine kutoka maeneo yenye uathirikaji wa viwango vya wastani, au vya chini.

Kwa sababu jamii nyingine, hasa zile zinazoishi katika maeneo kame na yenye ukame wa wastani, zina historia ya uhasama, bunduki huchukuliwa kuwa silaha muhimu za kutumia katika mapigano dhidi ya vikundi pinzani. Katika sehemu zenye vurugu za mara kwa mara, LEAs waliorodhesha 'kuilinda jamii' kwa kiwango cha juu kidogo kuliko 'hofu ya ghasia siku zijazo', kama motisha ya kumiliki silaha.

Shauku husika zinazochangia kuongezeka kwa idadi za bunduki ni pamoja na zile za watu kutaka kujihami dhidi ya makundi haramu, na wasiwasi kuhusu kuzuka kwa vita au msukosuko. Pia, kuna sababau za kitamaduni zinazowafanya watu wamiliki silaha: asilimia 1.7 ya wahojiwa wa HH walisema wanamiliki bunduki kwa sababu za kitamaduni, ilhali huko Turkana, LEA mmoja alisema kuwa katika jamii za wafugaji wa kuhamahama, wao huwa 'na motisha ya kuiba mifugo kwa ajili ya ufahari fulani na ulipaji mahari'.[30]

Mtazamo mwingine ni kipengele kinachoangalia vile umilikaji bunduki unavyochukuliwa kizazi hadi kizazi—vipo visa ambapo vijana wa vizazi vidogo hurithi bunduki zilizokuwa za wazazi wao.[31] Kwa kweli, asilimia 1.7 ya wahojiwa walisema kuwa kumiliki bunduki ni kuwa na uwezo wa kuwa

na kitu chenye thamani kubwa sana. Thamani hii ya kuwa na bunduki ina maana ya undani zaidi, hasa kwa sababu mtu anaweza kuitumia ili kuilinda jamaa na mali yake katika muktadha wa ukosefu wa ulinzi kamili kutoka kwa serikali. Kwa hivyo bunduki ni ishara ya utambulisho wa jamii, usalama na uhifadhi wao. Kwa njia hii basi, bunduki ni kifaa chenye thamani kubwa kwa familia.

Wizi wa mifugo na mapigano kati ya makabila yangali matatizo sugu huko kaskazini mwa Kenya, na husababisha kuwepo kwa haja kubwa ya kutafuta silaha kwa sababu inakuza uwezo wa jamii husika kuweza kujihami. Katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, jamii za wafugaji wa kuhamahama mara nyingi hujikuta wanapigania rasilimali vikali, wakitafuta kujishindia uwezo wa kumiliki na kudhibiti maji na lishe kwa mifugo yao.

Kwa upande mwingine, kuonekana kwa watu wanaobeba bunduki mara kwa mara, hususan katika maeneo ya wafugaji, pamoja na kushindwa kwa serikali kukusanya silaha zote haramu, kumechangia hali ya kuonekana kuwa kuna ruhusa fulani ya kutojali. Kwa hivyo, wapo wanoamua kumiliki bunduki kwa vile ndiyo hali halisi iliyopo. 'Kwa sababu wengine wana silaha, na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa dhidi yao, basi sisi nasi tunanunua bunduki', alisema mhojiwa mmoja kutoka Samburu.[32]

Aidha, kuna sababu za kijambazi za kutaka kumiliki silaha katika maeneo wanamoishi wafugaji, na mijini, pia. Baadhi ya uhalifu unaofanywa kwa kutumia bunduki katika maeneo ya wafugaji ni pamoja na wizi wa mifugo na ujambazi barabarani. Huko mijini, silaha haramu hutumika sanasana katika visa vya wizi wa kutumia nguvu, na utekeji nyara wa magari kwa nguvu. (NTA, 2009, uk. 19).[33]

Katika jamii fulani za wafugaji, ni jambo la kawaida kwa *morani* kutarajiwa kuua kabla hajatambuliwa kama mpiganaji shupavu. Katika jamii ya Waturkana, miili ya *wamorani* huchorwa alama fulani kwa kutumia vifaa vyenye ncha kila mara wanapoua.[34] Lakini uchoraji huu hauna maana hii tu: bali hutumika pia katika unadhifishaji—inaamimika kwamba damu ya *wamorani* inapomwagika wakati wanapochorwa, basi laana ambazo zingewaandama kwa mauaji waliofanya zitakuwa zimevunjika. Kwa njia hii hii, bunduki imekuza itikadi kuhusu hali ya uume – Fikra za ujasiri, ushujaa, na hata ukakamavu kama mwanamume zinaambatanishwa na kufanikiwa

katika wizi wa mifugo, na ulinzi wa jamii, miongoni mwa jamii za wafugaji. Hali hii inazua haja kubwa ya kutaka kumiliki bunduki.[35]

**Kisanduku 2.1** Dondoo toka FGD, Mandera, 19 Julai 2011

***Swali: Kwa nini watu kutoka eneo hili hununua bunduki?***

- Majirani wachokozi hutuvamia. Inabidi tujihami.
- Jamii za wafugaji huja na silaha. Wanaweza kutuvamia.
- Hakuna ulinzi wa kutosha kutoka kwa serikali. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kujilinda wenyewe.
- Koo zetu huzusha mapigano hata kwa visababu vidogo. Lazima tukae chonjo kila wakati ili tulinde ukoo wetu.
- Ni sharti tujilinde wenyewe na mali [zetu].
- Kwa sasa, hii ni biashara yenye maana sana. Uuzaji wa silaha haramu ni biashara yenye manufaa. Tunafanya hivyo kwa sababu za kibiashara.
- Tunataka tujisikie kwamba tuko salama, kwa hivyo tunazinunua [bunduki] na tunazihifadhi tu.
- Tunazipata kutoka kwa wanaotoroka mapigano huko Somalia. Hatuwezi kuzitupa.
- Pia, zinaonyesha hadhi fulani. Matajiri ni sharti wazimiliki [bunduki] ili wajihami.
- Baada ya mapigano, huwa tunabaki na silaha tulizoteka.

## *Makadirio ya umiliki wa bunduki nyumbani*

Walipoulizwa moja kwa moja, 'Je wewe, ama yeyote katika kaya yako, ana bunduki?' ni asilimia 2.7 tu ya wahojiwa wa HH waliokiri kumiliki bunduki. Idadi hii imepungua kwa kiwango kikubwa—kwa nusu—ya idadi ya kaya zilizosema zinamiliki bunduki mnamo mwaka 2003, wakati kulikuwa na asilimia 6 ya wamiliki (KNFP, 2006, uk. 16). Ni vigumu kusema kuwa kupungua huku kunatokana na juhudi zilizofaulu za kujaribu kukusanya silaha, au kupungua kwa idadi ya wanaotafuta silaha hizi. Kama hii ingalikuwa ndiyo sababu basi, ingebidi mamia ya maelfu ya bunduki ziwe zimeshakusanywa tangu mwaka 2003, huku ikitiliwa maanani kwamba kwa sasa inawezekana kuwa takriban kaya 210,000 zina angalau bunduki moja moja.

Kwa bahati mbaya, hakuna mkondodata au takwimu mahususi zilizohifadhiwa vyema zinazoonyesha ni bunduki ngapi zilikusanywa kila mwaka tangu 2003 (wakati ambapo uchunguzi wa mwisho wa kuratibu bunduki

ulifanywa). Hata hivyo, takwimu zilizotoka katika idara kuu ya silaha, Central Firearms Bureau, zinaonyesha kwamba katika mwaka 2010 pekee ni bunduki 1,411 na risasi 17,997 zilizopatikana. Kwa upande mwingine, takwimu kutoka ASTU zinaonyesha kwamba kati ya 1 Januari 2010 na 31 Julai 2011, bunduki kumi na risasi 74 zilipatikana.[36] Haijabainika wazi iwapo takwimu za Central Firearms Bureau zinajumuisha zile zilizotolewa na ASTU. Lakini muhimu zaidi ni kwamba ukosefu wa habari kamili zilizokusanywa kwa utaratibu katika miaka minane iliyopita unadhihirsha wazi kuwepo kwa mwanya muhimu unaohitaji kuzibwa.

Basi, yawezekana kwamba katika mwaka 2011, ni wamiliki wachache zaidi waliojitokeza kukiri kuwa wanamiliki bunduki, ikilinganishwa na mwaka 2003, hasa kwa sababu ya uwezekano mkubwa kwamba silaha hizo si halali. Hivi karibuni, kumekuwa na operesheni kadhaa za kuwashurutisha watu wasalimishe silaha, Operesheni Dumisha Amani iliyoanza 2010 ikiwa moja yao. Inawezekana kuwa labda wahojiwa walielewa madhara yanayoweza kuzuka iwapo wangeyataja maeneo yao kuwa maeneo yenye silaha nyingi. Kumekuwa na historia ya kuweko kwa operesheni za kuwashurutisha watu wasalimishe silaha mkoani Kaskazini Mashariki, ambazo zimesemekana baadaye kuwa zilisababisha vifo vya watu wengi—ya hivi karibuni ikiwa Operesheni Chunga Mpaka huko Mandera mnamo 2008 (Wepundi, Ndung'u, and Rynn, 2011, uk. 11).

Mbali na Bungoma, wengi wa wakaazi wa kaunti ambapo wahojiwa walikiri kumiliki bunduki walitoka katika maeneo ya wafugaji. Huko Bungoma, ni wahojiwa 11 kati ya 86 (asilimia 13.3) waliothibitisha kuwa wana bunduki. Ni katika wilaya ya Mt Elgon, iliyoko kaunti ya Bungoma, ambapo wanamgambo wenye silaha wa SLDF walikuwa wanapigania ardhi katika mpango wa makao wa Chepyuk. Operesheni Okoa Maisha, iliyoongozwa na jeshi mnamo 2008, iliweza kuwadhibiti na kuwapokonya bunduki, lakini kutokana na matokeo ya sasa, inadhaniwa kuwa kungali kuna wananchi ambao wangali wanamiliki silaha katika kaunti hiyo.

Watu wengi waishio katika kaunti zenye wafugaji wengi za Baringo, Isiolo, Laikipia, Samburu, Tana River na Turkana, ndiyo walikiri kuwa na bunduki. Wakaazi wa kaunti za Nairobi, Mandera, na Garissa walikana kuwa wana silaha, ingawaje, kwa mfano, kwenye utafiti wa masaibu ya waathiriwa mjini

Nairobi uliofanywa 2002, asilimia 3 ya wahojiwa wote walikiri kwamba nyakati nyingine huwa wanabeba bunduki (Stavrou, 2002, uk. 37). Pamoja na hayo, hali ya sasa ya kuzorota kwa usalama huko kaskazini-masahriki mwa Kenya, inayosababishwa na al-Shabaab, inadhihirisha kwa kweli kuwa mipaka ya Kenya ina mianya mingi, na kwamba kuna uwezekano kuwa tatizo la silaha ni kubwa zaidi kuliko walivyosema wahojiwa. Utata unaozingira athari za kukiri kumiliki silaha huenda uliwafanya wahojiwa wengi katika baadhi ya maeneo kutofichua ukweli halisi kuhusu kiwango cha umiliki wa silaha.

Jumlisho la majibu yanayothibitisha umiliki wa silaha katika kaunti yaliyowekwa katika maeneo makubwa zaidi ya uchambuzi linaonyesha kwamba kiwango kikubwa cha wahojiwa wa Kaskazini mwa Bonde la Ufa walikiri kuwa na silaha. Thelathini kati ya wahojiwa 266 katika eneo hilo (asilimia 11.3) walithibitisha haya (Jedwali 2.2).

**Jedwali 2.2** Majibu kwa swali: 'Je, wewe ama yeyote kwa kaya yako anamiliki bunduki?' (%)

| Eneo | Ndio |
|---|---|
| Bonde la kaskazini | 11.3 |
| Magharibi | 10.4 |
| Bonde la kusini | 1.5 |
| Pwani | 1.7 |
| Nyanza | 0.8 |
| Mashiriki ya Juu | 3.7 |
| Kati | — |
| Kati na Mashariki ya chini | — |
| Nairobi | — |
| Kaskazini Mashariki | — |
| Wastani katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti | 2.7 |

**Marejeo:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

## *Hisia za umma*


Kwenye maeneo ya makazi ya Kibera na Kayole mjini Nairobi, wahojiwa walielezea wasiwasi wao kuhusu makundi ya vijana waliokuwa wanajihusisha na uhalifu. 'Vijana husika wana mtandao wao. Wale kutoka Kibera

wanasaidiwa na wengine walioko kwingine Nairobi ili kutenda visa vya uhalifu huko, nao, kwa upande wao, watavunja sheria hapa Kibera. Ni aina fulani ya mpango wa ubadilishanaji kati ya wahalifu.'[37]

Kutegemea silaha kama visu, mapanga na simi, na bunduki, ni suala jingine linalozua changamoto. Katika jamii ambazo hazihamihami kama Wameru, wizi wa mabavu hufanywa kwa kutumia silaha zenye bapa kama visu na mapanga, na silaha butu.[38] Huko Nakuru, utumiaji wa silaha butu na bunduki umechangia kuongezeka kwa visa vya uhalifu vizito, hususan ujambazi. Wananchi wanazidi kuvunjika moyo kwa sababu polisi wameshindwa kutatua tatizo hilo.[39]

Walipoulizwa 'Je, kwa maoni yako, ni kaya ngapi katika eneo uishimo zinazomiliki bastola/bunduki?' ni wazi kwamba kuna mwelekeo unaoonyesha kwamba idadi ya silaha hushuka wakati ule uwezekano wa eneo husika kuathiriwa na fujo unapungua. Yaani, jinsi kiwango cha uathirikaji wa eneo na fujo kinavyopungua, ndivyo idadi ya kiwango cha wahojiwa waliohisi kukithiri kwa silaha katika eneo hilo inavyopungua pia (angalia Mchoro 2.2).

**Mchoro 2.2** Hisia kuhusu umiliki wa bunduki nchini,* kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




* Alama ya wastani ya utambuzi kwa kiwango cha 1 = wachache sana hadi 4 = wengi/karibu wote.
**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Ingawaje ni wahojiwa wachache sana waliokiri kumiliki bunduki katika maeneo fulani, wakati wa FGDs, washiriki walitoa maoni ya wazi zaidi, na

wakakubali kwamba silaha haramu zilikuwepo. Huko Mandera, Marsabit, Lokichoggio, Pokot Magharibi, Baringo Mashriki, na Samburu, ambapo wakaazi wengi ni wafugaji wa kuhamahama, wahojiwa walikubali kuwa kulikuwepo na idadi kubwa zaidi ya silaha mikononi mwa watu kuliko ilivyokuwa imeonyeshwa kwenye utafiti wa HH.

Huko Samburu, kwa mfano, washiriki wa FGD walikadiria kuwa kulikuwa na bunduki 10,000 mikononi mwa raia na silaha 3,000 zilizokuwa zimemilikiwa na KPRs.[40] Na huko Mandera, makadirio ya wahojiwa wa makundi mahususi kuhusu waliokuwa na bunduki Kaskazini Mashariki yalikuwa asilimia 20 ya kaya zote. Kwa maoni yao, idadi ya bunduki imepungua kwani uhasama kati ya koo mbalimbali pia umepungua. Mara ya mwisho kulipozuka mapigano makali kati ya koo ilikuwa mnamo 2008, na mapigano haya yalizua zoezi la serikali la kuwashurutisha watu wasalimishe silaha lililojulikana kama Operesheni Chunga Mpaka.[41]

Huko Marsabit, wahojiwa walikadiria kuwa ni watu wachache tu waliokuwa na silaha. Kwa maoni yao, bunduki haramu katika maeneo ya Marsabit ya Kati ndiyo hutumika kwa visa vichache vya ujambazi vinavyotokea huko. Baadhi ya visa hivi yasemekana vinafanywa na KPRs.[42]

Wahojiwa wa Lokichoggio huko Turkana walikiri kuwepo kwa silaha katika eneo hilo, na wakatoa makadirio ya juu zaidi ya idadi ya silaha kuliko maeneo mengine. Kulingana nao, watu wengi, wa umri zote, wana bunduki, na nyakati nyingine hata watoto huwa wanazibeba.[43] Kwa maoni ya wahojiwa wa FGD, kuathiriwa kwa jamii kwa sababu ya uvamizi wa mara kwa mara kutoka kwa jamii hasimu nchini Kenya (hususan kwa Wapokot), Uganda, Sudan Kusini, na Ethiopia kunaelezea sababu ya kuwepo kwa haja kubwa ya bunduki.[44]

Yaonekana kwamba huko Turkana kuna aina mbalimbali ya bunduki za hali ya juu. Mhojiwa mmoja alisema, *'kuna ile unaweka kwa mshipi na inaonyesha risasi, na ingine kwa mabega na ni kama bomu'.* Hii inaonyesha dalili ya kwamba kweli kuna bunduki za rashasha na silaha nyingine za hali ya juu huko Turkana zipo.[45]

Pia, kuna uwezekano kwamba ni silaha chache tu ambazo hutumika katika visa vingi. Uwezekano huu unadhihirika huko Migori, ambapo kulisemekana kuwa kulikuwa na bunduki haramu 15 tu zilizokuwa zinatumika

katika eneo hilo kutekeleza takriban visa vyote vya uhalifu wa kutumia silaha au wizi wa mabavu.[46]

Upo uhusiano wa karibu kati ya utovu wa usalama na kuwepo kwa azma zaidi kutaka kumiliki bunduki ili kujihami na kujilinda. Kwa mfano, kuna wasiwasi kwamba vurugu za kisiasa zinazotokea mara kwa mara zinaweza kuwa zinakuza haja ya watu kutafuta bunduki katika maeneo fulani.[47] Kulingana na matokeo ya utafiti (angalia Jedwali 2.1), katika maeneo waishimo wafugaji wa kuhamahama, umiliki wa bunduki ndiyo tu unaosaidia ulinzi wa watu binafsi, familia na mali zao. Hii inaipa nguvu hisia kuwa eneo la Turkana lina bunduki nyingi.[48]

Katika utafiti wowote ule, ni changamoto kubwa kujaribu kupata makadirio ya kitaifa kuhusu idadi ya silaha ndogo ndogo haramu. Kulingana na takwimu zilizokusanywa kuhusu watu walioripoti kuwa wana silaha (kulingana na majibu ya wahojiwa wa HH pekee), inaweza kusemekana kwamba takriban asilimia 2.4 ya HHs nchini Kenya (ikiwa ni pamoja na wale ambao wako kwenye kaunti ambazo hazikujumuishwa kwenye utafiti huu[49]) wanamiliki angalau bunduki moja. Kulingana na majibu ya swali 'Kwa maoni yako, ni kaya ngapi katika eneo uishimo zenye kumiliki bunduki?', swali lililokuwa katika kila hojaji, kwa kila kikundi (HHs, LEAs, na CSOs), inaweza kukadiriwa kuwa kiwango hicho ni cha juu zaidi kuliko walivyosema wahojiwa wa HH. Makadirio haya ya 'juu' hutofautiana kwa vile inategemea ni nani aliyejibu maswali (jambo linaloashiria kuwa kuna viwango tofauti vya kueleweka kwa tatizo hili) na uathirikaji wa kaunti.

Jedwali 2.3 inaonyesha matokeo ya swali la moja kwa moja kuhusu umiliki ulioripotiwa na mtu binafsi (lililoulizwa HHs pekee), na takwimu stahilifu zilizokusanywa kutoka HHs, LEAs, na CSOs. Takwimu stahilifu zilitoa makadirio ya kiwango cha juu zaidi kuliko ripoti za kibinafsi, na kuashiria kwamba ueneaji wa bunduki unaweza kuwa zaidi ya mara tano ya kiwango cha ripoti za kibinafsi. Makundi yote ya wahojiwa yalithibitisha kwamba viwango vya umiliki vilikuwa vya juu zaidi ya vile vya ripoti za kibinafsi za wahojiwa wa kaya. Kwa hivyo, idadi ya bunduki haramu kote nchini inaweza kukadiriwa kuwa kati ya 210,000 (kulingana na ripoti za kibinafsi) na 1,150,000 (kulingana na makadirio ya juu, ukitilia maanani vikundi vyote). Ingawaje tofauti hii inaonekana kuwa kubwa, inaonyesha

**Jedwali 2.3** Makadirio ya umiliki wa bunduki katika HH kote nchini Kenya (hesabu zimefanywa kamili kukaribia 10,000)

| | | **Ripoti za kibinafsi** | | **Maoni kuhusu idadi ya HHs zinazomiliki bunduki katika eneo husika** | | | | | **Wastani** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uathirikaji wa kaunti | Jumla ya idadi ya HHs* | % | Hesabu ya ripoti ya kibi-nafsi | HHs | LEAs | CSOs | Makadirio ya juu zaidi | Hesabu ya maka-dirio ya juu zaidi | Wastani | Hesabu ya wastani |
| Juu | 2,159,115 | 4.7 | 100,000 | 13.3% | 20.9% | 16.8% | 20.9% | 450,000 | 12.8% | 280,000 |
| Wastani | 2,389,231 | 1.0 | 20,000 | 4.6% | 5.1% | 11.5% | 11.5% | 270,000 | 6.3% | 150,000 |
| Chini | 1,571,364 | 2.4 | 40,000 | 10.2% | 7.5% | 7.9% | 10.2% | 160,000 | 6.3% | 100,000 |
| Jumla ndogo | 6,119,710 | 2.7 | 170,000 | 9.1% | 14.5% | 12.4% | 14.5% | 890,000 | 8.6% | 530,000 |
| Kaunti ambazo Haziku-chungu-zwa | 2,648,244 | 1.6 | 40,000 | 6.5% | 6.1% | 9.9% | 9.9% | 260,000 | 5.8% | 150,000 |
| **Jumla** | **8,767,954** | **(2.4)**** | **210,000** | | | | **(13.1%)**** | **1,150,000** | **(7.8%)**** | **680,000** |

* Angalia majadiliano yaliyo hapo chini kuhusu utaratibu wa sampuli.

** Asilimia hizi zilikokotolewa upya kulingana na hesabu ya jumla iliyopatikana; angalia Kiambatisho 2.

**Marejeo:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

bayana tofauti kubwa kati ya ripoti za kibinafsi na wanavyoelewa wahojiwa wa HH na CSO, na LEAs. Utaratibu uliotumika kukadiria idadi ya bunduki ulijumuisha hatua ya kwanza yenye msingi katika kaunti 31 zilizofanyiwa utafiti, na ulihusisha kutumika kwa asilimia zilizopatikana kwenye sampuli ya jumla ya idadi ya HHs.[50] Kutokana na utaratibu wa sampuli[51] wakilishi uliotumika kwenye uchunguzi huu, kiwango cha chini (kuambatana na maeneo yenye uathirikaji wa kadiri na wa chini) baadaye kilitumiwa kwa idadi ya HHs katika kaunti 16 ambazo hazikufanyiwa uchunguzi. Jedwali 2.3 inaonyesha kwamba makadirio hayo yalisababisha matokeo ya viwango kuanzia kiwango cha chini cha 170,000/210,000 (ripoti za kibinafsi zisizojumuisha/zikijumuisha kaunti ambazo hazikuchunguzwa) na kiwango cha juu cha 890,000/1,150,000 (makadirio ya juu), huku kiwango cha kadiri kikiwa takriban kaya 530,000/680,000 zinazomiliki angalau bunduki moja (angalia sehemu V kwa maelezo ya utaratibu uliotumiwa).

## *Ufahamu kuhusu namna silaha zinapatikana*

Wahojiwa walisema kuwa bunduki nyingi zilikuwa zinamilikiwa na wahalifu: asilimia 29.5 ya wahojiwa wa LEAs na asilimia 34.8 ya wahojiwa wa CSO walidhani kuwa wahalifu wote wana bunduki.

KIIs na FGDs waliwatia lawamani vijana, wakiwa vikundi vya kihalifu au wapiganaji wenye bunduki. Kwa kuzingatia ukweli kwamba mizozo ya kiukoo au kikabila kaskazini mwa Kenya ni jambo la kawaida, kutambuliwa kunakojikita kwenye ukoo ni kikwazo dhidi ya usimamizi wa usalama. Hii ni kwa sababu kumshitaki mtu aliye na bunduki na anayetoka kwa jamii yako kunachukuliwa kama jambo linalozorotesha nguvu na hadhi ya jamii yako.[52]

Mara nyingi bunduki hununuliwa kutoka kwa wauzaji haramu, huku asilimia 57.6 ya wahojiwa wa HH, asilimia 77.4 ya LEAs, na asilimia 61.6 ya wahojiwa wa CSO wakithibitisha hivyo. Asilimia kubwa ya kiasi cha wahojiwa (asilimia 21.9), walidhani kuwa ni polisi ndiyo wanaogawa bunduki. Takwimu hii haikufanana na wanavyoelewa wahojiwa wa LEAs na CSO. Ni wachache sana kati yao waliodhani kuwa bunduki hutolewa na wenye bunduki au na wanasiasa viongozi (asilimia 6.3 na asilimia 9.7 mtawalia). Matokeo haya pia yanaonyesha kuwa kukodishwa kwa bunduki kutoka kwa maafisa wa usalama kunachangia padogo sana kwa utumizi wa bunduki haramu. Hakuna mhojiwa wa HH hata mmoja aliyeonelea hivi, na ni asilimia 2.7 pekee ya LEAs na asilimia 5.1 ya wahojiwa wa CSO waliosema kuwa maafisa wa usalama ndio chanzo cha bunduki.

Mitandao ya wauzaji na wagawaji imefichika, lakini wanajulikana na jamii. Inaaminika kuwa wana wadadisi wao wanaotafutatafuta hapa na pale kuwatambua wale wanaotaka kununua bunduki.[53]

Katika Mkoa wa Bonde la Ufa, wahojiwa walizumgumza kuhusu muuzaji bunduki haramu fulani anayetumia magari ya kibinafsi ili kusafirisha silaha kutoka Garissa hadi Nakuru. Nyakati fulani silaha hizo hufichwa ndani ya sukari au mizigo mingine.[54] Ni katika maeneo ya Nakuru, Samburu, na Trans-Nzoia ambapo shauku kali kuhusu kuhusika kwa polisi katika visa vya uhalifu ziliibuka. Kwa sababu hii, ni sharti kuwepo kwa taratibu muafaka za uwajibikaji, na kwa maafisa wa usalama kuchukua hatua za

udhibiti ili kukomesha visa vya wao kuhusika na uhalifu.[55] Huko Samburu, kulikuwa na wasiwasi kuhusu silaha mbalimbali zilizoachwa na Jeshi la Uingereza na ambazo hazikukusanywa, huku kukiwa na madai kwamba kulikuwepo na baadhi ya wenyeji wa jamii waliokuwa wakipata silaha na risasi kutoka kwa kambi za mafunzo za Jeshi la Uingereza.[56] Baadhi hutolewa kama zawadi baada ya kukamilika kwa mafunzo, huku wakati mwingine nyingine zilizokuwa zimefichwa zikifichuliwa na kuuzwa kwa bei nafuu.

Habari hizi zilithibitishwa na waliokuwa wanahojiwa, pamoja na walioshiriki katika FGD, waliosema kwamba kuna ulegevu fulani katika kuwajibikia kufuatilia silaha na risasi zinazoingizwa nchini, na zile zinazotumika wakati wa mazoezi ya jeshi na polisi. Nyakati nyingine, maafisa hushindwa kuelezea zilipo risasi wanazodai wametumia wakati wa mapigano au makabiliano, huku ukweli wa mambo ukiwa kwamba wameziuza au wamewapa jamii fulani.[57]

Wakati mwingi, ipo biashara ya uuzaji silaha haramu baina ya makabila, inayotegemea msimu na matukio fulani. Nyakati za misukosuko, bunduki zinahitajika kwa wingi na bei hupanda, huku wakati wa amani na haja iliyopo ikipungua basi bei hushuka.

Njia nyingine iliyotajwa ya kumiliki silaha ni kupitia kutwaliwa kutoka kwa maadui. Pia, kuna jamii chache ambazo hugawiana silaha, jambo linaloashiria kwamba zipo bunduki ambazo zinakodishwa kutoka kwa maafisa wa usalama. Hili ni jambo la kawaida mijini.

Lakini, katika maeneo yote matatu kaya ziliripoti ugumu mkubwa wa kuweza kupata silaha.[58] Kuna mwelekeo mzuri uliodhihirisha kwamba kuimarisha usalama (kupunguza uathirikaji) kuna uhusiano wa karibu na kuongezeka kwa ugumu wa kununua bunduki, kwa makundi yote matatu ya uchunguzi. Mwelekeo huu ni dhabiti zaidi miongoni mwa kundi lililochunguzwa la HH (angalia Mchoro 2.3).


Kulingana na washiriki wa FGD, huko Mandera kulikuwa na wakati ambapo silaha zilikuwa zinaweza kununuliwa kwa urahisi sana sokoni.[59] Aidha kuna soga za ujasiri na hali ya kutojali kuadhibiwa zinazohusiana na namna silaha zinavyopatikana.[60]

Kiashirio cha muhimu kinachoonyesha kiwango cha idadi na kusambaa kwa silaha ni kile wahojiwa huchukulia kuwa silaha za kawaida. Makundi

yote ya wahojiwa (HHs, LEAs, na CSOs) walisema kuwa silaha butu na zenye bapa ndizo zilizopatikana kwa wingi (angalia Michoro 2.4, 2.5, 2.6, na 2.7). Silaha zaidi zenye bapa zimeripotiwa na kaya katika maeneo yenye uathirikaji wa kadiri kuliko ilivyothibitishwa na wahojiwa wa LEAs au CSO. Kinyume cha hayo, bunduki ndogo zimeripotiwa kwa kiasi kikubwa zaidi na wahojiwa wa LEAs na CSO kuliko wahojiwa wa HH. Badala yake, HHs zimeripoti kiwango kikubwa zaidi cha silaha ndogo katika maeneo yenye fujo kuliko maeneo yenye uathirikaji wa wastani na wa chini.

Fauka ya hayo, wahojiwa wa HH waliripoti idadi kubwa zaidi ya bunduki kubwa aina ya 'rifle' na 'shotgun' katika maeneo yenye uathirikaji wa juu kuliko katika maeneo yale mengine mawili yenye kiwango kidogo cha ukosefu wa usalama. Lakini wahojiwa wa CSO waliripoti kuwepo kwa silaha hizo kwa wingi katika maeneo yenye uathirikaji wa viwango vya juu na vya kadiri, ikilinganishwa na wahojiwa wa HH. Katika maeneo yote, wahojiwa wa LEAs na CSO waliripoti idadi kubwa zaidi ya 'rifles/shotguns' kuliko wahojiwa wa HH.


**Mchoro 2.3** Hisia kuhusu urahisi wa upatikanaji wa bunduki,* kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




* Alama ya wastani ya utambuzi wa upatikanaji kwa kiwango cha 1 = rahisi hadi 3 = ngumu.


**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 2.4** Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba silaha zenye bapa ni kawaida katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs)





Duru: KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 2.5** Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba bastola ndogo ni nyingi katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs)





**Duru:** KNFP na Small Arms Survey, 2011.

**Mchoro 2.6** Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba bunduki za marisaa ni nyingi katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti na makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 2.7** Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba bunduki za rashasha ni nyingi katika eneo lao, kwa uathirikaji wa kaunti kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Vilevile, wahojiwa wa HH waliripoti kuwepo kwa silaha za kiotomatiki katika maeneo yenye fujo kuliko yale yanayoathiriwa kwa viwango vya wastani na vya chini. Wahojiwa wa LEAs na CSO, kwa upande mwingine, waliripoti idadi kubwa zaidi ya silaha za kiotomatiki katika maeneo yote matatu, kuliko wahojiwa wa HH. Pamoja na hayo, wahojiwa wa LEAs na CSO waliripoti idadi kubwa zaidi ya silaha za kiotomatiki katika maeneo ambayo hukumbwa na fujo kuliko maeneo yenye uathirikaji wa kadiri na wa chini.

Matokeo haya yanaashiria kuwa wahojiwa wa LEAs na CSOs walikuwa wazi zaidi walipokuwa wanajibu maswali na kutoa habari, au wahojiwa wa HH hawakuelewa kikamilifu zilipo na zinavyotumika silaha kama wenzao, na hivyo wakatoa makadirio ya chini zaidi. Hata hivyo, jambo moja lililojitokeza na la maana ni kwamba katika maeneo yenye fujo, makundi yote ya wahojiwa yaliashiria kuwa silaha za kiotomatiki zilipatikana kwa wingi zaidi kuliko bunduki za kawaida, na hivyo kuthibitisha kwamba bunduki hizo kwa kweli zinapatikana kwa wingi.

Kwa kweli, wakati wa mahojiano, pamoja na FGDs, bunduki aina ya AK-47 zilitajwa kuwa bunduki zilizotumika kwa wingi zaidi katika visa vya uhalifu na vurugu kote nchini, huku bunduki aina ya G3 zikihusishwa

na maghala ya serikali ya silaha (Jedwali 2.4). Hata hivyo, kupatikana kwa aina nyingine za silaha hutegemea eneo husika na zitokako silaha hizo. Kwa mfano, katika eneo la juu la Mkoa wa Mashariki, washiriki walitaja bunduki ambazo kwa kawaida hupatikana huko Ethiopia, kama za aina ya FN na M16.[61]

**Jedwali 2.4** Baadhi ya bunduki/silaha zilizotajwa katika FGDs

| Mandera | AK-47s, G3s, maguruneti, mabomu |
|---|---|
| Marsabit | AK-47s, G3s, Mark 4s, M16s, FNs |
| Lokichoggio | AK-47s, Mark 4s, HK11s, maguruneti, bunduki za aina ya LPG, MANPADS* |
| Pokot Magharibi | AK-47s, G3s, bunduki za LPG, bunduki zilizotengenezwa nyumbani |
| Samburu | AK-47s, G3s, M16s |
| Migori | AK-47s, bunduki zilizotengenezwa nyumbani |
| Kilifi | AK-47s, bunduki za LPG |
| Mombasa | AK-47s, bastola, 'shotguns' |

* Silaha za kudhibiti anga zinazoweza kubebwa na mtu.
**Marejeo:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Umilikaji silaha huwa ni jambo la kisiri na kwa hivyo wengi wa wahojiwa wa LEAs na CSO walionelea njia za kuhifadhi bunduki kama siri za kibinafsi, kama inavyoonekana katika Jedwali 2.5.

**Jedwali 2.5** Hisia za wahojiwa kuhusu mahala silaha zinapohifadhiwa (LEAs na CSOs)

| Hifadhi | LEAs | CSOs |
|---|---|---|
| Ni siri ya mtu binafsi | 66% | 56% |
| Majumbani | 20% | 25% |
| Kwenye mashamba | 5% | 4% |
| Kwenye maghala ya siri ya jamii | 5% | 2% |
| Sijui | 4% | 13% |

**Marejeo:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Lakini, katika maeneo ya wafugaji wa kuhamahama ni jambo la kawaida kuwaona walisha mifugo wakiwa wamebeba silaha. Tabia hii inatilia mkazo thamani kubwa ya mifugo kwa jamii hizi kama njia muhimu ya kujipatia

riziki. Pia inathibitisha kiwango cha uhasama kati ya vikundi tofauti, kama sababu mojawapo inayokuza ongezeko la silaha. Kwa mfano, huko Samburu Kaskazini, ambapo wakati wa utafiti huu kulikuwa na uhasama kati ya Wasamburu na majirani zao Waturkana na Wapokot, *wamorani* wanaolisha mifugo yao walitembeatembea huku wakiwa wamebeba bunduki zao.[62]

## Viashirio vya hisia kuhusu athari za silaha ndogo ndogo

Huku viashiria vya athari za silaha ndogo ndogo vikitiwa maanani, utafiti huu uliangazia namna tofauti za utovu wa usalama unaoletwa na silaha ndogo ndogo, vifo kutokana na kupigwa risasi na majeraha.

### *Vifo kutokana na kupigwa risasi na/au majeraha*

Huku wahojiwa wengi wa LEAs (asilimia 57.1) na CSO (asilimia 47.5) wakiamini kuwa kati ya mwathiriwa mmoja na watano wanauawa kwa kupigwa risasi au kujeruhiwa kila mwezi, kuna idadi kubwa hata hivyo iliyoonelea kuwa hakuna vifo wala majeruhi (asilimia 31.1 kati ya wahojiwa wa LEAs na asilimia 35.0 kati ya CSO) (Jedwali 2.6).

**Jedwali 2.6** Hisia za wahojiwa zinazoonyesha ni mara ngapi vifo au majeraha hutokea kupitia mtutu wa bunduki (LEAs na CSOs)

| | LEAs | CSOs |
|---|---|---|
| Waathiriwa 1–5 kwa mwezi | 57.1% | 47.5% |
| Hakuna vifo wala majeruhi | 31.1% | 35.0% |
| Waathiriwa 6–10 kwa mwezi | 6.0% | 8.5% |

**Marejeo:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

### *Athari za silaha ndogo ndogo*

Kuna hisia moja muhimu miongoni mwa wahojiwa wa HH yenye kiwango cha wastani cha majibu cha asilimia 30.7, ya kwamba silaha ndogo ndogo haramu zina uhusiano wa karibu sana na uzorotaji wa usalama. Ukosefu huu wa usalama katika maeneo kadhaa nchini ndiyo unaokuza biashara ya silaha

hizi. Kwa mfano, kwa sababu ya ukame kaskazini mwa Kenya mwanzoni mwa mwaka 2011, jamii wenyeji zilipoteza mifugo yao, jambo lililowapa msukumo kujaribu kuongeza idadi ya mifugo kwa njia ya uvamizi, na wizi wa mifugo. Katika maeneo yaliyokumbwa na ghasia za baada ya uchaguzi mwaka 2007, usalama sasa umeimarika na visa vya uhalifu vimepungua, kulingana na takwimu za Idara ya Polisi ya Kenya 2008. Kuboreka huku kwa kiasi fulani ni kwa sababu ya juhudi za uimarishaji amani na usimamizi wa usalama katika maeneo husika kupitia kamati za amani na majopokazi yanayoshughulika na silaha ndogo ndogo na zile nyepesi.


Kwa sababu ya tabia ya wafugaji wa kuhamahama kumiliki bunduki, kuna nyakati watu wa jamii hizo hutumia bunduki ili kuamua mizozo midogomidogo. Kwa mfano, wakati wa FGD huko Samburu, ilisemekana kwamba wakati mwingine *wamorani* hata hufikia hatua ya kutumia bunduki (AK-47s) ili kuamua ugomvi kuhusu wapenzi wao.[63] Huko Marakwet, ukosefu wa usalama umekithiri—kuna visa vya vijana waliojihami kwa silaha kuwaibia watu ambao wametoka kuuza mifugo wao, au yeyote yule anayeshukiwa kuwa ana pesa.[64]

Viashiria fulani vinavyodhihirisha ukosefu wa usalama kwa binadamu ni kama ghasia ambapo silaha hutumika na athari zake za moja kwa moja (vifo na majeraha), kupotea kwa mali na/au kuharibiwa kwake, ukosefu wa chakula na wa ajira, vitendo vya kikatili vinavyohusu mapenzi, na hali zinazowalazimu watu kuhama, miongoni mwa nyingine. Kuna fikra inayozidi kukua kwamba visa vya ghasia ambapo silaha hutumika vinapungua, huku wizi wa mifugo nao pia ukipungua.

## Mahali silaha ndogo ndogo zitokako na ziendako


Wahojiwa wa LEAs na CSO walitoa habari zaidi kuhusu kutokako na kwendako bunduki, kuliko familia katika kaya. Lakini vikundi vyote, katika ripoti zao, vilikubaliana kwamba silaha nyingi huingizwa Kenya kutoka kwa nchi jirani. Kumbukumbu za wahojiwa kuhusu silaha katika jamii zilirudi nyuma hadi Karne ya 19 wakati Wasomali walipata bunduki ya kwanza huko Mkoa wa Kaskazini Mashariki au Turkana huko Kaskazini mwa Bonde la Ufa.[65]

**Mchoro 2.8** Asilimia ya wahojiwa inayoonyesha nchi jirani kama chanzo cha silaha na risasi haramu katika maeneo yao, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)


**Mchoro 2.9** Asilimia ya wahojiwa inayoonyesha wauzaji silaha haramu/wafanyabiashara ya silaha haramu kuwa chanzo kikuu cha silaha na risasi hizo katika maeneo yao, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba ilhali idadi ya wahojiwa wa HH wanaotaja nchi jirani kama chanzo cha silaha ilikuwa ya chini kuliko ile ya wahojiwa wa LEA na CSO, hii ni kinyume na wanavyohisi wao kuhusu walanguzi wa silaha. Hivyo basi idadi kubwa zaidi ya wahojiwa wa HH kuliko wahojiwa wa LEA na CSO walionelea kwamba silaha zilitoka kwa wafanyabiashara haramu wa silaha—ambao pia huenda wanaendesha biashara yao katika nchi mbalimbali—katika maeneo yenye uathirikaji wa kiwango cha wastani (angalia Michoro 2.8–2.10).

**Mchoro 2.10** Asilimia ya wahojiwa wanaoonyesha maghala ya serikali ya silaha (polisi, jeshi) kama chanzo kikuu cha silaha na risasi haramu kwenye maeneo yao, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs,na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Kwa maoni ya wengi, Somalia ndilo eneo ambapo silaha nyingi hutoka na kuingizwa Kenya, lakini bunduki zadhaniwa zinatoka Ethiopia, Uganda, na Sudan Kusini, pia. Wahojiwa wa Nyanza kusini na Pwani kusini walisema ni silaha chache sana zitokazo Tanzania, na hivyo nchi hiyo huchangia padogo sana kwa tatizo hili la bunduki.

Yasemekana kuwa walanguzi wa silaha hutumia wanyama, kama punda, ili kusafirisha bunduki. Pia, wao huzificha kwenye mizigo/au magari yasafirishayo mifugo hadi mijini ili ziuzwe. Bunduki hizi hufichwa ndani ya mchanga, makaa, mafuta ya kupikia, miongoni mwa bidhaa nyingine. Wahojiwa walisema kuwa walanguzi wa silaha hutumia wenzao walioko Somalia, au katika miji iliyopo mipakani—kama Mandera na Garissa—ili kusafirisha kinyemela bunduki hizo hadi mwisho wa safari.[66]

Hatimaye, LEAs walioko kwenye maeneo yenye viwango vya uathirikaji vya kadiri na vya chini walikuwa hawana la kusema kuhusu kama ilikuwa kweli maghala ya serikali ya silaha ndipo patokapo bunduki (Mchoro 2.10). Lakini wale kutoka maeneo ambayo kuna uwezekano wa kuzuka fujo wakati wowote walikiri kwamba kulikuwa na uwezekano wa jambo hilo kuwa la kweli (asilimia 1.6). Labda ni kwa sababu ya kuwepo kwa visa vingi

vya uhalifu vinavyotumia silaha haramu.[67] Ingawaje kati ya asilimia 4.2 na 6.9 ya wahojiwa wa HH kote walitaja ghala za silaha za serikali kama chanzo mojawapo ambapo silaha hutoka, asilimia kubwa walikuwa wahojiwa wa CSO katika maeneo yenye uathirikaji wa kiwango cha chini (asilimia 8.1). Wahojiwa wa CSO katika maeneo ya uathirikaji wa kadiri hawakukubaliana na maoni haya.

**Jedwali 2.7** Njia za ulanguzi na namna ya usafirishaji

| Eneo | Chanzo kikuu | Namna* | Njia |
|---|---|---|---|
| Nairobi | Somalia, Uganda, Sudan | Barabara, reli, magari ya serikali, watu binafsi | Garissa–Eastleigh<br>Lodwar–Eldoret–Nakuru<br>Mombasa–Nairobi<br>Maralal–Nyahururu–Nairobi<br>Ethiopia–Moyale–Isiolo–Nairobi |
| Eneo la Kati mwa Kenya | Somalia, Uganda, Sudan | Barabara, watu binafsi | Isiolo–Nyeri<br>Nairobi–Thika<br>Nairobi–Kiambu |
| Pwani | Somalia, Tanzania | Barabara, meli, mashua | Lunga Lunga–Mombasa<br>Kiunga–Lamu–Malindi–Mombasa<br>Ocean–bandari kadhaa & majumba–Mombasa |
| Kaskazini Mashariki | Somalia, Ethiopia | Barabara, watu, wanyama | Somalia–Mandera<br>Somalia–Garissa<br>Mandera–Wajir<br>Ethiopia–Mandera–Wajir |
| Kanda ya Juu ya Mashariki | Somalia, Ethiopia | Barabara, wanyama, wafanyabiashara, magari ya serikali | Moyale–Marsabit–Isiolo<br>Garissa–Isiolo–Marsabit |
| Kaskazini mwa Bonde la Ufa/ Magharibi | Somalia, Ethiopia, Sudan, Uganda | Barabara, wafanyabiashara, jamii hadi jamii | Sudan–Lokichoggio–Lodwar–Kapenguria–Eldoret<br>Ethiopia–Maralal–Nyahururu<br>Kapenguria–Tot–Kapedo<br>Uganda–Lodwar<br>Uganda–Kapenguria–Kitale–Bungoma |
| Bonde la Ufa Kati | Somalia, Ethiopia, Sudan, Uganda | Barabara, wafanyabiashara, jamii hadi jamii | Kitale–Eldoret–Nakuru<br>Nairobi–Naivasha–Nakuru<br>Nyahururu–Nakuru |
| Nyanza Kusini | Tanzania | Barabara, wafanyabiashara, jamii | Tanzania–Isebania–Kisii |

* Silaha ndogo ndogo hufichwa ndani ya mizogo, wanyama waliokufa, makaa, na kwingineko, au zinabebwa na watu binafsi.

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Jedwali 2.7 ni muhtasari wa maeneo na mahali kutokako silaha ndogo ndogo, njia zinakopita, na jinsi silaha hizo huingizwa katika eneo hili. Haya yalielezewa wakati wa FGDs katika maeneo yote yaliyofanyiwa utafiti.

**Jedwali 2.8** Makadirio ya gharama ya bunduki (KES*)

| Eneo | Aina na bei ya bunduki | Bei ya risasi (kwa kila risasi) |
|---|---|---|
| Mandera | AK-47: 35,000<br>G3: 25,000 | |
| Marsabit | G3: 40–60,000<br>AK-47: 60,000 | 100–150 |
| Lokichoggio | AK-47: ng'ombe 4–6 (30,000–60,000) | |
| Samburu | G3: 50,000–70,000<br>AK-47: 30,000–40,000<br>M16: 45,000 | G3: 50<br>AK-47: 150 |
| Tana River | AK-47: 30,000–40,000 | |
| Mombasa | Bastola: 15,000<br>AK-47: 30,000<br>Kukodisha bastola: 3,000 | |
| Garissa | AK-47: 10,000–40,000 (au ndume moja au mbili, kwa kutegemea ukubwa wake | Bei ya moja ni shilingi 5; lakini bei hushuka pindi mnunuzi anaponunua risasi zaidi |
| Nakuru | Kiasi cha awali cha kukodisha bunduki kwa siku kilikuwa 3,000, lakini kuna uwezekano kuwa kimepanda | |
| Nairobi | Kodi inategema itakavyotumika bunduki hiyo, kwa mfano:<br>Ikitumika kwenye maeneo ya makazi: 25,000<br>Kwa mfanyabiashara: 50,000<br>Ili kutekeleza wizi kwenye eneo kubwa la biashara: 70,000<br>Kukodisha pingu: 2,000<br>Bei zilikuwa za juu sana wakati kulipotokea visa vingi vya wizi vya mabenki | |
| Mt Elgon | AK-47: 15,000–40,000 | |
| Trans-Nzoia | AK-47: 15,000–45,000<br>Kuna visa vya kukodishwa kwa bunduki) | |

* Shilingi za Kenya 84 = USD 1 mnamo Aprili 2011.

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

## Gharama ya silaha ndogo ndogo

Kiwango cha ufahamu kuhusu gharama ya silaha ndogo ndogo miongoni mwa wahojiwa kilitofautiana (Jedwali 2.8). Kuna uwezekano kuwa baadhi yao walidhani watajitia matatani wakikadiria gharama za bunduki. Lakini kwa jumla, bei ya bunduki na risasi ilitegemea umbali wa eneo husika kutoka chanzo cha silaha hizo.[68]

Ikitiliwa maanani kwamba mapato katika jamii hizi ni ya chini, silaha ni ghali, na hii inashinikiza upya sababu za jamii, hasa za wafugaji wa kuhamahama, kufanya juu chini ili kuhakikisha usalama wao. Pia, kuna gharama nyingine zinazoambatana na udumishaji, kama vile utunzaji na ununuzi wa risasi.

## Silaha ndogo ndogo, uhalifu na ghasia: uchunguzi wa masaibu ya waathiriwa


### *Maoni ya jumla*

Ndani ya uchunguzi mpana, kulikuwa na uchunguzi mwingine kuhusu masaibu ya waathiriwa waliokumbana na ghasia ambapo silaha zilitumika, na visa vya uhalifu, hasa vurugu zinazohusisha bunduki. Uchunguzi huu uligundua kwamba usalama, kwa ujumla, umeimarika katika maeneo yenye uathirikaji wa chini, ikilinganishwa na yale yenye viwango vya uathirikaji wa wastani na wa juu. (Mchoro 2.11). Masuala ya usalama katika maeneo ambayo kuna uwezekano wa kutokea kwa fujo yanaathiriwa na vipengele kadhaa, vikiwemo hali ya hewa, uhusiano kati ya makabila, tamaduni, na siasa, miongoni mwa nyingine. Kuweko kwa vitisho vingi kwa wakaazi wa maeneo yanayoathiriwa na vurugu kwa urahisi kunaelezea ni kwa nini imani yao kuhusu usalama ni ya chini kuliko wengine.

Asilimia 42 ya wahojiwa wa HH walihofia kuwa kulikuwa na uwezekano kuwa wangekuwa waathiriwa wa vurugu/na au uhalifu mwakani. Utathmini wa hisia za watu binafsi, na wa jamii kuhusu usalama, ulidhihirisha kwamba watu huwa na wasiwasi kuhusu usalama wao zaidi wakati wa uchaguzi, na asilimia 48.4 ya wahojiwa wa HH walionelea hivyo. Uchunguzi pia uligundua kuwa idadi kubwa (asilimia 42.5) ya wahojiwa wa HH hawakuwa

wakihisi kuwa salama walipokuwa nje ya nyumba zao usiku, na zaidi ya theluthi moja (asilimia 37.2) hawakujihisi kuwa salama hata walipokuwa ndani ya nyumba zao. Hata hivyo, ni wazi kwamba wengi wa wahojiwa wa HH walijihisi kuwa salama, popote walipokuwa na saa zotezote (angalia Jedwali 2.9).

**Mchoro 2.11** Hisia za wahojiwa wa HH kuhusu usalama mwaka 2011 ikilinganishwa na mwaka moja uliopita,* kwa uathirikaji wa kaunti




* Alama wastani ya hisia za usalama kwa kiwango cha 1 = mbaya zaidi na 3 = bora.

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Jedwali 2.9** Hisia za viwango vya usalama (maeneo na saa mbalimbali)


| Muktadha/wakati wa mchana au usiku | Si salama | Salama |
|---|---|---|
| Usalama nje ya nyumba mchana, wakati wa kampeni za kisiasa | 48.4% | 50.0% |
| Usalama nje ya nyumba usiku/gizani | 42.5% | 57.2% |
| Usalama nyumbani usiku /kwenye giza | 37.2% | 62.7% |
| Usalama nje ya nyumba mchana wakati wa sherehe | 26.5% | 72.6% |
| Usalama nje ya nyumba mchana, wakati wa mavuno | 23.0% | 75.5% |
| Usalama nje ya nyumba mchana, msimu wa mvua | 19.9% | 79.0% |
| Usalama nje ya nyumba wakati wa mchana, msimu wa kiangazi | 16.3% | 82.6% |
| Usalama wanapotembea peke yao kutoka nyumbani kuelekea sokoni mchana/kukiwa mwangaza | 13.9% | 86.0% |
| Usalama wanapotembeatembea sokoni mchana | 13.9% | 85.7% |
| Usalama nje ya boma mchana, umbali wa dakika moja kutoka nyumbani | 10.9% | 89.0% |
| Usalama ndani ya nyumba, mchana/kukiwa mwangaza | 8.8% | 91.2% |

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

*Masaibu ya waathiriwa*

Kama ilivyotarajiwa, wahojiwa wa HH katika maeneo yenye uathirikaji wa kiwango cha chini walikumbana mara chache tu na hatari ya kuathiriwa na uhalifu, ikilinganishwa na wale walioko kwenye maeneo yenye uathirikaji wa kadiri na wa juu (Mchoro 2.12).

**Mchoro 2.12** Tajriba ya kuathiriwa na uhalifu miongoni mwa wahojiwa wa HH mwaka 2011, kwa uathirikaji wa kaunti





**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Kwa ujumla, asilimia 21.1 ya wahojiwa wa HH waliathiriwa na visa vya uhalifu au ghasia katika mwaka uilotangulia. Kati yao, asilimia 46.8 walikumbwa mara moja, huku asilimia 53.2 wakikumbwa mara mbili au zaidi. Kunakuwa na visa vichache zaidi pale ambapo usalama unaimarika (angalia Mchoro 2.12): jinsi kiwango cha uathirikaji cha eneo husika kilivyo juu ndivyo uwezekano wa walioko kwenye kaya kuripoti kuwa waathiriwa. Hii ni kinyume na takwimu kutoka kwa Idara ya Polisi Kenya, ambapo eneo la kaskazini-mashariki mwa Kenya ndilo lililokuwa na takwimu za chini zaidi (Kenya Police, 2010, uk. 2).

Visa vingi vya uhalifu katika maeneo yenye uathirikaji wa kiwango cha chini vilitokea nyumbani. Visa katika maeneo yenye uathirikaji wa juu vilitokea katika maeneo mbalimbali, huku takriban theluthi moja vikitokea majumbani, theluthi nyingine barabarani/mtaani, na asilimia 18 katika makao ya watu binafsi. Visa vya uhalifu katika maeneo yenye uathirikaji wa wastani mara nyingi vilitokea barabarani au mtaani. Visa vya uhalifu

kwenye makao ya watu binafsi, mara nyingi, vilitokea katika maeneo yenye uathirikaji wa juu. Makundi yanayoishi katika maeneo yenye viwango vya kadiri na vya chini vya uathirikaji kwa ujumla siyo ya kuhamahama na yana kiwango cha juu zaidi cha ukuzaji miji, na hivyo basi kuna uwezekano mkubwa wa kuweko kwa visa vingi vya uhalifu majumbani na mitaani au barabarani (Mchoro 2.13).

**Mchoro 2.13** Eneo la uhalifu uliokumba wahojiwa wa HH, kwa uathirikaji wa kaunti




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Vingi kati ya visa vya uhalifu na ghasia vilivyowakumba au kushuhudiwa na wahojiwa vilisababisha vifo na/au majeraha (asilimia 60.9). Kulingana na majibu, hesabu ya walioumia inaonyesha ya kwamba mamia wameuawa au kujeruhiwa. Kwa ujumla, wahojiwa wa HH walikiri kwamba watu 264 wa kaya zao walijeruhiwa na wengine 260 kuuawa baada ya visa vya uhalifu au vurugu.


Visa hivi mara nyingi vilitokea usiku, kulingana na asilimia 65.4 ya wahojiwa walioathiriwa. Ni asilimia 34.6 pekee ya wahojiwa ambao walikumbwa na visa vya uhalifu au vurugu mchana. Mara nyingi, hawakuwafahamu waliowadhuru (asilimia 62.6). Ni asilimia 35.7 pekee ya waathiriwa waliowajua waliowashambulia kwa jina au sura.

Visa vingi vya uhalifu vilivyotokea mara kwa mara vilivyokuwa vinawakumba wahojiwa wa kaya vilikuwa vya wizi wa nguvu/wizi, na vilikuwa asilimia 61.2 ya visa vyote; vikifuatwa na vya vitishio/shuruti (asilimia 20.9);

na vya uvamizi, kupigwa, kupigwa risasi, au kupigana (asilimia 14.0; angalia Jedwali 2.10). Visa vilivyokuwa na uzito zaidi, kama pale ambapo mtu aliuawa, vilikuwa asilimia 15.6, vikijumuisha vya mauaji ya makusudi (asilimia 7.1), mauaji ya kulipiza kisasi (asilimia 5), na mauaji kwa kutokusudia (asilimia 3.5).

Kwa ujumla, zaidi ya theluthi moja ya waathiriwa wa uhalifu au vurugu za kutumia nguvu walikabiliana na bunduki (Mchoro 2.14). Miongoni mwa bunduki, silaha za kiotomatiki ndizo zilizotumiwa kwa wingi zaidi (asilimia 16.8), zikifuatiwa na bunduki aina ya 'handgun' (14.5 per cent). Silaha zenye bapa kama visu na mapanga, na za kitamaduni zilitajwa katika takriban robo moja ya visa, ilhali katika asilimia 19 ya visa hakuna silaha yoyote iliyotumiwa.

**Mchoro 2.14** Silaha zinazotumika katika visa vya uhalifu au ghasia




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Wengi wa waathiriwa wa HH wa visa vya uhalifu au ghasia (asilimia 85.5) walipiga ripoti kwa vyombo vya dola husika. Visa vingi viliripotiwa kwa polisi (katika asilimia 64 ya visa) na utawala wa mikoa (katika asilimia 21.5 ya visa). Katika visa vichache, ni jamaa zao ndiyo waliofahamishwa (katika asilimia 4.6 ya visa) au viongozi wa kitamaduni (katika asilimia 4 ya visa; angalia Jedwali 2.11).

Licha ya kutegemewa kwa maafisa wa kudumisha sheria hapo awali, zaidi ya robo moja ya waathiriwa waliohojiwa waliokuwa wamepiga ripoti kwa polisi (asilimia 26.8) walisema kuwa hawakufanya lolote. Asilimia nyingine 26.2 ya waliohojiwa nao walisema kwamba maafisa hao wa kudumisha sheria walikuwa wangali wanashughulikia mashtaka waliopewa. Ni asilimia 13.7 tu waliosema kuwa adhabu rasmi ilitolewa, huku asilimia 10.6 wakisema kuwa

kulitolewa adhabu isiyokuwa rasmi (ikiwa ni pamoja na watu kujichukulia sheria mkononi mwao).

**Jedwali 2.10** Aina ya uhalifu au ghasia (majibu kadhaa)

| Aina ya kisa | % ya visa |
|---|---|
| Wizi wa mabavu/wizi | 61.2 |
| Vitishio/shuruti | 20.9 |
| Uvamizi/kichapo/kupigwa risasi/kupigana | 14.0 |
| Vurugu za makundi ya kihalifu | 8.1 |
| Mauaji ya kukusudia | 7.1 |
| Mauaji ya kulipiza kisasi | 5.0 |
| Mapigano kati ya koo | 3.8 |
| Mauaji bila kukusudia | 3.5 |
| Ubakaji/dhulumua za kimapenzi | 3.3 |
| Dhuluma za kinyumbani | 2.2 |
| Mengine | 1.9 |
| Uuzaji wa dawa za kulevya | 1.6 |
| Utekaji nyara | 0.7 |

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Jedwali 2.11** Wale walioambiwa kuhusu visa vya uhalifu/vya kutumia nguvu

| Taasisi/wahusika | % ya visa |
|---|---|
| Polisi | 64.0 |
| Utawala wa mikoa | 21.5 |
| Familia | 4.6 |
| Viongozi wa kitamaduni | 4.0 |
| Majirani | 2.7 |
| Marafirki | 1.0 |
| Viongozi wa kidini | 0.6 |
| Jeshi | 0.6 |
| Sungusungu | 0.4 |
| Watoaji ulinzi wa kibinafsi | 0.3 |
| Sijui | 0.3 |

**Kumbuka:** Jumla ya safu ya mkono wa kulia huenda isitimie asilimia 100 kutokana na nambari kufanywa kamili.
**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Asilimia 17.5 ya waathiriwa hawakupiga ripoti kwa mtu yeyote. Wengi wao walisema kwamba ni kwa sababu hawakuwa na imani na polisi wala maafisa wa utawala (asilimia 40.6; angalia Jedwali 2.12).

**Jedwali 2.12** Sababu za kutoripoti visa vya vya uhalifu/vya kutumia nguvu

| Majibu | % ya visa |
|---|---|
| Kutokuwa na imani na polisi/wenye mamlaka | 40.6 |
| Nilisuluhisha tatizo mwenyewe | 26.2 |
| Nyingine | 25.9 |
| Polisi/wenye mamlaka wako mbali au hawapo | 4.1 |
| Sijui | 1.3 |

**Kumbuka:** jumla ya safu ya mkono wa kulia huenda isitime asilimia 100 kutokana na nambari kufanywa kamili.
**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Matokeo haya yanadhihirisha haja kubwa ya kuimarisha uwezo rasmi, na wa eneo husika, wa kusimamia usalama kwa njia zinazohakikisha haki na zinazopunguza viwango vya majeruhi. Uwezo huo, au mikakati hii inafaa iwe pamoja na kuweko kwa tahadhari za mapema na taratibu za kuchukua hatua, na mifumo mwafaka ya kiusalama. Huu ndiyo msingi wa uchanganuzi katika sehemu ifuatayo.

# III. Uwezo wa Kenya kudhibiti silaha ndogo ndogo

## Utangulizi


Shuguli moja muhimu ya uchunguzi huu ilikuwa kukadiria jinsi Wakenya wa tabaka mbalimbali wanavyochukulia juhudi zinazoendelea za serikali za kupunguza kuenea kwa bunduki haramu. Waliohojiwa waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu vipengele kadhaa vinavyohusika na hali ya usalama kwa ujumla, juhudi za Kenya za kuudhibiti usalama nchini na mipakani kupitia utungaji na udumishaji sheria, kampeni za kuwahamasisha watu, na mikakati mingine.

Uchanganuzi ulitilia maanani majibu kutoka uchunguzi wa HHs, CSOs, na LEAs, pamoja na FGDs na KIIs. Mfumo uliojikita kwenye msingi wa kiwango cha kuathirika kwa kaunti, sawa na ule uliotumiwa katika sehemu nyingine, ulitumiwa hapa. (angalia sehemu za I na V).

## Mafanikio kwa ujumla ya kudhibiti silaha haramu

Wahojiwa waliambiwa watathmini kiwango cha mafanikio ya serikali katika juhudi zake za kujaribu kudhibiti kuenea kwa silaha ndogo ndogo haramu katika miaka michache iliyopita. Ingawaje asilimia 75.5 ya LEAs walisema kuwa juhudi za serikali za kudhibiti silaha zilikuwa zimefaulu, ni CSOs wachache zaidi (asilimia 55.9) waliokubaliana na wazo hilo. Ingawa asilimia 42.4 ya CSOs waliohojiwa walionelea kuwa serikali haikufaulu katika juhudi zake, ni asilimia 24.2 tu ya LEAs waliosema hivyo pia (angalia Mchoro 3.1). Ikizingatiwa kuwa LEAs ni maafisa wa serikali, basi maoni ya wahojiwa wa CSOs ndiyo yenye msukumo zaidi. Kwa mfano, wawakilishi wa jamii wakati wa mijadala ya FGDs iliyofanywa hawakufurahishwa na kushindwa kwa serikali kuwadhibiti maafisa polisi wanaojihusisha kwenye visa vya uhalifu na magendo ya silaha, na pia kushiriki kwa KPRs katika visa vya utovu wa usalama.[69]

**Mchoro 3.1** Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kwamba Kenya imefanikiwa katika kudhibiti silaha ndogo ndogo katika muda wa miaka mitano iliyopita, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Swali lingine kama hilo lililolenga kutathmini maoni kuhusu iwapo mikakati ya udhibiti silaha imefanikiwa lilizua majibu yaliyokuwa yanaweza kulinganishwa (Mchoro 3.2). Huku maoni ya wadumishaji sheria yakiwa yamegawanywa baina ya wale walioonelea kwamba mikakati ilikuwa imefaulu (asilimia 49.7) na wale walioonelea kuwa mikakati hiyo ilikuwa duni (asilimia 48.2), wengi wa wahojiwa wa CSO (asilimia 71.1) walionelea kwamba udhibiti silaha ulikuwa duni.

Maoni ya jamii kuhusu utendaji na juhudi za serikali za kudhibiti silaha yalikuwa ya tahadhari. Kulingana nao, kukithiri kwa utovu wa usalama na changamoto kuhusu silaha zinainyooshea kidole cha lawama serikali: serikali inaonekana kana kwamba haijatilia mkazo tatizo hili, kutokana na mikakati na sera zake dhaifu. Serikali inachukuliwa kana kwamba haitaki kusuluhisha kikamilifu tatizo sugu la silaha ndogo ndogo, au imeshindwa kusambaza maafisa wa usalama wa kutosha wa kudumisha sheria na utangamano.

Katika maeneo mengine, maafisa wa udumishaji usalama hulalamika kuhusu rasilimali chache na duni wanazopewa ili kudumisha usalama na kudhibiti silaha ndogo ndogo. Kwa mfano, katika eneo la kaskazini-mashariki mwa Kenya, ambapo hali ya usalama sio imara, na eneo ambalo linahitaji upigaji doria wa polisi wa dhati wa mara kwa mara, kuna ukosefu


wa magari. Nyakati nyingine polisi wanalazimika kutumia magari pamoja na idara nyingine, jambo linalokwamisha juhudi zao za kupiga doria kikamilifu. Kuweko kwa barabara mbovu pia kunamaanisha kwamba bila magari ya kutosha, doria zinapigwa tu katika maeneo yanayoweza kufikiwa kwa urahisi.[70] Hali ya hewa isiyo ya kawaida, kwa mfano mvua, mara nyingine husababisha maeneo fulani yasifikike, kama Hulugho, eneo lililoko mpakani na lililotajwa mara kadhaa na wahojiwa wa kundi mahususi kuwa eneo ambako silaha ndogo ndogo na bidhaa za ulanguzi huingizwa, na ambapo wanamgambo wa al-Shabaab hupitia.[71]

Baadhi ya wahojiwa walisisitiza kuwa kunahitajika kuwa na juhudi mwafaka za kukusanya silaha na za kuzidhibiti ili kupata suluhisho la kudumu kwa tatizo hili. Huko Kaskazini mwa Bonde la Ufa, hususan katika maeneo ya Samburu na yale yanayopakana nayo ya Pokot katika Bonde la Suguta, maoni ya wahojiwa yalitiliwa mkazo na uhasama uliopo kati ya jamii hizo mbili. Wapokot wameelezewa kuwa wachokozi na wanaopenda kupanua eneo lao, na kwa sababu hii ni kama wamewafukuza wenzao wote. Kwa sababu hii, inapendekezwa kwamba ni sharti kuwe na zoezi la upokonyaji silaha litakalolenga eneo mahususi.[72] Hata hivyo, inafaa ikumbukwe kuwa shughuli za ukusanyaji silaha zilizolenga maeneo fulani fulani zimekuwa sababu za kutofaulu kwa operesheni nyingi kama hizo kaskazini mwa Kenya (Wepundi, Ndung'u, and Rynn, 2011, uk. 10–11).

Juhudi za kudhibiti silaha hazitegemei tu utekelezaji wa sheria zifaazo na mifumo ya sera, bali pia nia njema ya kisiasa. Hata hivyo, Kenya bado haijatekeleza sera ya kitaifa dhidi ya silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi. Pia, Kenya inatakiwa kufanya uhakiki upya na kwa upana wa sera na sheria zinzohusu silaha hizi ili kuziambatanisha kikamilifu na sera za nchi nyingine za eneo hili za udhibiti wa silaha na miongozo ya kanuni bora.

Hususan chini ya RECSA, hati na miongozo husika ni pamoja na Mwafaka wa Nairobi, na Mwongozo wa Kanuni Bora Kuhusu Upunguzaji wa Silaha katika eneo la RECSA (RECSA Best Practice Guidelines), kati ya nyingine.


**Mchoro 3.2** Asilimia ya wahojiwa wanaoona mikakati ya kudhibiti silaha nchini Kenya ni duni au inafaa, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Pia, upo Mpango wa Utekelezaji na viwango vya kimataifa vingine. Hati nyingine ambayo haijatilililiwa sana maanani ni Mwafaka kuhusu Kuzuia, Kupambana na Kuangamiza Wizi wa Mifugo katika eneo la Mashariki mwa Afrika, iliyotiwa sahihi na Kenya, Tanzania, Ethiopia, Sudan, na Uganda. Ikishaanza kufanya kazi, hati hii itazilazimisha nchi hizi zichukue hatua za kieneo ili kuangamiza kabisa wizi wa mifugo.

**Mchoro 3.3** Maoni ya wahojiwa kuhusu kuwa na habari kuhusu angalau mkataba mmoja wa kimataifa kuhusu udhibiti wa silaha, kwa makundi (CSOs na LEAs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Siyo wahojiwa wengi wa LEAs na CSOs walio na habari kuhusu hati hizi. Uchambuzi wa vikundi vyote viwili unadhihirisha kuwa LEAs ndiyo waliokuwa wanaelewa kidogo kuhusu mkataba wa kimataifa au wa kieneo kuliko wahojiwa wa CSOs (angalia Mchoro 3.3). Zaidi ya nusu ya CSOs hawana habari kuhusu kutiwa sahihi kwa mwafaka wowote wa kimataifa, au wa kieneo, unaohusu silaha ndogo ndogo (angalia Mchoro 3.3). Hii inaweza kumaanisha kwamba kwa vile shughuli za CSOs ni pana na hazihusu tu masuala ya amani na usalama, kuna uwezekano kuwa labda wengine wao hawajasikia kuhusu hati na masuala yanayohusu silaha ndogo ndogo. Kutokana na hali hii, ni sharti kuwe na kundi lengwa na pana litakaloshugulikia mipango ya kukuza uwezo dhidi ya silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi na uhamasishaji wake.


## Taratibu za kudhibiti mipaka

Kenya ni eneo maalum kijiografia na kisiasa—ina umuhimu wa kibiashara kwa vile ndio kitovu cha biashara na usafiri kwa nchi nyingi za Afrika mashariki na kati. Kenya pia inawahifadhi wakimbizi kutoka nchi jirani waliotoroka makwao baada ya misukosuko na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe kwa muda wa miaka kadhaa. Yote haya, pamoja na hali ya kuzungukazunguka kwa jamii nyingi ziishizo mipakani, hufanya usalama mipakani kupewe kipaumble ili kusuluhisha swala la ukosefu wa usalama na kupunguza visa vya uhalifu.

Changamoto kuhusu mianya iliyopo mipakani ni swala linalozipa nchi zote eneoni wasiwasi. Ulanguzi wa silaha ndogo ndogo hufanyika kwenye maeneo ya mipakani, jambo ambalo limekuza dhana kwamba silaha hizi huletwa kutoka nchi jirani.

Waliohojiwa waliulizwa kukadiria mafanikio ya taratibu za kudhibiti mpaka wa Kenya: asilimia 65.3 na 79 ya wahojiwa wa LEAs na CSOs, mtawalia, walizikadiria kuwa dhaifu. Ni idadi ndogo tu ya wahojiwa—asilimia 34.4 ya wadumishaji sheria na asilimia 20.5 kutoka CSOs—waliokadiria taratibu hizo kuwa zinafaa.

**Mchoro 3.4** Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa visa fulani vya uhalifu vimekithiri mpakani, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Kiashiria muhimu kinachodhihirisha ukosefu wa usalama ni idadi ya visa vya uhalifu vinavyoteka katika pande mbili za mpaka wowote ule. Wahojiwa walionelea kuwa ulanguzi wa dawa za kulevya, wizi wa magari na tatizo la wahamiaji haramu yamekuwa mambo ya kawaida. Wengi wao walisema kuwa visa vya uwindaji haramu ni vichache sana. Baadhi ya visa hivi ndivyo hutumika ili kulangua silaha.

Changamoto ya kuhakikisha usalama mipakani inafanywa kuwa tata na jamii zinazoishi katika zaidi ya nchi moja, pamoja na tamaduni za kuhamahama za jamii ziishizo mipakani. Kwa mfano, Wasomali Wakenya wana udugu na Wasomali wanaoishi Somalia. Waborana na Wagabra wa Kenya waishio Marsabit wana udugu na Waoromo wa Ethiopia. Wakaramoja nao wanaishi Kenya, Uganda, na Sudan Kusini. Na huko kusini mwa nchi, Kenya na Tanzania zina Wamaasai na Wakuria katika pande zote mbili za mpaka. Huko magharibi, Wasabaot wa Kenya na Wasebei wa Uganda wana udugu. Kati ya jamii za wafugaji wa kuhamahama, kuvuka mipaka hadi nchi nyingine ili kutafuta chakula na lishe kwa mifigo kwao ni jambo la kawaida. Lakini hizi shughuli za mipakani nyakati nyingine hutumika na jamii ili kununua silaha (Farah, Aisha, na Daud, 2005, p. 8).

Wasiwasi kuhusu mianya iliyoko katika mipaka ya Kenya unaathiri maoni kuhusu usalama wa Kenya kuhusiana na swala la silaha ndogo

ndogo. Walipoulizwa kutoa makadirio yao kuhusu usalama nchini Kenya kuhusiana na tatizo hili, asilimia 67.3 ya wahojiwa wa LEAs walihisi kwamba haikuwa salama, ikilinganishwa na asilimia 73.4 ya wahojiwa wa CSOs.

Hivyo basi, ingawaje gharama ya kuwa na mikakati kabambe ya kudhibiti mipaka ni ya juu, mikakati hii ni muhimu ili kupambana na visa vya uhalifu vilivyopangwa, na vinavyofanyika katika nchi kadhaa, ikiwemo ulanguzi wa silaha ndogo ndogo, miongoni mwa uhalifu mwingine. Lakini juhudi zozote zile za kudhibiti mipaka itabidi zikumbane na hali ya watu kujitambulisha kuwa na uraia wa nchi kadhaa. Kwa sababu jamii fulani zina udugu unaovuka mipaka, inamaanisha kwamba vikundi hivi vinauhusiano na wengine kwenye nchi nyingine. Hii ndiyo sababu makundi katika eneo hilo wanakuza juhudi zao za kuimarisha uwezo wao wa kujihami na kufanya mashambulizi dhidi ya kile wanachokiona kuwa tishio.


## Kupunguza changamoto kuhusu silaha haramu

Utafiti huu ulitafuta maoni ya wahojiwa kuhusu hatua kadhaa ambazo zimechukuliwa kushughulikia changamoto za tatizo la silaha ndogo ndogo haramu. Jitihada za kawaida zinajumuisha usalimishaji silaha, kuwahamasisha watu, kukamatwa kwao na kufikishwa mahakamani, na uwezekano wa kuundwa kwa kitengo maalum cha polisi cha kupambana na silaha ndogo ndogo.

### *Usalimishaji silaha*

Asilimia kubwa zaidi ya wahojiwa wa LEAs (asilimia 44.6) kuliko ile ya wahojiwa wa CSO (asilimia 34.5) walikuwa na habari kuhusu juhudi za serikali za usalimishaji silaha. Hii inalinganishwa na asilimia 13 pekee ya wahojiwa wa HH. Hata hivyo, wengi wa waliohojiwa walisema kwamba walikuwa hawana habari kuhusu juhudi zozote katika maeneo yao za kusalimisha silaha (Mchoro 3.5). Hali hii huenda inatokana na ukweli kuwa juhudi za hivi majuzi za upokonyaji silaha (kwa mfano Operesheni Dumisha Amani) zimelenga haswa eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, na kwa kiasi fulani Kanda ya Juu ya Mashariki.

**Mchoro 3.5** Asilimia ya wahojiwa ambao wanafahamu kuhusu kampeni za eneo lao za upokonyaji silaha, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Uthibitishaji wa uchanganuzi wa majibu ya utafiti unadhihirisha mwelekeo wa kuwepo kwa ufahamu zaidi kuhusu operesheni za kusalimisha silaha miongoni mwa wale walioko katika maeneo yenye hatari ya kutokea kwa fujo, ikilinganishwa na wale walioko katika maeneo yenye uathirikaji wa kadiri au wa chini. Kwa kweli, asilimia kubwa zaidi ya LEAs waliokuweko kwenye maeneo yenye uathirikaji wa juu walisema wamesikia kuhusu juhudi kama hizo kuliko CSO na HHs. Pia, asilimia kubwa ya wahojiwa wa CSO walijua kuhusu juhudi za kusalimisha silaha katika maeneo yao kuliko wahojiwa wa HH.

Ugunduzi huu unatilia shaka kiwango cha kuhusika kwa jamii katika juhudi za usalimishaji silaha. Ingawaje utaratibu wa serikali wa usalimishaji silaha na wa maendeleo (hususan Operesheni Dumisha Amani) hutumia vyombo vyote vya habari, mashirika ya kutetea haki za jamii, na uhusishaji wa jamii, inaonekana kuwa kiwango cha kushiriki kwa jamii mashinani si cha kuridhisha. Mengi zaidi yanapaswa kufanywa ili kushughulikia upungufu ulioko kuhusu ufahamu wa mikakati ya kudhibiti silaha miongoni mwa LEAs, CSOs, na HHs.

Ni sharti isisitizwe kuwa kukusanywa tu kwa silaha hakufai kuwa nia tu ya mikakati ya usalimishaji. Badala yake, kunafaa kuwe na faida

zinazoambatana na kupunguzwa kwa ugavi unaokuza ongezeko la silaha—zikiwemo kuimarishwa kwa usalama katika maeneo husika, miongoni mwa nyinginezo. Kwa hilo, kulikuwa na hisia tofauti kuhusu athari za usalimishaji silaha kwa usalama, huku wengi wa wahojiwa wa HH (asilimia 54.7) wakisema kuwa usalama ulikuwa umeimarika baada ya usalimishaji; asilimia 19.1 wakionelea kuwa changamoto za usalama hazijabadilika kamwe, huku asilimia 26.2 wakionelea kuwa hali ya usalama ilikuwa imezorota (Jedwali 3.1). Hata hivyo, wahojiwa katika FGD waliunga mkono mikakati kabambe ya usalimishaji silaha.[73]

**Jedwali 3.1** Athari za usalimishaji silaha kwa usalama wa wakaazi

| Athari | % ya watu |
|---|---|
| Zilipungua | 26.2 |
| Zilikuwa thabiti | 19.1 |
| Ziliongezeka | 54.7 |
| Jumla | 100.0 |

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)


Ukizingatia ukweli kwamba takriban theluthi moja ya wahojiwa walihisi kuwa ukosefu wa usalama ulizidi kuzorota baada ya usalimishaji silaha, inaeleweka kwamba viwango vya ushirikiano wa jamii wakati wa shughuli za usalimishaji silaha vilitofautiana baina ya makundi hojiwa. Kati ya waliokuwa na habari kuhusu usalimishaji silaha, asilimia 61.3 ya wahojiwa wa LEAs na asilimia 68.3 ya wahojiwa wa CSO waliashiria kuwa jamii zilijiunga na shughuli hizo (Mchoro 3.6).

Aina ya pili ya hisia inahusika na nyakati ambapo jamii zilisalimisha baadhi tu na wala siyo silaha zao zote: asilimia 65.0 ya wahojiwa wa CSO na asilimia 49.3 ya LEAs walithibitisha haya. Hata hivyo, kuna ongezeko la kiwango cha ufahamu kuhusu hatari za umilikaji silaha haramu na utumizi wake, kulingana na maoni ya asilimia 36.7 ya LEAs na asilimia 21.7 ya wahojiwa wa CSO (Mchoro 3.6).

Wale wanaohusika na mazoezi ya kusalimisha silaha huwa mara nyingi ni viongozi wa jamii na wanachama wa mashirika ya kutetea haki za raia wanaofanya kazi kwa ushirikiano na utawala wa mkoa ili kuwashawishi na

kuwatambua walio na silaha. Nyakati zote Idara ya Polisi Kenya na maafisa wa Utawala wanahusishwa, ila tu katika maeneo ambamo changamoto za usalama zimekuwa na vipengee vingi vyenye utata. Palipo na vikundi vyenye silaha, kama SLDF wa Mt Elgon, basi jeshi huingilia kati. Wakati mwingi, Jeshi la Kenya linatumwa katika maeneo husika ili kuyazingira, huku polisi na utawala wa mkoa wakiyaingia. Mara nyingi, kadri ukubwa wa operesheni ya kusalimisha silaha ilivyo, ndivyo idadi ya vitengo vya usalama vinavyohusishwa, hii ikiwa ni pamoja na wanajeshi. Shirika la Utunzaji Misitu nchini Kenya (KFS) na Shirika la Huduma kwa Wanyama Pori nchini Kenya (KWS) pia huwa yanahusishwa, na mara kwa mara hupata silaha na kuzisalimisha kwa polisi (KNFP, 2006, uk. 34).[74]


**Mchoro 3.6** Asilimia ya wahojiwa waliokubaliana na taarifa fulani kuhusu matokeo ya kampeni za mashinani za usalimishaji silaha, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Kumekuwa na madai ya mara kwa mara kwamba maafisa wa udumishaji sheria hukodisha bunduki zao na pia huuza risasi. Tatizo hili, kwa kiasi fulani, linakuzwa na kutowekwa ipasavyo kwa kumbukumbu za maghala au milundiko ya silaha za serikali. Uhifadhi wa kumbukumbu hizi kwenye mitambo ya kompyuta ni juhudi ya hivi majuzi, na siyo kila kituo cha polisi chenye uwezo huu.

**Mchoro 3.7** Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa serikali huweka kumbukumbu zifaazo za silaha zake, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Walipoulizwa kusema iwapo waliamini kuwa serikali huweka kumbukumbu zifaazo za maghala ya silaha zake, asilimia 83.3 ya LEAs walisema waliziamini kumbukumbu hizo, lakini idadi ya kutiliwa maanani, ya asilimia 11.6, hawakuamini, huku asilimia 5.1 wakiwa hawana uhakika. Hii ilitofautiana na asilimia 35.3 ya wahojiwa wa CSO walioamini kuwa serikali haiweki kumbukumbu inavyostahili (Mchoro 3.7).

Serikali ya Kenya imeanzisha mpango wa kuzitia alama silaha na risasi zake zote ili kuhakikisha usimamizi bora wa maghala ya silaha. Hatua hii inatarajiwa kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya bunduki za serikali (KNFP, 2011, uk. 1–2).

Baadhi ya silaha haramu zinazotumiwa visivyo ni zile wanazopewa KPRs. Kwa hivyo, kuna wasiwasi kuhusu uwajibikaji na utendakazi wa KPRs katika usimamizi wa silaha na risasi. Wapo KPRs ambao inadaiwa wanatumia silaha zao kutenda uhalifu, au wanazikodisha kwa wanaofanya ujambazi au kwa wanaovamia jamii jirani. Kwa mfano, tetesi za aina hiyo zilitanda huko Marsabit.[75]

Si dhahiri iwapo kweli silaha za KPRs hurudishiwa serikali. Kwa ujumla inaeleweka kwamba msemo 'KPRs hawafi' humaanisha kuwa hakuna kumbukumbu zozote zinazowekwa, hata za wanaokufa, na silaha zao hazirudishiwi serikali. Baadhi ya silaha hizo hurithiwa au huchukuliwa

na jamii, jambo linalozua swali linalohoji ikiwa usimamizi na udhibiti wa silaha zinazopewa KPRs kwa sasa ni thabiti.[76]

Usimamizi mbaya wa KPRs huzua utendakazi mbaya na ukiukaji wa majukumu yao. Taasisi ya KPR pia yaonekana kana kwamba imeingiliwa kisiasa, na kwa sababu hii kanuni na taratibu za kuwaandika kazi hazizingatiwi. Ingawaje KPRs wanatakiwa kufanya kazi kama polisi wowote wale wa kawaida chini ya afisa anayesimamia kituo, na wanatakiwa kuwa na vitendakazi au vifaa vya kufanyia kazi, usimamizi, mafunzo na motisha ili wafanye kazi kwenye eneo la jamii fulani, taratibu hizi za utendakazi zimepuuzwa kwa kiasi kikubwa.[77]

Hata hivyo, katika maeneo kama ya Samburu na Turkana, KPRs wanathaminiwa. Baadhi ya wahojiwa walisema wale polisi wa kawaida wachache waliopo hawawatoshelezi ili kudhibiti usalama. Lakini, ili kubainisha jinsi siasa zinavyozingira KPRs, ingawaje Wasamburu wana KPRs, jirani zao Wapokot hawana. Hii inawekea mkazo wazo kwamba KPRs wana upendeleo, ukabila na wameingiliwa na kuathirika kisiasa.[78]

## *Kukuza ufahamu kuhusu silaha ndogo ndogo*


Wahojiwa waliulizwa iwapo walikuwa wameona juhudi zozote za kukuza uhamasishaji na ufahamu kuhusu masuala yanayohusu silaha ndogo ndogo; asilimia 60.5 ya wahojiwa wa CSO na asilimia 40.5 ya LEAs, mtawalia, walisema walikuwa hawajahudhuria wala kuhusishwa au kuona juhudi zozote za kuimarisha uhamasishaji (angalia Mchoro 3.8).

Kumekuwepo na baadhi ya juhudi za kuimarisha uhamasishaji zilizofanywa na utawala wa mikoa, KNFP, na wahusika wa mashirika ya kutetea haki za jamii (hususan chini ya Mtandao wa Utekelezaji Nchini Kenya Kuhusu Silaha Ndogo Ndogo) ili kuendeleza elimu kuhusu masuala ya silaha ndogo ndogo na nyepesi. Baadhi ya njia za mawasiliano na za kukuza ufahamu wa masuala haya zilizotajwa kutumika mara nyingi zaidi ni mabaraza ya machifu na warsha (angalia Mchoro 3.9). Hizi zilisemekana kuwa zinazofaa (angalia Mchoro 3.10). Mabaraza ya machifu yaliorodheshwa kuwa yanayofaa zaidi na wahojiwa wa LEAs pamoja na wale wa CSO (asilimia 96.1 na asilimia 94.4, mtawalia). Warsha ziliorodheshwa za pili

kama njia muafaka ya kuelimisha watu. Filamu zenye kuonyesha hali halisi ya mambo, vijitabu na magazeti ziliorodheshwa kuwa zenye msukumo wa chini.


Wahojiwa waliulizwa wataje wazi ni vikundi vipi ambavyo vyaweza kuchukuliwa kuwa vya maana zaidi kuwa walengwa wa kampeni dhidi ya silaha ndogo ndogo. Vijana, na makundi ya wahalifu ndiyo yaliyopewa kipaumbele, yakifuatwa na CSOs—ambayo yanaweza kusambaza habari kupita njia mbalimbali—wazee-viongozi na *wamorani*. Vikundi vilivyotajwa hapo juu vinafikiriwa kuwa waenezaji wakuu wa visa vya uhalifu na vurugu zinazohusu bunduki, na kulengwa kwao ni sehemu ya mkakati muhimu wa kutatua tatizo la silaha.

**Mchoro 3.8** Asilimia ya wahojiwa ambao wamehudhuria/kuhusishwa/kuona matangazo yoyote ya kuimarisha uhamasishaji kuhusu silaha ndogo ndogo kwa makundi (LEAs na CSOs)





**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 3.9** Asilimia ya wahojiwa waliotaja njia mbalimbali za uhamasishaji, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 3.10** Asilimia ya wahojiwa ambao waliorodhesha baadhi ya njia za uhamasishaji kuhusu silaha ndogo ndogo na nyepesi kuwa zinafaa, kwa makundi (CSOs na LEAs)




* Maonyesho ya wasanii wanaozungukazunguka barabarani
** Mabango makubwa yanayoezekwa kandoni mwa barabara
*** Vipindi vya televisheni vinavyoonyesha hali halisi ya mambo

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Hata hivyo, katika baadhi ya FGDs—hususan katika jamii za wafugaji wa kuhamahama[79]—washiriki walitoa maoni kwamba inafaa watoto wafunzwe kuhusu hatari za silaha ndogo ndogo ili waweze kuwashawishi wenzao katika jamii. Wahojiwa walionelea kwamba kuonyeshwa njia tofauti za kujikimu maishani kupitia kujumuika na jamii nyingine katika mazingira rasmi, kama mashule, kungekuwa jambo la maana. Utaratibu wa masomo shuleni kuhusu uimarishaji amani na hatari za silaha ndogo ndogo ungefaa kuafikia lengo hili.


## *Kukamatwa na kufikishwa mahakamani*

Kufikishwa mahakamani na kukamilishwa kwa kesi zinazohusu uhalifu uliohusisha silaha ndogo ndogo na ghasia, ni kiini cha kutatua hali ya kutohofia kuadhabiwa kwa kumiliki silaha haramu. Mshiriki mmoja wa FGD alitoa mfano wa tamaduni iliyokita mizizi Lokichoggio ya kumiliki silaha: 'Katika baraza fulani la chifu lililohudhuriwa na DC [mkuu wa wilaya], wana jamii kadha walikuja wamebeba bunduki zao, huku wakimuashiria DC kwamba walichokuwa wanahitaji ni risasi kwa ajili ya bunduki zao, na siyo hayo maswala ya usalama na maendeleo aliyokuwa anayazungumzia.'[80]

Rasimu ya Sera ya Kitaifa kuhusu SALW iliyotayarishwa na KNFP inatoa nafasi kwa umiliki wa bunduki kuchukuliwa kama tendo la uhalifu. Kifungu 4(3) cha sheria kuhusu bunduki kina vipengee ambavyo vinatoa adhabu ya kati ya kifungo cha kati ya miaka 7 na 15 kwa kosa la kupatikana na bunduki na/au risasi haramu (Kenya, 1954). Lakini ingawaje kuna sheria za kuadhibu umilikaji silaha haramu, kufikishwa mahakamani kwa kesi zinazohusu silaha wakati mwingine hutatizwa na uchunguzi duni unaosababisha kushindwa kwa kesi hizo kuhukumiwa.

Wengi wa waliokuwa na imani na uwezo wa serikali kushtaki visa vya uhalifu vilivyohusisha silaha walitoka maeneo yenye kukumbwa na fujo, wakiwa asilimia 28.7 ya wahojiwa wa HH, asilimia 32.8 ya LEAs, na asilimia 29.2 ya wahojiwa wa CSO (Mchoro 3.11). Matokeo yalionyesha kwamba wahojiwa wa CSO kutoka maeneo yanayoathirika kwa viwango vya wastani na vya chini ndio waliokuwa hawakubaliani sana na maoni haya. Ikitiliwa maanani kwamba mahakama nyingi ziko katika maeneo yenye uathirikaji wa viwango vya wastani na vya chini vya kukumbwa na fujo, hali yao ya kutokuwa na imani na uwezo wa kushtaki— jukumu mojawapo la jadi la polisi—inaashiria haja ya kuimarishwa kwa kesi zinazowasilishwa mahakamani. Hii inaweza tu kuafikiwa kwa kufanya uchunguzi kabambe na wa kina, ufahamu wa sheria zinazohusika, na kuwa na ujuzi wa kutayarisha kesi thabiti.

**Mchoro 3.11** Asilimia ya wahojiwa wanaoashiria kwamba uhalifu unaohusisha silaha unashtakiwa ipasavyo, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Hata hivyo, ni muhimu kusisitiza kwamba wahojiwa wengi zaidi wa CSO na LEAs katika maeneo yenye fujo walikuwa na imani haba kuhusu mashtaka—wakiamini kuwa kuna ukosefu wa ujuzi kuhusu suala hili. Kwa kweli, asilimia 56.8 ya wahusika wa CSO kutoka maeneo yenye kuathirika kwa kiwango cha chini walikubaliana na kauli hii.


Sehemu kubwa ya wahojiwa wa HH kuliko wahojiwa wa LEAs na CSO walikubali kwamba kuna haja ya kuwepo kwa uwekezaji zaidi wa rasilimali ili kuimarisha utendakazi na uwezo wa uendeshaji mashtaka. Kufaulu kwa uendeshaji mashtaka unaohusu kesi za silaha ndogo ndogo ni kutilia nguvu ufumbuzi kuhusu masuala ya ukiukaji haki kwa kutumia mtutu wa bunduki. Hatua za kuadhibu zinazothibitika dhidi ya wahalifu wenye kesi zinazazohusu silaha ndogo ndogo ni hatua muhimu sana katika kupunguza haja ya kutaka kumiliki silaha. Ni sharti basi rasilimali zinazotosha na zenye uwezo kamili ziwepo ili kuhakikisha kufaulu kwa kesi hizi. Kwa wastani, asilimia 44.9 ya wahojiwa wa CSO, asilimia 36.1 ya wahojiwa wa HH, na asilimia 25.1 ya wadumishaji sheria waliohojiwa walidhani kuwa utendakazi wa uendeshaji mashtaka ya kesi zinazohusu silaha ndogo ndogo ulikuwa wa kima cha chini.

Asilimia nyingine 21.2 ya LEAs, asilimia 8.1 ya wahojiwa wa HH, na asilimia 13.1 ya wahojiwa wa CSO walitaja ukosefu wa rasilimali kama sababu ya kutofaulu kwa kesi zinazohusu silaha ndogo ndogo (angalia Mchoro 3.12). Hata hivyo, katika kaunti zenye uathirikaji wa kiwango cha chini, maoni yaya haya hutoka kwa wahojiwa kutoka makundi yote matatu. Mbali na hayo, kwa sababu ni wazi kwamba baadhi ya maafisa wa usalama/polisi wanashukiwa kushirikiana na makundi ya kihalifu, inamaanisha kwamba umma hauna imani na utendakazi wa mashirika ya udumishaji sheria.[81]

Hatimaye, sehemu kubwa ya wahojiwa kutoka maeneo yenye uathirikiaji wa kadiri kuliko wale kutoka maeneo yenye viwango vya juu na vya chini vya kutokea kwa fujo walionelea kuwa katika maeneo yao kesi zilizohusu silaha ndogo ndogo zilikuwa hazifikishwi mahakamani (Mchoro 3.13). Maeneo yenye viwango vya wastani vya uathirikaji ndiyo yaliyokuwa na uwezekano zaidi wa kutumika kwa silaha butu na zenye bapa kama visu na mapanga, kwa mfano vurugu na visa vya ukatili vinavyofanywa


na Mungiki katika eneo la kati mwa Kenya.[82] Kuwepo kwa fikra kuwa ni mashtaka machache sana ya kesi zinazohusisha bunduki yanayofikishwa mahakamani katika maeneo yenye uathirikaji wa wastani kuliko maeneo yenye uathirikaji wa chini labda kunathibitisha ni kwa nini wilaya kama ya Mt Elgon katika kaunti ya Bungoma inachangia tatizo hili la kuzidi kwa idadi za bunduki, na kesi zinazozihusu.

**Mchoro 3.12** Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa tatizo linalohusu uendeshaji mashtaka wa visa vya uhalifu vinavyohusu silaha yanatokana na ukosefu wa rasilimali na siyo utendakazi, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 3.13** Asilimia ya wahojiwa waliosema kwamba kesi zinazohusu silaha ndogo ndogo katika maeneo yao hazifikishwi mahakamani, kwa uathirikaji wa kaunti na kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Walipoulizwa kama walikuwa na habari yoyote iwapo kulikuwa na yeyote aliyekamatwa kwa sababu za silaha haramu, asilimia 34.4 ya LEAs na

asilimia 43.8 ya wahojiwa wa CSO walisema walikuwa wamesikia kuhusu waliokamatwa. Lakini asilimia 63.8 ya LEAs na asilimia 54 ya wahojiwa wa CSO walikuwa hawana habari kuhusu visa kama hivyo vya kukamatwa.

Kuhusu utekelezaji haki, wahojiwa waliulizwa kama walijua kuhusu hukumu zozote zilizofanywa mwaka uliotangulia zilizohusu kesi za silaha ndogo ndogo. Kati ya LEAs, asilimia 80.7 hawakuwa na habari zozote kuhusu hukumu kama hizo, ikilinganishwa na asilimia 19.3 waliokuwa nazo. Wengi wa wahojiwa wa LEAs na CSO walionelea kuwa uwezo wa mahakama wa kushtaki kesi zinazohusu silaha ndogo ndogo ulikuwa chini ya kiwango cha wastani au wastani: asilimia 18.8 ya LEAs na asilimia 35.1 ya wahojiwa wa CSO walionelea uwezo huo kuwa chini ya wastani, huku asilimia 65.7 ya LEAs na asilimia 51.7 ya wahojiwa wa CSO wakishikilia maoni kwamba kuna uwezo wa kisheria wa wastani wa kufanya mashtaka.

**Jedwali 3.2** Kesi zinazohusu utumiaji wa bunduki/risasi na wahalifu katika mwaka mmoja na matokeo ya kesi hizo (2010/11)

| Mkoa | Bunduki ndefu | Bastola | Jumla* | Idadi ya visa vya kukamatwa | Idadi ya hukumu | Idadi ya walioachiliwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Eneo la Nairobi | 22 | 135 | 157 (666) | 10 | 3 | 0 |
| Bonde la Ufa | 66 | 43 | 109 (712) | 65 | 24 | 0 |
| Kati | 38 | 51 | 89 (320) | 6 | 2 | 1 |
| Mashariki | 46 | 19 | 65 (4,139) | 50 | 6 | 1 |
| Kaskazini Mashariki | 32 | 0 | 32 (3,396) | 29 | 9 | 0 |
| Pwani | 11 | 17 | 28 (18) | 24 | 7 | 0 |
| Nyanza | 7 | 3 | 10 (99) | 4 | 1 | 0 |
| Magharibi | 9 | 7 | 16 | 7 | 2 | 1 |
| **Jumla kuu** | **231** | **275** | **506 (9,350)** | **195** | **54** | **3** |

* Tarakimu zilizopo ndani ya mabano zinaashiria risasi zilizotwaliwa.

**Duru:** Mahojiano ya Small Arms Survey katika makao makuu ya Idara ya Upelelezi wa Jinai (CID), Nairobi, 23 Agosti 2011; yametumiwa kwa ruhusa


Jedwali 3.2 inaonyesha takwimu za kipindi cha 2010/11 kimkoa ambapo watu 195 walikamatwa, 57 walifikishwa mbele ya mahakama, ambapo hatimaye

54 kati yao walihukumiwa na watatu kuachiliwa. Visa hivi vya uhalifu vilihusu utumizi wa silaha 516 na risasi 9,350 za aina mbalimbali. Visa ambavyo havikufikishwa mbele ya mahakama vingali vinachunguzwa. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba eneo la Bonde la Ufa ndilo lililotoa hukumu nyingi katika kesi zilizohusu bunduki, huku Nyanza ikiwa na chache zaidi, Magharibi na Kati zilikuwa katika nafasi moja, ya pili kutoka chini. Kaskazini Mashariki, Pwani, na Mashariki ndizo zilizokuwa katika nafasi ya pili, kulingana na wingi wa kesi zilizohukumiwa. Hii, kwa ujumla, inadhihirisha fikira kuhusu uendeshaji mashtaka, huku maeneo yenye kiwango cha juu cha uathirikaji yakiwa na mashtaka mengi zaidi.

## *Kitengo maalum cha polisi*

Wahojiwa waliulizwa ikiwa kuundwa kwa kitengo maalum cha polisi kungeboresha juhudi za kupunguza silaha haramu (Mchoro 3.14). Jumla ya asilimia 74.6 ya LEAs na asilimia 82.4 ya wahojiwa wa CSO waliunga mkono maoni haya, ilhali asilimia 23.9 na asilimia 17 mtawalia, hawakuunga mkono.

**Mchoro 3.14** Asilimia ya wahojiwa waliosema kuwa kuna haja ya kuwepo kwa kitengo maalum cha polisi cha silaha ndogo ndogo, kwa makundi (LEAs na CSOs)





**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Aidha, utafiti huo ulitaka kupima maoni kuhusu uboreshaji wa masuala ya mafunzo kwa polisi ya kudhibiti silaha: asilimia 88 ya LEAs na asilimia 82.4 ya wahojiwa wa CSO waliunga mkono hoja hii. Mbali na kuweko kwa

mafunzo yanayoendeshwa na KNFP ya kukuza ufahamu katika Taasisi ya Utawala ya Kenya (KIA) na katika Chuo cha Mafunzo kwa Polisi wa Utawala cha Embakasi, kuna haja ya kuwepo kwa mafunzo maalumu zaidi kuhusu mikakati ya udhibiti wa mipaka, usimamizi wa maghala ya silaha, mbinu bora za usalimishaji silaha, na hati rasmi za kimataifa na kitaifa za kudhibiti silaha, pamoja na nyinginezo. Mikakati kama hii inafaa kulenga mashirika yote ya udumishaji sheria, hata kupitia taasisi kama Chuo cha Polisi cha Kenya, Chuo cha Mafunzo cha CID, Police Academy, na Vyuo vya Polisi wa Utawala.

**Mchoro 3.15** Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kuwa kuna uhusiano mzuri kati ya mashirika ya kudumisha sheria na jamii, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Lakini, kushindwa kwa wadumishaji sheria katika harakati za kudhibiti silaha kunaweza kulaumiwa kwa kiasi fulani kwa kukosa kwao kufanya kazi pamoja na jamii. Ingawaje asilimia 76.5 ya LEAs walidhani kuwa kiwango cha ushirikiano kati ya polisi na jamii kilikuwa kizuri, idadi ndogo zaidi ya wahojiwa wa CSO (asilimia 58.2) walikubaliana na maoni haya (Mchoro 3.15). Hata hivyo, utawala wa mikoa ndiyo umepewa alama za juu zaidi kwa uhusianio wao na jamii: asilimia 89.8 ya LEAs na asilimia 85.8 ya wahojiwa wa CSO walionelea kuwa maafisa wa utawala walikuwa na ushirikiano mzuri na jamii.

## *Mfumo wa kutoa tahadhari ya mapema*

Mfumo wa kutoa tahadhari ya mapema unategemea kuwepo kwa uhusiano wa karibu na thabiti kati ya wahusika wote; utaratibu mzuri wa mawasiliano na maoni rejea; na cha muhimu zaidi, uwezo wa kuwepo kwa mfumo kabambe wa kuweza kukabiliana na hali zozote zile. Kwa bahati mbaya, wahojiwa wengi walilalamikia kushindwa kwa mashirika ya kudumisha sheria kuchukua hatua au kufuatilia habari wanazopewa. Madokezo ya tahadhari kuhusu uvamizi au uhalifu uliokuwa umepangwa nyakati nyingine hupuuzwa.[83] Hata hivyo, nyakati nyingine, tahadhari hutolewa, lakini serikali inakuwa haina vifaa au ala za kutosha ili kukinga au kuzuia visa hivi. Wakati mwingine, serikali huchukua hatua baada ya kisa kutendeka, badala ya kuchukua hatua za kuzuia kutendeka kwa kisa chenyewe.[84]

Kulingana na maoni ya wahojiwa, ni sharti mfumo uliopo wa kutoa tahadhari uimarishwe. Kwa mfano, NSC na KNFP zinaweza kuwa na mpango wa pamoja katika programu ya NSC ya kitaifa ya kuota tahadhari ya mapena. Katika mpango kama huu, KNFP inaweza kuleta ujuzi wake kuhusu masuala ya silaha ndogo ndogo na nyepesi, huku ikibidi wasimamizi wapewe mafunzo yanayostahili. Itakuwa jambo zuri kuweko kwa mfumo usiokuwa na hitilafu ambao hautatatanisha au kutia hatarini usalama wa wasimamizi, wadumishaji sheria, au mhusika yeyote yule. Lakini itabidi kuwe na juhudi za kukuza imani, ili kuhimiza umma kujitokeza zaidi na habari za tahadhari ya mapema.

Walipoulizwa kukadiria namna umma unafaa kuhusishwa ili kutoa taarifa kuhusu bunduki kwa serikali au mashirika ya udumishaji sheria, walisema utumizi wa simu ndio uliofaa (Mchoro 3.16). Kutumwa kwa ujumbe mfupi kupita simu za mkono (SMSs), kuweko kwa wasimamizi wa kukusanya na kusambaza habari, na kutumika kwa DTFs pia kuliorodheshwa kwa kiwango cha juu miongoni mwa njia zinazopendelewa. Barua pepe ndiyo njia isiyofaa zaidi kutokana na uhaba wa mtandao wa Internet, hususan katika maeneo ya mashambani.

## Changamoto zinazokabiliwa katika kupambana na silaha haramu


Uchunguzi ulitafuta kubaini maoni ya wahojiwa kuhusu changamoto kadha wa kadha zinazokumba mashirika ya udumishaji sheria katika kushughulikia masuala ya silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi. Wahojiwa wa CSO pamoja na LEAs walikuwa na maoni sawia kuhusu masuala mengi.

LEAs na wahojiwa wa CSO walionelea kuwa idadi ndogo ya maafisa wa polisi, uhaba wa rasilimali, ukosefu wa motisha, na ufisadi kuwa ndizo changamoto kubwa zaidi. Pia zipo changamoto zinazohusu ukosefu wa ushirikishi kati ya mashirika ya udumishaji sheria; uzoefu wa kazi wa kima cha chini miongoni mwa maafisa, wengine wao ambao hawajapata mafunzo kamili; na uchache wa mahakama na vituo vya polisi (angalia Mchoro 3.17).

Wahojiwa wa FGDs na mahojiano walithibitsha maoni hayo. Changamoto iliyorudiwarudiwa na wengi ilikuwa ya ukosefu wa maafisa wa kutosha wa kudhibiti usalama. Miundomsingi duni inachangia kushindwa kupambana na wizi wa mifugo na ujambazi. Kwa mfano, yapo maeneo katika Bonde la Suguta lililopo kati ya Wasamburu na Wapokot, ambako barabara hazipitiki. Hali ya ardhi, yenye milima na vilima, hufanya kazi ya maafisa wa usalama ya kupambana na wizi wa mifugo na kusambaa kwa silaha ndogo ndogo haramu kuwa ngumu. Eneo hilo linaweza kufikiwa tu kwa mguu, ikimaanisha kwamba pindi tu wezi wa mifugo wanapoongoza mifugo iingie bondeni, maafisa-usalama hushindwa kuwafuata. Jambo hili linazua wasiwasi zaidi kwa sababu awali, maafisa-usalama fulani wameshawahi kupoteza maisha yao katika operesheni za kiusalama katika eneo hili.[85]

Ueneaji wa silaha ndogo ndogo kwenye eneo hili dogo wenyewe ni changamoto. Kutokana na uadui baina ya makabila tofauti miongoni mwa jamii za kaskazini mwa Kenya na nchi jirani (Ethiopia, Somalia, Sudan Kusini, na Uganda), kuhitajika kwa silaha ndogo ndogo ni jambo linaloendelea kukua. Hivyo basi, silaha zinachukuliwa kama ala au vifaa muhimu vya kuhakikisha usalama. Katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, Wapokot na Waturkana wanakabiliwa na uwezekano wa kuathiriwa na mashambulizi kutoka kwa wapiganaji wenye silaha Watoposa na Wamerille kutoka Sudan Kusini na Ethiopia, mtawalia. Katika eneo la kaskazini mashariki, jamii

**Mchoro 3.16** Asilimia ya wahojiwa wanaoonelea kwamba njia kadhaa za mawasiliano kuwa zinazofaa, kwa makundi (LEAs na CSOs)





* Wasimamizi Maalumu wa kukusanya na kusambaza habari.

** Jopo kazi la wilaya kwa ukusanyaji/usambazaji habari.

**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

**Mchoro 3.17** Asilimia ya wahojiwa wanaoonelea kwamba changamoto zinazokumba mashirika ya kudumisha sheria ni za muhimu, kwa makundi (LEAs na CSOs)





**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

ya Wasomali wa Kenya haijaepushwa na athari za mapigano ya makundi mbalimbali nchini Somalia.[86]

## Fikra za umma kuhusu mafanikio ya juhudi za kudhibiti silaha ndogo ndogo

Wahojiwa waliulizwa kukadiria iwapo serikali ilikuwa inashinda vita dhidi ya kuongezeka kwa silaha ndogo ndogo haramu. LEAs wengi walikuwa na maoni kwamba serikali kweli ilikuwa inashinda, huku asilimia 59.6 yao wakisema hivyo. Lakini idadi ya wahojiwa wa CSO ilikuwa ya chini zaidi, na ni asilimia 30.6 walioamini kwamba serikali ilikuwa inashinda (Mchoro 3.18). Kwa kweli, inafaa mengi zaidi yafanywe ili kushinda vita dhidi ya kusambaa kwa silaha ndogo ndogo haramu, ikitiliwa maanani uzito wa changamoto zinazohitaji kukabiliwa.

**Mchoro 3.18** Asilimia ya wahojiwa wanaoamini kwamba Kenya inafaulu katika juhudi zake za kudhibiti silaha ndogo ndogo haramu, kwa makundi (LEAs na CSOs)




**Duru:** KNFP na Small Arms Survey (2011)

Tofauti zilizopo kati ya makundi ya wahojiwa katika Mchoro 3.18 inadhihirisha umuhimu wa kuwahusisha washikadau kadha wa kadha ili kutathmini zinavyoenda juhudi za kudhibiti silaha ndogo ndogo. Kwa kweli, ingawa LEAs wanahisi kuwa juhudi zao zinaendeleza, kwa kiwango

kikubwa, hali hii kuhusu bunduki, wengi wa wawakilishi wa CSOs (takriban theluthi mbili) hawakuamini kwamba serikali inashinda vita hivi. Hii inaonyesha kwamba kwa maoni ya mashirika ya kutetea haki za jamii, inabidi serikali ijizatiti zaidi ili kupunguza uhalifu na vurugu, kuimarisha usalama, na kubana kuenea kwa idadi ya silaha.

# IV. Maamuzi na Mapendekezo

## Maamuzi

Miaka minane baada ya zoezi la mwaka 2003 la kuratibu silaha, uchunguzi huu umezua tathmini ya kwanza ya kina ya ueneaji wa silaha ndogo ndogo na hisia kuhusu usalama nchini Kenya. Matokeo muhimu ya uchunguzi huu ndiyo yafuatayo:

- Ingawaje uchunguzi wa 2003 uligundua kuwa kwa wastani asilimia 6 ya wahojiwa wa HH walikuwa wanamiliki bunduki, uchunguzi huu uligundua kwamba ni asilimia 2.7 pekee ya wahojiwa wa HH—kiwango kidogo zaidi—waliosema wana angalau bunduki moja haramu, jambo linalomaanisha kwamba, kwa kiwango cha chini, kuna takriban silaha haramu 210,000 katika mikono ya raia kote nchini. Sababu za kushuka kwa idadi hii ni kadhaa. Mwanzo, inaweza kuwa ni kwa sababu ya kufaulu kwa mikakati ya serikali na mashirika ya kutetea haki za jamii ya kupunguza silaha.[87] Pili, inawezekana kwamba kwa kutilia maanani operesheni kadhaa kubwa za upokonyaji silaha tangu 2003 hadi sasa, na ambazo mara nyingi zilishurutisha watu wasalimishe silaha katika maeneo fulani, jambo hili liliwafanya wahojiwa wasitake sana kukiri kuwa walikuwa wanamiliki bunduki, kwa kuhofia kujishitaki. Kuna uwezekano kuwa idadi ya silaha zilizoripotiwa ni ya chini kuliko hali halisi, na jambo hili linafaa kutiliwa maanani. Kwa sababu hii, majibu ya maswali kuhusu fikra za kuenea kwa bunduki zilizotolewa na vikundi vyote (HHs, LEAs, na CSOs), zilitumika ili kuzalisha makadirio ya 'juu' yalioyoonyesha kuwa idadi ya HHs wanaomiliki bunduki inaweza kuwa zaidi ya milioni 1.1. Kwa vile ripoti za kibinafsi zinaweza kutoa makisio ya chini, na za hisia kutoa makadirio ya juu kuhusu idadi hizi, ukweli wa idadi kamili unaweza kuwa hapo katikati. Matokeo yanadokeza kwamba kama makisio ya tahadhari kutoka kwa uchunguzi huu yakitumika kote nchini Kenya, basi idadi ya bunduki inaweza kuwa takriban 680,000.

- Uchunguzi ulitambua mienendo mipya kuhusu silaha. Ingawaje viwango vya idadi ya silaha kote nchini vilishuka, maeneo fulani yalirekodi ongezeko kubwa la idadi ya silaha tangu mwaka 2003. Kiwango cha kuenea kwa silaha mkoani Magharibi kilipanda kutoka asilimia 4 hadi idadi ya sasa ya asilimia 10.4. Hali kadhalika, kiwango cha umiliki silaha katika eneo la Bonde la Ufa kiliongezeka kwa kiasi cha asilimia 6.8. Matokeo haya yanasisitiza haja ya kuchunguza upya kama mitazamo ya serikali kuhusu usalimishaji silaha kweli unafaa. Ingawaje Operesheni Okoa Maisha iliyofanywa Mt Elgon iliweza kufaulu kulivunja kundi la wanamgambo wa SLDF, kuimarisha usalama na kuweza kuchukua silaha kutoka kwao, maoni yanayoendelea kuwepo kwamba bunduki zingali zinapatikana yanafaa yazue maswali magumu. Vivyo hivyo, hali sawa na hiyo inaweza kusemwa kuhusu Operesheni Dumisha Amani, ambayo imelenga zaidi eneo la Bonde la Ufa.
- Kaya nyingi huhisi ukosefu wa usalama mkubwa nyakati za uchaguzi. Vurugu za uchaguzi wa Desemba 2007 zimeiachia umma alama. Zaidi ya asilimia 40 ya wahojiwa wa HH walionelea kwamba kuna uwezekano kuwa wanaweza kuwa waathiriwa wa visa vya vurugu au uhalifu katika mwaka utakaofuata.
- Kuna tofauti kati ya maoni ya wahojiwa wa LEAs na CSO kuhusu kufaa kwa juhudi za sasa za kupunguza kukua kwa idadi ya bunduki, na kuzorota kwa usalama. LEAs walikuwa na matumaini mema zaidi kuliko CSOs.

Kufaulu kwa juhudi za kudhibiti silaha na za kudumisha usalama kunaashiria umuhimu wa mikikati ya majadiliano inayoanzia mashinani, na ambayo inahusisha washikadau mbalimbali. Eneo la kaskazini-mashariki, ambapo historia yake ya utovu wa usalama ilichochewa na jaribio la Wasomali kujaribu kujitenga mapema baada ya Kenya kujipatia uhuru, hutajwa kama hadithi ya mafanikio ya mipango ya kupunguza vurugu zinazotumia silaha. Juhudi hizi ziliwajumuisha viongozi wa mashinani, wawakilishi wa akina mama, utawala wa eneo, na wadumishaji sheria katika juhudi za pamoja, ambazo hazikumshurutisha yeyote, za kudumisha amani na kudhibiti silaha ndogo ndogo na nyepesi.[88]

Mafanikio yanayosherehekewa mara kwa mara ni kazi ya Kikundi cha Wanawake wa Wajir kwa Ajili ya Amani, kilichoanzisha juhudi katika eneo hilo la Wajir za kuangamiza visa vya mapigano vilivyohusisha bunduki. Mafanikio haya yalisababishwa kuundwa kwa kikundi kingine kilichohusisha koo kadhaa kilichofahamika kama Kikundi cha Amani cha Wajir, ambacho kilisimamia mkataba wa amani ya eneo hilo—Azimio la Al Fatah. Harakati hizi baadaye zilipelekea kubuniwa kwa Kamati ya Amani na Maendeleo ya Wajir (WPDC)—mpango wa amani wa eneo hilo ambao, hatimaye, ulijumuishwa kama kamati ndogo ya serikali chini ya Kamati ya Wilaya ya Maendeleo mnamo 1995. Huu ulikiwa mwanzo wa kuundwa kwa kamati za maeneo husika za amani za kupunguza mapigano na kusimamia usalama, mwanzoni huku kaskazini mwa Kenya, lakini baadaye zikasambaa kote nchini. Kamati hizi zilikuwa na kazi muhimu ya kutumia mbinu za kitamaduni ili kusuluhisha mizozo, kwa mfano kupitisha makubaliano ya amani yenye masharti yaliyohusisha mila za jamii ambazo zimechangia usalama uliopo.

Kwa kweli, Shirika la Polisi wa Kimataifa, Interpol, hivi majuzi liliorodhesha Garissa—mji mkuu katika eneo la kaskazini-mashariki—kama mji ulio na usalama wa juu zaidi katika eneo la Afrika Mashariki na Kati (Astariko, 2011). Visa vya uhalifu na utumizi wa silaha mkoani Kaskazini Mashariki vimepungua, na juhudi za kieneo zimeibua hali ya upatanisho—utulivu wa kadri uliotokana na mikakati iliyokita mizizi kwenye ushirikiano kati ya serikali na raia.[89] Ingawaje kuna utulivu Kaskazini Mashiriki, jamii zingali zina wasiwasi, zikihofia athari za vita vinavyoendelea Somalia. Wasiwasi mkubwa zaidi katika eneo hilo kwa sasa ni tishio la kupenya kwa al-Shabaab, na kutumika kwa eneo hilo kama njia ya kupitisha silaha hadi maeneo mengine nchini. Taarifa za hivi karibuni kuhusu visa vya ulipuzi wa guruneti dhidi ya raia huko Garissa ili kulipiza uvamizi wa majeshi ya Kenya nchini Somalia, na vinavyoshukiwa vilifanywa na al-Shabaab, vinathibitisha wasiwasi huo.[90]

Maeneo mengine, kama Kanda ya Juu ya Mashariki na Kaskazini mwa Bonde la Ufa yangali yanapambana na ukosefu wa usalama unaosababishwa na silaha ndogo ndogo. Uhasama kati ya jamii mbalimbali ungalipo, ambapo kwingine unavuka mipaka na kuhusisha vikundi vingine (kutoka Ethiopia, Sudan Kusini, na Uganda).

Miongoni mwa sababu zinazozua upinzani kati ya jamii tofauti ni wizi wa mifugo na ubishi kuhusu mipaka, unaosababisha mizozo mingi kati ya jamii tofauti, kwa mfano huko Pwani, mzozo kati ya Wardei na Waorma kuhusu maeneo ya lishe kwa mifugo na mipaka. Jamii ziishizo Kaskazini mwa Bonde la Ufa hulaumiana kwamba huwa zinatafuta kuongeza ardhi, kama Wasamburu, ambao hudhani kuwa Wapokot hupenda kutafuta kupanua ardhi wanayomiliki. Wamaasai, Wakisii, na Wakuria wanazozana juu ya mipaka huko Nyanza, ilhali Wasabaot wana malalamishi kuhusu masuala ya ardhi huko Mkoa wa Magharibi. Mzozo kati ya Watharaka na Waigembe wa eneo la Meru pia ni kwa sababu ya mipaka. Mizozo yote hii, pamoja na vurugu zinazoambatana na uchaguzi, huhusu rasilimali.[91]

Kwa hivyo, ni wazi kwamba kungali kuna hali zinazochangia mazingira ya kuwepo kwa silaha ndogo ndogo. Ni dhahiri kwamba kutokea kwa michafuko iliyochochewa kisiasa mara kwa mara, iliyoongezewa nguvu na ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007/08, kumezua haja mpya ya kutaka kumiliki silaha ndogo ndogo, hususan katika maeneo ya kati ya Kaskazini mwa Bonde la Ufa. Kupungua kwa visa vya wizi wa mifugo huko Pokot Magharibi, wakati huo huo, kulihusishwa na biashara iliyofana ya ulanguzi wa silaha kwa sababu za ongezeko la wateja katika eneo la kati la Bonde la Ufa (UNDP/OCHA, 2008, uk.1). Katika eneo hili, haja ya kutaka kumiliki silaha inasemekana kuwa inasababishwa na vipengele viwili vipana. Mwanzo, serikali inachukuliwa kana kwamba imeshindwa kuhakikisha usalama wa kutosha. Pili, jamii zinazidi kuhisi uwezekano wa kuathiriwa kutokana na mashambulizi kutoka kwa majirani zao, vikundi vipya vya majambazi, na vijana waliojihami.

Ni sharti kusisitizia jambo hili moja muhimu: kuwa pamoja na kwamba ni jambo la maana kwa serikali kuchanganua vilivyo tatizo la silaha ndogo ndogo, itabidi pia itambue kwamba sababu za vikundi kutaka kukusanya silaha ndogo ndogo siyo tu kwa ajili ya kujihami bali pia ni kwa kutaka kujidhibiti vilivyo kisilaha, ili waweze kuwa na uwezo wa kufanya mashambulizi. Mbali na hayo, mikakati inayohusisha majadiliano, kama vile mashauri ya kuingilia kati ya serikali na wahusika wa mashirika ya kutetea haki za jamii katika maeneo husika, inabakia kuwa muhimu katika juhudi za kupunguza ghasia ambapo silaha hutumika, na hatimaye kupungua kwa/au

kuangamizwa kabisa kwa haja ya kuweko kwa silaha ndogo ndogo (Bevan, 2007, uk. 7).

Utafiti huu pia uligundua kwamba kaya nyingi zilihofia usalama wao zaidi wakati wa uchaguzi. Basi, usimamizi mzuri, na wa amani, wa uchaguzi nchini Kenya ni muhimu ili kujaribu kupunguza haja ya kuweko kwa silaha ndogo ndogo.

Katika kushughulikia mageuzi yanayoendelea, uimarishaji wa imani ya umma kwa mashirika ya udumishaji sheria wafaa usisitizwe, pamoja na uimarishaji wa utendaji kazi na kuwajibika kwa vikosi vya usalama, kukuzwa kwa mifumo inayoshirikisha serikali na raia katika usimamizi wa usalama. Sehemu ya uchunguzi huu iliyokuwa ikichunguza masaibu ya waathiriwa ilibainisha kuwa wengi wao walikuwa hawana imani na vikosi vya usalama.

Kwa hivyo, juhudi pia zinahitajika ili kuunganisha kiwango cha kitaifa cha mageuzi ya kitaasisi na mikakati ya amani na usalama ya eneo husika. Majopo-kazi ya wilaya kuhusu silaha ndogo ndogo na nyepesi, na kamati za amani za wilayani zinafaa zidumishwe. Pamoja na hayo, mifumo ya sera, kama ile iliyotungwa na KNFP ya Sera ya Kitaifa kuhusu Silaha Ndogo Ndogo na Nyepesi na Sera ya Amani ya NSC, zinahitaji kuratibiwa na serikali. Sera hizi zitasaidia sana juhudi za kujaribu kuziba pengo kati ya mikakati ya kitaifa na ya mashinani. Aidha uwezo wa utendakazi wa vikosi vya usalama unafaa kuimarishwa kupitia kutolewa kwa rasilimali za kutosha na kusambazwa kwa maafisa wa usalama wa kutosha kote nchini.

Ingawaje maendeleo yaliyopatikana kutoka kwa mikakati iliyoanzia mashinani, kama utumiaji wa mifumo ya amani ya eneo husika, imeigizwa kote nchini (kupitia kuundwa kwa kamati za amani na DTFs), mafunzo ya kina kutoka kwa juhudi zilizofaulu za kupunguza michafuko na idadi ya bunduki yamechukua muda kukubalika. Kwa mfano, ingawaje serikali ilionyesha maendeleo kwa kujumuisha hatua za kuimarisha imani ya wananchi kwa Operesheni Dumisha Amani, utata wa kiusalama wa sehemu husika na eneoni, miongoni mwa changamoto nyingine za ndani, zilirudisha nyuma juhudi za vikosi vya usalama. Hivyo basi, ingawa mpango huo wa upokonyaji silaha ulilenga wilaya kadhaa kwa wakati moja, jamii pinzani zilihisi kwamba zililengwa kwa njia isiyofaa, kwa kiasi fulani kutokana na

tuhuma kwamba jirani zao hawakupokonywa silaha kwa kiwango sawa na wao. Kwa sababu hiyo, makundi yaliyopokonywa silaha yalidhihirisha mahitaji zaidi ya silaha, huku mizozo ya sehemu husika ikiongezeka katika baadhi ya maeneo. Ukweli huu ulidhihirika wazi haswa huko Isiolo. Ni wazi kwamba suluhisho la haraka-haraka limekuwa usalimishaji silaha kwa nguvu. Imekuwa vigumu zaidi kujumuisha mikakati ya kuimarisha amani na ile ya kusalimisha silaha, licha ya kuwepo kwa mifumo ya mashinani ya amani na upunguzaji silaha.

Lakini mikakati inayoanzia mashinani ni kipande kimoja tu cha fumbo tata. Utafiti huu umedhihirisha kuwa kwa vile silaha hutoka mahala mbalimbali na husambazwa kokote, ni sharti kuwepo na mifumo kabambe katika eneo hili inayojumuisha udhibiti mipaka, mikakati ya pamoja kati ya nchi husika, na unchunguzi ufaao wa ndani, pamoja na mfumo wa kuhakikisha kwamba hatua za mikakati zinafuatwa.

Mifumo hii dhidi ya mahitaji na ugavi wa silaha inafaa, kwa sehemu fulani, kutegemea taratibu zilizoimarishwa za kutoa tahadhari ya mapema na kuchukua hatua zinazohitajika ambazo zinajumuisha kufuatilia na kuripoti changamoto kuhusu silaha. Kitengo-mwenza cha KNFP, NSC, kina kipengee kinachotoa tahadhari ya mapema ambacho kinafaa kutumika ili kuweza kuchukua hatua kabla ya shida za tatizo la silaha kuibuka. Hili ni suala linalohusu siyo tu ushirikishi wa vitengo na mashirika mbalimbali, bali pia ni onyo dhidi ya ushawishi wa kurudia juhudi badala ya kuziwianisha.

Uchunguzi huu haujamulika tu mienendo mipya inayoonyesha kunakopatikana silaha—kwa mfano hisia kuhusu ongezeko la kuenea kwa silaha magharibi mwa Kenya, pamoja na Bonde la Ufa —lakini pia unasaidia katika kutoa tahadhari za mapema na kuchukuliwa kwa hatua za mapema. Kuhusiana na hayo, utendakazi wa pamoja kati ya wadau wa KNFP, NSC, polisi, huduma ya upelelezi, na mashirika mengine ya kutetea haki za jamii ungekuwa na matokeo endelevu zaidi.

Kwa kiwango fulani, utafiti huu umeonyesha athari hasi za silaha ndogo ndogo kwa usalama wa binadamu. Katika kiasi kidogo tu chini ya theluthi moja ya visa, wahojiwa kwa ujumla walionelea kuwa vurugu ambapo silaha hutumika zilikuwa zimeongezeka, pamoja na vifo na majeruhi zaidi, visa vingi zaidi vya wizi wa mifugo, na ukosefu wa chakula uliokithiri

mipaka, mbali na mambo mengine. Haiwezi kukanushwa kwamba silaha ndogo ndogo zina athari isiyo ya moja kwa moja kwa afya, elimu, maendeleo duni, mbali na viashiria vingine vya maendeleo ya binadamu. Kwa hivyo, chunguzi zaidi zinazomulika uhusiano kati ya silaha ndogo ndogo na usalama wa binadamu na/au masuala ya maendeleo, ni muhimu ili kuziba mwanya uliopo.

La muhimu zaidi ni kwamba huu ndiyo utafiti wa kwanza na wa kina kufanywa kuhusu uratibu wa silaha zilipo eneoni tangu kuundwa kwa Mwongozo wa Kanuni Bora wa RECSA. Kulingana na mwongozo huo, uchunguzi wa kimsingi wa hali ya silaha unafaa ufanywe kabla ya zoezi lolote la kukusanya silaha. Mfano wa nchi ya Kenya, kupitia uchunguzi huu na ule wa uratibu wa silaha wa KNFP wa mwaka 2003, wafaa kuelekeza kuboreshwa kwa mikakati na mifumo ifaayo kuhusu silaha ndogo ndogo. Hii itahitaji kuyapa maarifa zaidi mataifa wanachama wa RECSA ili kuimarisha uwezo wa utafiti na kukuza ujuzi wao kuhusu masuala muhmu ya silaha ndogo ndogo na nyepesi.

## Mapendekezo

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, mapendekezo kadhaa yanaweza kuafikiwa au kubuniwa. Mapendekezo hayo yanaibuka kutokana na utambuzi na maoni ya LEAs na wahojiwa kutoka HHs, CSOs, na FGDs, na yamewekwa katika makundi kulingana na kujitokeza kwa masuala muhimu.

### *Kufuatilia na kuelewa hali halisi ya tatizo*

Kulingana na wajibu wa Mashirika ya kutetea haki za raia nchini Kenya wa kuunda jamii ya utekelezaji kuhusu ghasia ambapo silaha hutumika na maendeleo, uchunguzi huu umeangazia umuhimu wa kupima na kufuatilia (jinsia kutojumlishwa), mara kwa mara, matukio na athari za vurugu katika maeneo mbalimbali na kitaifa, na kuunda kikundi cha viashiria mahsusi na vinavyoweza kupimwa ili kutathmini maendeleo ya juhudi zinazofanywa za kupunguza visa vya ghasia za kutumia silaha na kuenea kwa silaha. Hususan, ufuatiliaji wafaa uhusu:

- kukuza, kuhifadhi katika kompyuta, kujumuisha na kuunda mahala ambapo takwimu na habari kuhusu usimamizi wa silaha ndogo ndogo na nyepesi zinaweza kutumika na wengi;
- kuunda miundo mipana ya kuripoti na ya ushirikiano kuhusu tahadhari na hatua za mapema ambazo zitahusisha kikamilifu raia, pamoja na washikadau mbalimbali. Zaidi ya hayo, kuna haja ya kuwahusisha viongozi wa jamii ili kusaidia kudhibiti ueneaji wa silaha haramu kupitia juhudi za kuwatambua walanguzi wa silaha, mahali zinapopitishwa, na masoko zinapouzwa;
- kuharakishwa kwa utaratibu wa kuziweka alama silaha halali za serikali na za watu binafsi;
- kukuzwa na kuimarishwa kwa maabara ya Kenya ya kutafuta ushahidi unaohitajika na mahakama, na ununuzi wa vifaa vipya vya kitekinolojia;[92]
- kufanyika kwa majaribio ya kufyatua risasi kwa kila bundiki inayomilikiwa na serikali au watu binafsi, na kukusanya habari kuhusu sifa za mwendo wa silaha hizo. Habari hizo zinafaa zihifadhiwe katika mkondodata au hifadhi ya data ya kitaifa ili kusaidia katika uchunguzi wowote ule kuhusu visa vinavyohusu silaha, na kupunguza kutumiwa vibaya kwa silaha haramu na za serikali; na[93]
- kuhakikisha kwamba silaha zitakazonunuliwa baadaye zinakuja na habari kuhusu sifa au mienendo ya silaha hizo.

### *Mazingira ya kitaasisi*

Kuimarishwa kwa juhudi za polisi kwafaa kujumuishe:

- kuongezwa kwa maafisa wa usalama zaidi, na kuonekana kwao zaidi katika maeneo husika. Katika maeneo mengi ya wafugaji wa kuhamahama, uhusiano kati ya jamii na taasisi rasmi za kiserikali na mashirika ya udumishaji sheria ni mdogo sana, na hii inatilia nguvu haja ya kuweko kwa mipango ya kiusalama iliyobuniwa na wanachi wenyewe. Hususan, kupelekwa kwa maafisa wa usalama kwenye maeneo tofauti tofauti kunafaa kuambatanishwa na mahitaji muhimu ya maeneo hayo.Katika maeneo ya mpakani, wasiwasi uliopo ni kuhusu udhibiti wa usalama wa mipakani, wizi wa mifugo, na ulanguzi wa silaha. Katika maeneo ya mijini,

changamoto za wizi wa mabavu na utekeji nyara wa magari, miongoni mwa nyingine, ndiyo masuala nyeti ya usalama;

- kupewa vifaa vya kutosha kwa mashirika ya udumishaji sheria, ikiwa ni pamoja na utoaji magari ya usafiri na vyombo vya mawasiliano, huku kipaumbele kikipewa maeneo yaliyo kwenye mipaka (kaskazini mwa Kenya);
- kuimarishwa kwa ubadilishanaji habari kuhusu usalama kati ya mashirika ya udumishaji sheria na wananchi kwa kutumia mikakati kama vile jamii kusaidiana na polisi katika upigaji doria, DTFs, kamati za wilaya za amani, na taratibu nyingine husika. Hii pia itajenga na kuimarisha imani ya umma kwa mashirika ya kudumisha sheria;
- kuimarishwa kwa uchunguzi na majukumu ya uendeshaji mashtaka ya mashirika ya kudumisha sheria na Idara ya Uendeshaji Mashtaka, ikiwa ni pamoja na mahakimu, hasa kuhusiana na juhudi za kukumbana na visa vya uhalifu vinavyohusu silaha ndogo ndogo na nyepesi;
- kuimarisha uwezo wa upelelezi wa taifa, hususan kwa upande wa udhibiti wa kuenea kwa silaha ndogo ndogo na nyepesi;
- kuundwa kwa kitengo maalum cha polisi kitakachohusika na silaha ndogo ndogo;
- ulainishaji ili kuleta ufanisi kwa usimamizi wa KPRs kwa minajili ya kuhakikisha kuimarika kwa nidhamu ya KPR, na uwajibikaji zaidi katika utumizi wa bunduki;
- kuchunguzwa na kuundwa upya kwa taratibu za KPR kuhusu kupatikana kwa usalama kupitia kuongezwa kwa idadi ya maafisa wa polisi; na
- Kukubali na kuelewa kwamba Mkoa wa Magharibi na eneo la South Rift ni maeneo ambapo idadi ya silaha ndogo ndogo inazidi kukua. Kuna haja ya kuimarisha uchunguzi kuhusu kuweko kwa silaha ndogo ndogo katika maeneo haya, na kusuluhisha migogoro, kudhibiti vitisho vinavyojitokeza dhidi ya usalama, na sababu zinazochangia kuwepo kwa mahitaji ya silaha.

Juhudi za kudhibiti ulanguzi wa silaha na maswala ya kudhibiti mipaka yafaa yahusu:

- Kuimarishwa kwa mikakati ya kudhibiti mipaka kupitia doria za mara kwa mara, kuimarishwa kwa vituo vya ukaguzi mpakani, kuundwa kwa vituo zaidi mpakani na kuimarishwa kwa taratibu za uchunguzi wa mipakani;

- Kupelekwa kwa vikosi vya usalama vya kukabiliana na matukio ya haraka mipakani ili kuzuia kuingizwa kwa silaha haramu na kukabiliana na wizi wa mifugo na mashambulizi;
- Kuimarishwa kwa majukumu ya polisi wa trafiki na wa CID katika kubuni njia za kuweza kugundua ulanguzi wa silaha, na kudhibiti uhalifu huu, na pia kuongezwa kwa vifaa kwa polisi hawa vya kuwasaidia kugundua silaha hizi;
- Kuimarishwa kwa uwajibikaji wa maafisa wa usalama wanaohusika katika uchunguzi wa maeneo panapoingizwa silaha hizi na njia za ulanguzi wa silaha kupitia kupambana na ufisadi katika maeneo haya na usimamizi mkali zaidi na kuchunguzwa kwa makini kwa maafisa hawa; na
- Kuboreshwa kwa hali na masharti ya kikazi ya LEAs ili kupunguza ufisadi na kuwapa motisha.

Kuboreshwa kwa mifumo ya sera kunafaa kuhusishe:

- kushawishi kupitishwa na kutekelezwa kwa sera za amani kuhusu silaha ndogo ndogo. Inahitaji sera hizi kukaguliwa kwa makini ili kutathmini iwapo kweli zinafana na ni muafaka kutumika kikamilifu kushughulikia vipengele kadha wa kadha vya masuala ya kijamii, kibiashara, kisiasa na kiusalama kuhusu ulanguzi wa silaha ndogo ndogo, usalimishaji silaha, na matatizo ya usalama wa jamii;
- kuchunguzwa upya kwa kifungu cha sheria kuhusu bunduki kwa lengo la kujumuisha hatua kalikali dhidi ya umilikaji wa silaha ndogo ndogo haramu, na
- kujumuishwa na kutumika kwa Kanuni bora za utekelezaji kuhusu usimamizi wa silaha ndogo ndogo katika juhudi na mazungumzo yanayoendelea kwenye sekta ya kuimarisha usalama nchini Kenya, kwa mfano, Mwongozo wa Kanuni Bora wa RECSA.

### *Hatua za kupunguza kupatikana kwa bunduki*

Hatua hizi zafaa zihusishe:

- hususan miongoni mwa jamii za wafugaji wa kuhamahama, utekelezwaji wa mipango ya kitamaduni ya kujenga hisia za jamii zitakazowafanya watupilie mbali tabia za umilikaji bunduki na tabia nyingine potofu.

Mfano mmoja ni mkakati wa Kanisa Katoliki wa Haki na Amani unaojumuisha amani na hali ya kujenga maisha huko Samburu, mkakati ambao umetilia maanani wepesi wa kuathiriwa na mzozo kwenye shughuli zake ili kuimarisha ushirikiano na majadiliano kati ya mahasimu Wasamburu, Wapokot, na Waturkana (Wepundi, 2011). Ingawaje kumekuwa na mafanikio fulani, mafanikio haya yanaweza kukita mizizi iwapo tu juhudi nyingine kama hizo zinaweza kutekelezwa kwa upana zaidi. Juhudi kama hizi zinafaa pia kuwa na sehemu ambapo kuna nafasi ya kuwa na mipango ya ubadilishanaji wa tamaduni ili kuimarisha umuhimu wa kuishi kwa utangamano na kujengwa kwa taasisi za kitamaduni, kwa mfano wazee viongozi, ili kuweko na uwezo wa kijamii wa kudumisha utangamano wa kijamii;

- kuchukuliwa kwa hatua madhubuti za usalimishaji silaha zinazolenga vikundi vyote chini ya Mwongozo wa kanuni Bora wa RECSA na juhudi za serikali za usalimishaji silaha na maendeleo. Hatua hizo zinapaswa pia kuunganishwa na nyingine husika zinazohusu amani na maendeleo;
- kushirikisha jamii katika suluhu za amani za mizozo ili kupunguza haja ya silaha ndogo ndogo, na
- kuweko kwa juhudi za usalimishaji silaha za kieneo, kama zile za pamoja, hususan katika maeneo ya Wakaramoja na Wasomali.

## *Hatua za kuwashughululikia wahasiriwa*

Hatua hizi zapaswa zihusishe:

- kushughulikia hatima ya wanaolazimishwa kuhama kwa sababu ya vurugu au mapigano. Mara nyingi serikali hulenga juhudi zake kwa wakimbizi wa ndani (IDPs) waliopo kwenye maeneo yanayokumbwa na fujo za uchaguzi mkuu kama katikati ya eneo la Bonde la Ufa. Ingawaje suluhisho kamili kwa kikundi hiki halijapatikana, utoaji upya wa makao na ulipaji fidia ni sharti pia uwajumuishe wengine kama hawa wanaoishi katika maeneo ya wafugaji wa kuhamahama. Matatizo ya watu kulazimika kuhama kwa sababu ya matukio ya wizi wa mifugo na mapigano kuhusu masuala ya jamii za wafugaji wa kuhamahama ndiyo matatizo ya kibinadamu yaliyopuuzwa zaidi katika nchi hii; na

- serikali kuboresha vifaa na huduma za mahospitalini, na kuziimarisha ili ziweze kuwatibu wagonjwa wenye majeraha ya risasi, mengi ya majeraha ambayo huwa na ugumu fulani.

### *Hatua zenye misingi ya utaratibu wa kimaendeleo*

Hatua hizi zapaswa zihusishe:

- Kukuzwa kwa hali ya kutafuta ajira mbadala huko Kenya kaskazini, kama kuchunguza zaidi uwezekano mkubwa uliopo wa kuchimba na kusafisha madini, kujengwa kwa maeneo ya watalii, biashara ya kuuza na kununua mifugo, na ukulima. Aidha, mipango ya kuzipa nguvu jamii inapaswa kuwahusisha vijana katika juhudi za kuzalisha mapato ili kupunguza mvuto wa ujambazi na visa vingine vya uhalifu ambako bunduki hutumika;
- Kuboreshwa kwa miundomsingi huko kaskazini mwa Kenya ili kulipa eneo hilo uwezo zaidi wa kuzalisha mali. Maeneo mengi ya kaskazini mwa Kenya hayana barabara zenye lami. Wakati huohuo, miumdombinu ya mawasiliano haijajengeka na ni duni Hii huzua athari za kiusalama, kwa mfano, katika kijiji kimoja huko Parkati, Samburu Kaskazini, shambulizi moja hivi majuzi lilisababisha vifo vya watu kadhaa, lakini jamii haikuweza kusambaza habari hizi mapema iwezekanavyo kwa sababu ya kutokuweko kwa mtandao wa simu za rununu. Lakini hata kama ripoti hii ingewafikia wahusika mapema, inachukua muda wa saa tano kwa gari kutoka Baragoi (mji mkubwa) hadi Parkati. Kuimarishwa kwa miundomsingi kwaweza pia kupunguza visa vya ujambazi barabarani (Wepundi, 2011, uk. 20);
- Kufanywa kwa utafiti zaidi, hususan miongoni mwa jamii za wafugaji wa kuhamahama na katika maeneo ya mijini ili kutambua uhusiano kati ya visa vya uhalifu, utumiaji wa silaha ndogo ndogo na masuala ya kijamii na kiuchumi;
- Kujumuishwa kwa mikakati ya udhibiti na upunguzaji wa visa vya ghasia za kutumia silaha katika mipango ya maendeleo, kuambatana na ahadi ya mashirika ya kutetea haki za jamii ya kubuni jamii ya utekelezaji kuhusu ghasia zinazohusisha silaha na maendeleo;
- Kukadiria njia zipitapo silaha ndogo ndogo ndani na nje ya nchi. Ingawaje uchunguzi huu uliangalia mienendo, idadi ya silaha haramu zinazovuka

mipaka inafaa ichunguzwe kwa makini ili kuthibitisha ni nani wahusika wakuu, kutokako silaha hizi haramu na halali, na ziendapo. Kushindwa kufanya hivi kulikuwa udhaifu mmoja wa uchunguzi huu; na

- Kutathmini majibu ya jinsia zote mbili, wake na waume, kwa mada na mitazamo mahususi. Takwimu zilizotumika katika uchunguzi huu na katika chunguzi za baadaye zinaweza kutumika kutenganisha maoni ya jinsia yanayohusu wasiwasi wao kuhusu silaha ndogo ndogo.

# V. Utaratibu au Methodolojia

## Utangulizi

Sehemu kubwa ya uchunguzi huu ni uchunguzi wa nyumba au kaya ulio-ambatanishwa na eneo fulani la kijiografia. Mfumo wa nyumba unatoka kwa taasisi ya kuhesabu idadi ya watu, Kenya National Population and Housing Census. Muhtasari wa hesabu ya idadi ya watu na nyumba zao (zinazolingana nayo) unapatikana katika machapisho kadhaa kuhusu idadi ya watu. Takwimu hizo zimeainishwa au kugawanywa katika viwango vya chini zaidi vinavyotumika wakati wa shughuli ya kuhesabu watu. Maeneo hayo yanafahamika kama kata ndogo, ambalo ndilo eneo dogo zaidi la utawala nchini Kenya. Maeneo haya yanatumiwa kwa kuhesabu idadi ya watu, kwa hivyo uorodheshaji au mpangilio unazitumia kata hizi ndogo kama msingi wake. Kwenye shughuli halisi ya kuhesabu idadi ya watu, kata ndogo hugawanywa katika maeneo ya kuhesabia ili kurahisisha shughuli ya kuhesabu. Kila eneo la kuhesabia linahitajika kuwa na wastani wa takriban nyumba 100. Mkusanyiko wa kata ndogo huunda lokesheni au kata, ambayo kwa upande wake huunda divisheni. Divisheni kadhaa huunda wilaya.

Kenya ina jumla ya wilaya 287 (PAIS, n.d.), nyingi zikiwa zimebuniwa katika muda wa miaka kadhaa iliyopita, kwani kulikuwa na wilaya 41 wakati wa kujinyakulia uhuru. Baadhi ya wilaya zilizopo kwa wakati huu zinakusanywa pamoja ili kuunda kaunti, na kwa hivyo zinafanana sasa na wilaya 41 za awali, isipokuwa wilaya zilizokuwa kubwa zaidi kieneo au pale idadi ya watu imekuwa kubwa kupita rasilimali zilizopo, na hivyo kulazimisha mgawanyo zaidi ili kuunda kaunti nyingine. Jambo hili liliathiri kaunti sita, na tangu kutangazwa rasmi kwa katiba mpya, Kenya sasa ina kaunti 47. Kaunti hizo zinawakilisha maeneo madogo ya kitaifa yaliyotumika kwa shughuli hii ya uratibu.

## Utaratibu wa Sampuli

### *Mfumo wa sampuli kwa uchunguzi wa nyumba*

Takwimu za idadi ya watu zilipatikana kutoka kwa idara ya kitaifa ya takwimu, Kenya National Bureau of Statistics, ambazo zilijumuisha kiwango cha idadi ya watu na idadi ya nyumba. Ilihesabiwa kwamba idadi ya watu 38,610,997 wakiwa wakaazi wenye nyumba au kaya (HH) 8,767,954 za eneo letu lililolengwa linaashiria ukubwa wa wastani wa nyumba kuwa 4.65 (angalia hapo chini kwa maelezo kuhusu eneo-lengwa). Kwa kuwa kipimo kilichohitajika kwa uchunguzi huu ni nyumba au kaya, mkakati wa utaratibu wa sampuli ulikokotolewa kwa kutumia idadi ya nyumba nchini Kenya. Kwa kutumia kiwango cha uhakika cha asilimia 95, na kipindi cha uhakika cha 2, ukokotozi wa kiasi cha sampuli yenye viwango viwili hatimaye ulitoa sampuli ya nyumba 2,400. Maelezo ya kina ya ukokotozi huu ni kama yafuatayo:

(1) $$\text{ss_indefinite} = \frac{Z2 * (p) * (1 - p)}{C2}$$

Ambapo:
*ss_indefinite* = kiwango cha sampuli kwa kiwango cha sampuli kisichokuwa na mpaka
*Z* = Z thamani (k.m. 1.96 kwa kiwango cha uhakika cha asilimia 95)
*p* = asilimia ya wanaochagua, kuelezwa kama desimali
(0.5 kutumiwa kwa kiwango cha sampuli kinachohitajika[94])
*C* = kipindi cha uhakika, kuelezwa kama desimali
(e.g. 0.02 = ±2)

(2) $$\text{ss_definite} = \frac{\text{ss_indefinite}}{1 + \frac{\text{ss_indefinite} - 1}{\text{Pop}}}$$

Ambapo:
*ss_definite* = kiwango cha sampuli kwa kiwango chenye mpaka cha sampuli (kiwango cha mwisho cha sampuli)
*Pop* = kiwango cha idadi ya watu (k.m. idadi ya nyumba)

## *Sampuli kwa mahojiano ya CSO na LEA*

Ili kuendesha mahojiano ya mashirika ya kutetea haki za jamii, CSO, wasimamizi na makarani waliagizwa kuchagua, bila kuzingatia mpangilio maalum, watumishi tisa wa CSO kwa kila kaunti, mradi tu watimize maelezo na sifa zilizotajwa awali zinazotambulisha CSO (yaani Mashirika yasiyo ya Kiserikali, NGOs, zinazondesha kazi zake kwenye kaunti). Makundi haya yalifanyiwa sampuli kulingana na urahisi wa kupatikana kwao (yaani kadri yalivyopatikana).

Ili kuendesha mahojiano ya LEA, wasimamizi na makarani waliagizwa kuchagua wafanyakazi 25 wa mashirika ya udumishaji sheria, bila kuzingatia mpangilio maalum, kwa kila kaunti, mradi tu watimize sifa zilizowekwa awali kutambulisha shirika la udumishaji sheria la eneo husika (k.m. usimamizi wa mkoa, polisi, KWS, KFS, forodha, na kadhalika.)

## *Mfumo wa Sampuli kwa FGDs*

Makundi Mahususi ya Mjadala, FGDs, yaliendeshwa katika maeneo ambayo kwa kawaida yana sifa ya kuwa na tatizo la silaha haramu, kwa mfano sehemu za Magharibi mwa Kenya, Kaskazini mwa Bonde la Ufa, Kanda ya Juu la Mkoa wa Mashariki, Mkoa wa Kaskazini Mashariki, na miji mikubwa mitatu ya Nairobi, Mombasa, and Nakuru.

Washiriki wa FGD waliteuliwa makusudi kutoka kwa utawala wa mkoa husika, maafisa wa usalama (yaani polisi), wawakilishi wa NGO, wazee wa vijiji. Wafanyakazi wa utawala wa wilaya, wakielekezwa na mkurugenzi wa KNFP, waliwateua washiriki halisi wa FGD kutoka kwa kila kikundi.

## *Eneo-lengwa*

Kaunti zilipangwa katika matabaka mbalimbali kuambatana na idadi za nyumba, na kisha kupangwa zaidi kwa kutumia taarifa zilizopo kuhusu usalama.

Hivyo basi, kaunti zilipangwa kwenye makundi manne yafuatayo:

- Kaunti ishirini zenye chini ya nyumba 150,000 zilijumuisha tabaka I.
- Kaunti ishirini na tatu zenye kati ya nyumba 150,001–300,000 zilijumuisha tabaka II.

- Kaunti tatu zenye nyumba 300,001–500,000 zilijumuisha tabaka III.
- Kaunti moja yenye zaidi ya nyumba nusu milioni ilijumuisha tabaka IV.

Kila kaunti iliwekewa kiwango cha usalama kulingana na tajriba ya watafiti. Makundi matatu ya kaunti yalitambuliwa:

- Kaunti kumi na nne zenye kiwango cha juu cha uathirikaji na fujo zilichaguliwa, sehemu ambazo silaha ni nyingi, uhalifu umekithiri na hali ya ukosefu wa usalama ni ya juu sana. Kila mojawapo ya kaunti hizi 14 ilichaguliwa makusudi (angalia Jedwali 5.1).
- Kaunti nne za ziada kutoka tabaka III na IV pia zilichaguliwa makusudi kutokana na idadi yao kubwa ya nyumba.
- Kaunti zilizosalia 13 zilichaguliwa bila kuzingatia utaratibu maalum.

**Jedwali 5.1** Uteuzi wa viwango vya juu-, kadiri-, na chini vya uathirikaji wa kaunti kote nchini Kenya kwa uchunguzi huu

| Uathirikaji wa juu | Uathirikaji wa kadiri | Uathirikaji wa chini (nyingine) | |
|---|---|---|---|
| 1. Tana River | 15. Mombasa | 25. Kilifi | 39. Kakamega |
| 2. Garissa | 16. Kwale | 26. Lamu | 40. Vihiga |
| 3. Wajir | 17. Kirinyaga | 27. Taita Taveta | 41. Bungoma |
| 4. Mandera | 18. Murang'a | 28. Meru | 42. Busia |
| 5. Marsabit | 19. Kiambu | 29. Tharaka Nithi | 43. Siaya |
| 6. Isiolo | 20. Uasin Gishu | 30. Embu | 44. Homa Bay |
| 7. Turkana | 21. Nakuru | 31. Kitui | 45. Migori |
| 8. West Pokot | 22. Narok | 32. Machakos | 46. Kisii |
| 9. Samburu | 23. Bomet | 33. Makueni | 47. Nyamira |
| 10. Trans-Nzoia | 24. Kisumu | 34. Nyandarua | |
| 11. Elgeyo-Marakwet | | 35. Nyeri | |
| 12. Baringo | | 36. Nandi | |
| 13. Laikipia | | 37. Kajiado | |
| 14. Nairobi | | 38. Kericho | |

Kama hatua ya utaratibu wa sampuli, kiwango cha nyumba katika kata ndogo kiligawanywa kwa nyumba 100 (zilizoangaliwa kama kipimo kimoja kikubwa) kuvipatia usawa vizio vyote. Hizi zilipatiwa nambari zinazofuatana katika kaunti. Ikiwa kata ndogo ilikuwa na nyumba 2,000, ambazo ni sawa na kipimo cha 20 kwa ukubwa, hizi zingepewa nambari kutoka 1

hadi 20 kutoka kwa nambari kubwa zaidi iliyokuwepo. Hii inamaanisha kuwa katika kaunti yenye nyumba N kulikuwa na N/100 ya vipimo vya ukubwa, ambapo idadi ya mafungu inayohitajika (ikiwakilishwa hapa na kata ndogo) ilichaguliwa kwa utaratibu huku, mwanzo usiokuwa na mpangilio maalum ukiwakilisha kaunti. Hii ingelingana na kata ndogo, ambazo ndizo sehemu za kimsingi za sampuli yetu. Hata katika matukio ambayo kata ndogo zilikuwa na zaidi ya kipimo kimoja cha ukubwa, nambari ambazo zingechaguliwa zingewakilisha kata ndogo hiyo. Katika kila kizio kilichochaguliwa, nyumba 10 zingeteuliwa ili kuwakilisha nyumba zote 100 katika kata ndogo hiyo (fungu).

Kwa vile iliamuliwa kwamba tabaka I inapaswa kugawiwa nusu ya nyumba zilizotengewa tabaka II, huku matabaka mengine yakitofautiana kwa ukubwa, matokeo yalikuwa nyumba 700 zihojiwe katika tabaka la kwanza, 1,300 katika tabaka la pili, 360 katika tabaka la tatu, na 260 katika tabaka la mwisho. Sampuli hiyo imewasilishwa katika Kiambatisho 1.

**Jedwali 5.2** Ugawaji wa sampuli ya nyumba katika matabaka na kaunti

| Tabaka | Sampuli ya kaunti | Tabaka la HHs (N) | Sampuli ya tabaka la HHs | Sampuli ya HHs (n) |
|---|---|---|---|---|
| I | 14 | 1,773,160 | 1,237,287 | 700 |
| II | 13 | 4,769,735 | 2,657,354 | 1,300 |
| III | 3 | 1,240,053 | 1,240,053 | 360 |
| IV | 1 | 985,016 | 985,016 | 260 |
| **Jumla** | **31** | **8,767,964** | **6,119,710** | **2,620** |

Mgao wa mwisho wa hojaji zilizojazwa kote nchini Kenya uko kwenye Jedwali 5.3.

**Jedwali 5.3** Ugawaji wa sampuli ya HHs

| Eneo la utawala wa mkoa | Kaunti (idadi ya HHs zilizofanyiwa sampuli) | | Jumla ya HHs zilizofanyiwa sampuli |
|---|---|---|---|
| Nairobi | Nairobi | | 264 |
| Mkoa wa Kati | Kirinyaga (43)<br>Murang'a (68) | Kiambu (132) | 243 |
| Pwani | Mombasa (58)<br>Kilifi (71) | Kwale (41)<br>Tana River (14) | 184 |
| Mashariki | Meru (117)<br>Machakos (81) | Marsabit (19)<br>Isiolo (10) | 227 |
| Kaskazini Mashariki | Garissa (39)<br>Wajir (39) | Mandera (59) | 137 |
| Nyanza | Kisumu (66) | Migori (56) | 122 |
| Bonde la Ufa | Turkana (56)<br>West Pokot (30)<br>Baringo (36)<br>Samburu (13)<br>Laikipia (28)<br>Keiyo Marakwet (24) | Narok (51)<br>Trans-Nzoia (52)<br>Uasin Gishu (63)<br>Nandi (50)<br>Bomet (58)<br>Nakuru (113) | 574 |
| Magharibi | Busia (47) | Bungoma (86) | 133 |
| **Jumla** | | | **1,884** |

## Kukagua, kuthibitisha na kupima takwimu

Ili kuhakikisha ukweli, uthabiti na uzingatiaji maadili katika utayarishaji takwimu, utaratibu mkali wa kukagua na kuthibitisha ulitekelezwa kabla ya uchambuzi kufanywa.[95] Jumla ya hojaji 2,633 zilizokusanywa kutoka kwa sampuli ya taifa zima ya HHs ziliwekwa kwenye mkondodata wa kwanza. Wakati wa shughuli ya ukaguzi na uthibitishaji, hojaji 750 ziliondolewa, zikabaki hojaji 1,883. Kwa hojaji za LEA, jumla ya hojaji 710 ziliwekwa kwenye mkondodata wa kwanza, na 374 zikatupiliwa mbali kutokana na kiwango cha juu cha dosari au kiwango cha juu cha maswali kutojibiwa, na kuacha

jumla ya hojaji 336 za LEA. Kwa hojaji za CSO, jumla ya hojaji 255 ziliwekwa kwenye mkondodata wa kwanza. Kutokana na utaratibu wa ukaguzi, hojaji 77 zilitupiliwa mbali kutokana na kiwango cha juu cha dosari na kiwango cha juu cha maswali kutojibiwa na kuacha jumla ya hojaji 178.

Baada ya takwimu kukaguliwa na kuthibitishwa, visa binafsi vilipimwa ili kubuni sehemu ya uwakilishi wa idadi ya watu wote. Vipimo hivyo vilivyowekewa uchunguzi wa nyumba pekee, vinazingatia kaunti husika ilipo na uwiano wa jinsia kwa kila kaunti. Kisa kimoja hakikuwa na taarifa kuhusu mahali kilipo na kwa hivyo kikapewa kipimo cha alama moja, na kufanya idadi ya mwisho iliyopimwa ya nyumba kuwa N = 1,884.

Mbali na hojaji 2,620 za HH, takwimu hizo zilipaswa kujalizwa na takriban hojaji 775 za LEA, hojaji 279 za CSO, na 18 za FGDs. Za kwanza tatu zilichambuliwa kwa njia sawa na makundi ya takwimu ya HH. Kutokana na vikwazo dhidi ya utaratibu wa ugavi na usafirishaji, malengo hayakuafikiwa. Hata hivyo, yafaa kutiliwa maanani kwamba kiwango cha majibu kilifika asilimia 90, jambo ambalo litazipa nguvu takwimu zilizopatikana. (angalia Jedwali 5.3).

**Jedwali 5.4** Matokeo ya ukusanyaji takwimu kwa sampuli tatu za idadi ya watu

| Uchun-guzi | Sampuli-lengwa | Kiwango asili cha majibu | Idadi ya mwisho ya hojaji zilizojazwa | Kipimo cha makosa |
|---|---|---|---|---|
| HHs | 2,620 | 99.5% | 1,884 | 1.56% |
| LEAs | 775 | N/A | 710 | 2.69% |
| CSOs | 336 | N/A | 255 | 1.60% |

## Vifaa au njia zilizotumika

Aina tatu za hojaji zilizolenga HHs, LEAs, na wanachama wa CSOs zilitolewa. Vifaa vya ukusanyaji takwimu kwa uchunguzi wa HH, LEA, na CSO vilifanana sana. Shughuli za FGDs zilirahisishwa kwa kutumia mwongozo maalum uliokusudiwa kusaidia chunguzi pana kwa kuzipa taarifa bora zaidi zenye msingi wa maudhui sawa na yale yaliyopo kwenye hojaji zilizotumika kwa uchunguzi huu.

## Mafunzo na ukusanyaji takwimu

Jumla ya makarani 64 na wasimamizi 15 waliajiriwa kutoa hojaji hizo. Wasimamizi na makarani walipewa mafunzo kuhusu utaratibu wa uchunguzi na namna ya utoaji wa hojaji. Mafunzo hayo yalishughulikia masuala ya madhumuni ya utafiti, maadili ya utafiti, maswali yaliyomo kwenye hojaji na namna mahojiano yatakavyofanywa, upeo wa kijiografia, taratibu za utafiti, na mbinu za kudhibiti ubora. Hojaji ya uchunguzi wa HH, hali kadhalika, ilifanyiwa majaribio ya awali huko Nairobi, na kutokana na tajriba hiyo hojaji hiyo ilichunguzwa upya ili kushugulikia masuala yaliyojitikeza kutokana na majaribio hayo.

### *Namna mahojiano yalivyofanywa*

Kwa uchunguzi wa HH, takwimu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa katika sampuli za nyumba kuambatana na mpango uliotolewa. Mahojiano yalifanywa ana kwa ana na kila mhojiwa. Mzee wa kijiji alisaidia katika shughuli za nyanjani. Mzee huyo wa kijiji alimuonyesha karani mipaka ya kata ndogo na eneo la wastani lenye takriban nyumba 100. Karani aliagizwa kuchagua mahali bora pa kuanzia, na kuteua nyumba moja kwa kuchagua nambari moja kati ya moja na kumi (tuseme X). Kisha karani angetambua nyumba hiyo ilipo na kuanza mahojiano. Kwa hivyo basi hii ndiyo ingekuwa nyumba ya kwanza kufanyiwa mahojiano. Baada ya nyumba ya kwanza, karani alitakiwa kuhesabu na kuruka nyumba kumi ili kutambua nyumba ya pili kufanyiwa mahojiano. Utaratibu huu ulirudiwa hatua kwa hatua hadi fungu lote likawa limeshughulikiwa kikamilifu. Katika kila HH karani aliagizwa kumtambua mhojiwa mmoja mwenye umri wa zaidi ya miaka 16, na kujaribu kuwahoji wake kwa waume kadiri ilivyowezekana.

Hojaji zote zilizojazwa zilikabidhiwa wasimamizi kuzikagua na kuzihifadhi mwishoni mwa kila siku. Wasimamizi waliagizwa wahakikishe kuwa hojaji zimejazwa kikamilifu, zinasomeka, hazijapitwa na muda, hati zinaweza kusomeka kwa urahisi, na uthabiti wa majibu. Kuhakikisha usalama wa takwimu, wasimamizi walipaswa kuzichukuwa takwimu zote zilizokusanywa na kuzipeleka ofisini mwao, bila kutumia huduma ya tarishi, na hivyo basi usiri na usalama wa takwimu ulidumishwa.

### *Uingizaji takwimu kwenye tarakilishi na ukaguzi*

Uingizaji takwimu mitamboni na uchambuzi wa hojaji zote ulifanywa kwa pamoja mjini Nairobi. Programu ya kompyuta ya CSPro ilitumiwa ili kuingiza takwimu, ilhali ile ya SPSS ilitumiwa kwa uchambuzi. Ukaguzi wa takwimu na uthibitishaji ulifanywa kwa utaratibu ili kuhakikisha kuwa takwimu hizo zilizotumiwa kwa uchambuzi zilikuwa thabiti. Kundi la wataalamu wenye tajriba ya hali ya juu waliajiriwa kuingiza takwimu kwenye mitambo ya kompyuta kwa kutumia programu ya CSPro. Kundi hilo liliongozwa na mtaalamu wa tekinolojia ya kurusha habari kwa njia ya kiteknolojia, IT, ambaye alibuni programu hiyo ya uingizaji takwimu kwa ushirikiano na Small Arms Survey, ili kuhakikisha kwamba hojaji zote tatu zilizotumiwa kwenye uchunguzi zimo. Mtaalamu huyo wa IT alitoa mafunzo na kuwasimamia waingizaji takwimu, huku akiwasaidia pale ilipohitajika. Mtakwimu wa mradi pia alihakikisha kwamba hakuna takwimu mbovu au sisizoeleweka zilizoingizwa kwenye kompyuta. Takwimu yoyote ambayo haikuwa dhahiri ilirejeshwa kwa mtakwimu kwa ufafanuzi. Uchambuzi ulipaswa kutekelezwa kwa kutumia programu ya SPSS pamoja na Microsoft Excel. Baada ya takwimu zote kuingizwa mitamboni, zilitumwa kwa Small Arms Survey huko Geneva kwa uhifadhi, na uthibitishaji. Makosa yaliyogunduliwa yalirudishwa tena Nairobi ili kuthibitishwa kwa kutumia hojaji asili. Kwa sababu kumekuwa na zoezi hili la kurudiarudia mara kadhaa, takwimu hizo sasa ziko sawa, zimekaguliwa na kuthibitishwa. Maswali wazi, ambapo mtu anafaa atoe maelezo badala ya kujibu 'la' au 'hapana' tu yaliwekwa pamoja ili kuwepo na msingi wa uchambuzi wa pamoja. Uchambuzi wa majibu ya matini huru yalitoa maelezo mengi ya ziada.


## Matokeo ya demografia

### *Uwakilishi wa jinsia*


Uchunguzi wa nyumba (HH) ulikuwa na uwakilishi wa wake kwa waume uliokaribiana. Juhudi zilifanywa kimakusudi ili kuhakikisha usawa huu wa jinsia. Hata hivyo, miongoni mwa LEAs, kiwango cha wanaume kilikuwa

cha juu kuliko cha wanawake, kutokana na ukweli kwamba ni wanaume zaidi wanaoajiriwa katika mashirika ya udumishaji usalama. Miongoni mwa HHs, wahojiwa wa kike walijumuisha asilimia 49.9 (n = 935), na wa kiume walijumuisha asilimia 50.1 (n = 940)[96] (angalia Mchoro 5.1).

**Mchoro 5.1** Mgawanyo wa wahojiwa kijinsia, kwa makundi (HHs, LEAs, na CSOs)




**Mchoro 5.2** Kiwango cha elimu cha wahojiwa (HHs na CSOs)




## *Umri wa wahojiwa*

Katika kiwango cha HH (angalia Mchoro 5.3), umri wa wengi ulikuwa miaka 30–39, asilimia 28.0 ya wahojiwa. Vile vile, miongoni mwa wahojiwa

wa LEAs na CSO, wengi wa wahojiwa walikuwa na umri wa miaka 30–39, asilimia 39 na asilimia 34 mtawalia.


Uwakilishi wa chini zaidi ulikuwa wa wahojiwa wa umri wa miaka 16–19, uliowakilisha asilimia 4.6 ya sampuli ya HH, huku hesabu hiyo ikiongezeka mara dufu kwa wenye umri wa miaka 60 na zaidi, au asilimia 11.1. Hata hivyo wahojiwa wa CSOs wa makundi ya umri wa miaka 16–30 na miaka 60 na zaidi walijumuisha asilimia 1 na asilimia 5 ya jumla ya wahojiwa mtawalia (angalia Mchoro 5.5).

## *Elimu*

Katika uchunguzi wa HH na CSO, takriban theluthi moja ya wahojiwa walikuwa wamesoma hadi sekondari. Miongoni mwa wahojiwa wa HH, asilimia 23.2 hawakuwa wamekamilisha elimu ya shule za msingi, ilhali asilimia 29.6 walikuwa wamepata elimu ya shule za msingi. HHs ndiyo walikuwa hawajasoma sana, ilhali kwa wahojiwa wa CSOs, wale wenye elimu ya juu zaidi ya sekondari wakiunganishwa na wale wa vyuo vikuu kwa pamoja, walijumuisha asilimia 59.5 (angalia Mchoro 5.2).


**Mchoro 5.3**

Mgawanyo wa sampuli ya HH, kwa umri





**Mchoro 5.4**

Mgawanyo wa sampuli ya LEA, kwa umri




**Mchoro 5.5**

Mgawanyo wa sampuli ya CSO, kwa umri



# Kiambatisho 1: Mgawanyo wa sampuli kwa kaunti

**Jedwali A1** Sampuli ya ugawaji kwa kaunti

| Kaunti Jina | Hesabu |
|---|---|
| Baringo | 36 |
| Bomet | 58 |
| Bungoma | 86 |
| Busia | 47 |
| Garissa | 39 |
| Isiolo | 10 |
| Keiyo Marakwet | 24 |
| Kiambu | 132 |
| Kilifi | 71 |
| Kirinyaga | 43 |
| Kisumu | 66 |
| Kwale | 41 |
| Laikipia | 28 |
| Machakos | 81 |
| Mandera | 59 |
| Marsabit | 19 |
| Meru | 117 |
| Migori | 56 |
| Mombasa | 58 |
| Muranga | 68 |
| Nairobi | 264 |
| Nakuru | 113 |
| Nandi | 50 |
| Narok | 51 |
| Samburu | 13 |
| Tana River | 14 |
| Trans-Nzoia | 52 |
| Turkana | 56 |
| Uasin Gishu | 63 |
| Wajir | 39 |
| Pokot Magharibi | 30 |

# Kiambatisho 2: Utaratibu au methodolojia ya makadirio ya umiliki bunduki katika Jedwali 2.3

Makadirio ya umiliki wa bunduki yalifanywa kuambatana na msingi wa maswali mawili ya uchunguzi, ripoti za kibinafsi, na hisia kuhusu umiliki, huku kukiwa na makisio ya chini na ya juu, mtawalia. Katika makisio ya ripoti ya kibinafsi, hesabu iliyopatikana ilitokana na swali la moja kwa moja lililoulizwa wahojiwa wa kaya – iwapo nyumba au kaya yao ilimiliki bunduki. Ingawaje swali hili linategemewa kuwakilisha hesabu sahihi zaidi, ni wazi kwamba watu wengi hawapendi kufichua iwapo wanamiliki silaha, kama ilivyo majibu ya kawaida kwa maswali nyeti kama haya. Kiwango cha hisia kuhusu swali hili kinaweza kuwa cha juu au cha chini katika miktadha tofauti na nyakati tofauti, na hivyo basi kuonyesha sababu za kuwepo kwa tofauti kati ya matokeo yaliyotarajiwa na yale yaliyopatikana katika baadhi ya kaunti.

Katika makisio ya juu, hesabu iliyopatikana ilitokana na swali lisilo la moja kwa moja lililoulizwa wahojiwa wote wa uchunguzi (HHs, LEAs, na CSOs). Lilikuwa kuhusu ufahamu au hisia zao juu ya umiliki wa bunduki katika eneo lao. Kwa kuzingatia kwamba hizi ni hisia tu za wahojiwa, tunafahamu kwamba hesabu hii huenda haina msingi wa ukweli, na huenda hata ikawa imeongezwa zaidi. Ili kutoa kiwango cha juu zaidi, tulichagua makadirio ya juu zaidi kutoka kwa makundi hayo matatu (HHs, LEAs, na CSOs). Ili kutoa hesabu ya kadiri, kwa kutilia maanani mwisho kabisa wa pande zote mbili, hesabu ya juu zaidi na ya chini zilifanyiwa wastani ili kutoa makisio ya kadiri ya umiliki wa bunduki katika kaya.

Kwenye Jedwali 2.3, makundi matatu ya wahojiwa yaliainishwa kulingana na kiwango kilichodhihirishwa cha uathirikaji wa kaunti ambako walikuwa wanaishi (kiwango cha juu, kadiri au chini). Asilimia zilitolewa kutoka kwa kila kundi athirika, na kisha kuzidishwa dhidi ya jumla ya idadi ya kaya kwenye sampuli ya kaunti ya kundi athiriwa husika. Kwenye sampuli hii, kaunti zote zilizotajwa kuwa maeneo yaliyoathirika kwa kiwango cha juu

yalijumuishwa, ilhali kaunti 16 kutoka maeneo yaliyotajwa kuathirika kwa kiwango cha kadiri na cha chini hayakujumuishwa. Hivyo basi, tulibuni kielelezo-mfano, kilichoainisha sampuli katika sehemu mbili, athari ya kiwango cha juu na athari ya kiwango cha kadiri na cha chini, kisha tukatayarisha asilimia za umiliki wa bunduki kuambatana na majibu ya makundi yetu matatu. Asilimia ya athari za kadiri na chini kwa kila kundi ilitumiwa kama hesabu ya kubashiri ili kukisia umiliki wa bunduki katika kaunti 16 zilizosalia. Matokeo ya hesabu ya makisio ya umiliki wa bunduki yalijumlishwa na yale ya sampuli yetu na yakafikia jumla ya kaunti 47, ambazo zimeorodheshwa kwenye Jedwali 2.3.

## Mkokotoo au kufanywa kwa hesabu

### *Kaunti ambazo Hazikuchunguzwa*

Kupatikana kwa sampuli wakilishi katika utafiti kitakwimu hukabidhi sifa za sampuli hiyo kwa maeneo ambayo hayajachunguzwa lakini ambayo yana sifa za kidemografia au miktadha inayofanana na iliyochunguzwa. Hivyo basi, matokeo yaliyopatikana katika kaunti zenye kiwango cha kadiri na cha chini cha uathirikaji kutoka kwa sampuli ya uchunguzi wa sasa, yanaweza kuchukuliwa kuwakilisha kaunti ambazo hazikuchunguzwa lakini zenye viwango vya kadiri na chini vya uathirikaji, kutokana na hatua za kitakwimu zilizotekelezwa ili kuhakikisha kwamba sampuli hiyo inawakilisha taifa zima la Kenya, kama eneo zima kwa ujumla.

Ili kujumuisha kaunti ambazo hazikuchunguzwa, asilimia ya jumla ya wastani ilikokotolewa kwa kutumia asilimia iliyopatikana kutoka kwa maeneo yenye uathirikaji wa kiwango cha kadiri na cha chini. Kisha asilimia hii ilipimwa kuambatana na idadi ya kaya katika kila eneo la uathirikaji (kadiri: 2,389,231; chini: 1,571,364). Asilimia hii, hatimaye, ilizidishwa dhidi ya idadi ya kaya zilizosalia katika eneo ambalo halikuchunguzwa.Utaratibu wa kuhesabu uliotumiwa kupata asilimia za juu na za wastani kwa kila eneo la uathirikaji umetolewa hapa chini.

Hesabu ya asilimia ya maeneo ambayo hayakuchunguzwa:

([Kadiri HH x low %] + [Chini HH x low %]) / (Kadiri HH + Chini HH)

([2,389,231 x 1.0 %] + [1,571,364 x 2.4 %]) / (2,389,231 + 1,571,364) = 1.6 %

1.6 % x 2,648,244 = 42,371.9 → 40,000

Hesabu ya asilimia ya juu:

| | |
|---|---|
| Swali: | 'kwa maoni yako, ni nyumba ngapi zinazomiliki bunduki katika eneo hili?': |
| Chaguo la majibu: | (1) Chache sana (2) Chache kiasi<br>(3) Nyingi (4) Nyingi sana/Karibu zote |
| | 1 = 0 %, 2 = 25 %, 3 = 50 %, 4 = 75 % |

(Wastani wa % zote kwa swali hili hasa kwa kila eneo la uathirikaji)
x (eneo HH)
K.m., uathirikaji wa juu: 20.9 % x 2,159,115 = 450,000

Hesabu ya asilimia ya wastani:

(Juu % + Chini %) / 2
K.m.: Uathirikaji wa juu: (20.9 % + 4.7 %) / 2 = 12.8

# Kiambatisho 3: Silaha zilizopatikana mwaka 2010

**Jedwali A2** Silaha zilizopatikana mwaka 2010

| | Muundo/aina ya silaha | Jumla |
|---|---|---|
| 1. | Bunduki aina ya AK-47 | 481 |
| 2. | Bastola aina ya Revolver | 16 |
| 3. | Bastola | 60 |
| 4. | Bunduki ya kujitengenezea nyumbani | 25 |
| 5. | HK21 | 4 |
| 6. | Bunduki bandia | 105 |
| 7. | Karabini au bunduki fupi | 266 |
| 8. | Bunduki aina ya Mark 4 | 52 |
| 9. | Bunduki aina ya G3 | 138 |
| 10. | Bunduki aina ya M16 | 43 |
| 11. | Bunduki aina ya air gun | 11 |
| 12. | MG3 | 1 |
| 13. | Bunduki aina ya Mark I | 57 |
| 14. | Bunduki aina ya Liai | 35 |
| 15. | Bunduki ya rashasha | 6 |
| 16. | Bunduki aina ya Beretta | 45 |
| 17. | Chombo cha kurushia makombora | 6 |
| 18. | Suez | 2 |
| 19. | Mark 3 | 3 |
| 20. | She Carbing* | 2 |
| 21. | Bunduki aina ya Stun | 14 |
| 22. | FN | 7 |
| 23. | Bunduki aina ya Tranquillizer | 3 |
| 24. | H/Killer* | 9 |
| 25. | C/Mace* | 5 |
| 26. | Bunduki yenye mtutu mzito aina ya FN | 2 |
| 27. | Bunduki aina ya Bren | 2 |
| 28. | HK4 | 1 |
| 29. | Bunduki ya kuvulia | 1 |
| 30. | Patchet/Sterling | 1 |
| **Jumla** | **17,997 risasi (aina mbalimbali)** | **1,411 silaha** |

* Haieleweki wazi kinachomaanishwa hapa

**Duru:** Hati ambayo haijachapishwa iliyotolewa na shirika la Central Firearms Bureau wakati wa mahojiano na mwandishi, mjini Nairobi, 18 Agosti 2011; imetumiwa kwa kibali

# Tanbihi

1 Hakuna fasiri ambayo imekubalika kimataifa ya silaha ndogo ndogo na nyepesi. Ripoti hii inatumia orodha iliyotayarishwa mnamo mwaka wa 1997 na jopo la wataalamu wa Umoja wa Mataifa. Jopo hilo linaorodhesha silaha ndogo ndogo kuwa zile zinazojumuisha '[b]astola za kawaida na zile zinazojipakia; [b]unduki aina ya 'rifle' na karabini, au bunduki fupi; [b]ombomu au bunduki za rashasha; [b]unduki za mashambulizi; [na] [b]ombomu nyepesi'. Linaorodhesha silaha nyepesi kujumuisha 'bombomu nzito; vifaa vya kurushia makombora vyenye mtutu unaoshikiliwa chini kwa mkono; [b]unduki za kutungua ndege zinazoweza kubebeka na za kushambulia vifaru, bunduki zisizorejea nyuma baada ya risasi kutoka; [v]ifaa vinavyobebeka ili kurushia makombora ya kushambulia vifaru na mifumo ya roketi; [v]ifaa vinavyobebeka vya kurushia makombora ya kutungua mifumo ya ndege; [na] [m]akombora ya kipenyo cha mwanzi kwa chini ya 100 mm' (UNGA, 1997, sura 26). Kwa ujumla ripoti hii inatumia maneno 'silaha ndogo ndogo' kumaanisha silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi, isipokuwa pale inapotajwa tofauti.

2 Kwa mfano, Kamenju, Singo, na Wairagu (2003, uk. 47–52) wanataja usalama, ushindani wa rasilimali za kiasili zinazopungua, wizi wa mifugo, umaskini na ufisadi miongoni mwa maafisa wa usalama kama chanzo kikuu cha ueneaji silaha katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa.

3 Ubia wa mashirika yanayounda Kundi la Utafiti wa Ushauri Barani kwa sababu hiyo ulionya kwamba ajenda thabiti ya marekebisho isipotekelezwa, uhuru wa usafiri mkoani Bonde la Ufa utaathiriwa wakati wa uchaguzi hapo baadaye (CART, 2010, uk. 8–9).

4 Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari, kulikuwa na zaidi ya risasi 28,000 za kipimo cha 9 mm, na takriban risasi nyingine 2,500 za silaha nyinyine ndogo ndogo anuwai za viwango mbalimbali (angalia, kwa mfano, *Daily Nation*, 2010a

5 Kumekuwa na tetesi kwamba silaha na risasi kama zile zilizopatikana huko Narok zinaweza kutumiwa kuwapa tena silaha wanamgambo katika eneo la Bonde la Ufa na kwingineko (Citizen TV, 2010).

6 Kwa uchambuzi wa kihistoria wa kina zaidi kuhusu upinzanivita na ushindi wa Uingereza kanda ya Afrika Mashariki, tazama Collins (2006, uk. 16–22).

7 Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inajumuisha Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania, na Uganda (EAC, n.d.a). Jamhuri ya Sudan Kusini ilituma ombi la kutaka kujiunga na EAC mnamo 11 Novemba 2011; ombi hilo lingali linasubiri uamuzi (EAC, n.d.b).

8 Cock (2000, uk. 78–79) anatoa hoja kwamba kutokana na hayo AK-47 ina maana na utambuzi wa kijamii unaozua mjadala Afrika Kusini, kwa mfano.

9 Hizi zinajumuisha KNFP (2003), ambayo ina matokeo ya uratibu wa silaha ndogo ndogo nchini, na pia Adan na Pkalya (2005) na Kamenju, Singo, na Wairagu (2003).

10 Shughuli ya kijeshi ya Wajir hufahamika mara nyingi kama Mauaji ya halaiki ya Wagalla. Angalia, kwa mfano, ACORD (2010, uk. 19).

11 Ripoti hizo mbili za Human Rights Watch zinaelezea ukatili na ukiukaji wa haki za binadamu uliotekelezwa na maafisa wa usalama wakati wa shughuli za kijeshi huko Mt Elgon na Mandera (HRW, 2008; 2009).

12 Licha ya mafanikio haya, bado ilihofiwa kwamba kundi la SLDF lingejikusanya tena huko Mt Elgon (Wachira, Muluka, na Wepundi, 2010, uk. 43).

13 Mahojiano ya mwandishi na kamanda wa ASTU Gilgil, 19 Agosti 2011.

14 Mahojiano yasiyo rasmi ya mwandishi na naibu mkurugenzi wa KNFP, Nairobi, Julai 2011.

15 Mahojiano ya Small Arms Survey na ofisi ya KNFP, Nairobi, 20 Machi 2012.

16 Uchunguzi huo ulihusisha kaunti saba katika eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa, hususan Trans-Nzoia, Pokot Magharibi, Turkana, Marakwet, Baringo, Samburu, na Laikipia. Ripoti hizo zinasubiri kuchapishwa.

17 Haya ni pamoja na RECSA, Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), ISS, Saferworld, Oxfam GB, Shirika la Ujerumani la Ushirikiano wa Kimataifa, na EAC, miongoni mwa mengine.

18 Baadhi ya chunguzi jumuishi zaidi kuhusu silaha ndogo ndogo nchini Kenya zilizingatia haswa eneo zima, au sehemu za eneo la kaskazini mwa Kenya (Mkutu, 2008; Adan na Pkalya, 2005; Kamenju, Singo, na Wairagu, 2003; Oxfam GB, 2003; Pkalya, Adan, na Masinde, 2003).

19 Uchunguzi wa RECSA/ISS kuhusu shughuli ya usalimishaji silaha haujachapishwa. Ulizingatia changamoto za silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi katika sehemu za mashambani na mijini, huku ukitoa mapendekezo juu ya hatua za usalimishaji silaha. Ulikuwa sehemu ya utafiti wa RECSA/ISS katika eneo hilo uliosababisha kubuniwa kwa Mwongozo wa Utendaji Bora kuhusu Upunguzaji Silaha kwa eneo la RECSA (Angalia Wepundi, 2010).

20 Uchunguzi wa kila mwaka kuhusu uhalifu uliofanywa na kituo cha Utafiti wa Usalama na Habari, Security Research and Information Centre, unaofahamika kama 'Kenya Crime Survey', ulichapishwa kwa mara ya mwisho mnamo 2003, na inawezekana kuwa ndiyo ulikuwa uchunguzi mwingine wa mwaka kuhusu mielekeo ya uhalifu uliohimizwa na shirika la kutetea haki za jamii (SRIC, 2003). Kwa upande mwingine, ripoti za polisi za kila mwaka kuhusu uhalifu, kimsingi hutoa takwimu na ripoti simulizi ya mielekeo ya uhalifu (Kenya Police, 2008; 2010).

21 Wilaya hizi zilikuwa Turkana, Pokot Magharibi, Wajir, Samburu, Marsabit, Baringo Mashariki, Tana River, Moyale, Trans-Nzoia, na Marakwet.

22 Hesabu hii haijumuishi bunduki zilizokisiwa kufikia 50,000 huko Moroto, zilizofanya jumla ya bunduki kufikia 222,995. Yasemekana ziligharimu KES 16.7 bilioni (au USD 223 milioni kulingana na kiwango cha ubadilishanaji wa fedha wakati huo). Pesa hizo zingetosha kugharamia elimu ya bure ya shule za msingi nchini Kenya kwa miaka miwili, na kujenga madarasa 600,000.

23 Makisio katika Mkutu (2008, uk. 4) yanaweza kuwa na kasoro, ikizingatiwa kwamba gazeti linalorejelewa linataja bunduki haramu 5,000. Ripoti hiyo ya gazeti inataja Kizito Sabala (Mwaniki, 2000).

24 Kwa mfano, kuna mwanajeshi aliyeuawa mnamo Novemba 2011 wakati lori la kijeshi la Kenya lilipokanyaga IED barabarani huko Mandera (Wabala, 2011).

25 Mahojiano ya Mtoa Habari Mkuu (KII), Garissa, 23 Aprili

26 Taarifa ya Mtoa Habari Mkuu, KII, na ofisa wa udumishaji sheria, Garissa, 23 Aprili

27 Kwa msingi wa Watoaji Habari Wakuu na maafisa wa udumishaji sheria, Garissa, 23 Aprili 2011 na Laini Saba, 27 Aprili 2011.

28 Ripoti hii inajumuisha matokeo yenye msingi wa hisia na tajriba **za** wahojiwa. Hisia inadhihirisha maoni ya wahojiwa, ilhali tajriba inadhihirisha matukio halisi yaliyowakumba. Viashirio vyote viwili vinachangia hali ya kuelewa, hasa katika hali ambapo wahojiwa huenda hawakufichua yaliyowakumba kwa kuhofia kujishtaki wenyewe katika shughuli haramu.

29 Virai 'maeneo yenye athari za juu' na 'maeneo yenye fujo' vinatumika kumaanisha kitu kimoja.

30 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

31 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Lokichoggio, 20 Julai 2011; Mandera, 19 Julai 2011; Kapedo, 27 Julai 2011.

32 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Maralal, 27 Julai 2011.

33 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Nakuru, 28 Aprili 2011; KII, Laini Saba, 27 Aprili 2011.

34 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

35 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Mandera, 19 Julai 2011; Kapenguria, 20 Julai 2011.

36 Mahojiano ya mwandishi katika shirika la Central Firearms Bureau, Nairobi, 18 Agosti 2011.

37 Mtoa Habari Mkuu, KII, Laini Saba, 27 Aprili 2011.

38 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Kimeu, 25 Aprili 2011.

39 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Nakuru, 28 Aprili 2011.

40 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Maralal, 27 Julai 2011.

41 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Mandera, 19 Julai 2011.

42 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Marsabit, 19 Julai 2011.

43 Kwenye majadiliano ya kundi mahususi, FGD, mshiriki alisema kwamba 'hata wavulana wa miaka saba wana AK-47. Mmoja alikuja amebeba moja na nikamuuliza ina risasi ngapi. Alitoa chemba ya risasi na kuzihesabu. Zilikuwa nne' (Small Arms Survey FGD, Lokichoggio, 20 Julai 2011).

44 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

45 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

46 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Migori, 14 Julai 2011.

47 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Malindi, 23 Aprili 2011; angalia pia Otieno (2008).

48 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

49 Kama ilivyoonyeshwa katika sehemu ya kwanza, uchunguzi ulijumuisha, kwa makusudi, kaunti zote zenye fujo au vurugu, hivyo basi inaweza kuchukuliwa kwamba kaunti zote ambazo hazikujumlishwa kwenye uchunguzi zilikuwa katika kiwango cha umiliki silaha kilicho chini ya wastani wa uchunguzi wa asilimia 2.7 (athari ya wastani au chini).

50 Jumla ya nyumba au kaya zilizosajiliwa katika shughuli ya kitaifa ya kuhesabu idadi ya watu nchini. Angalia sehemu V ya ripoti hii kwa maelezo ya kina

51 Angalia sehemu V ya ripoti hii kwa ufafanuzi wa shughuli ya kufanya sampuli.

52 Mtoa Habari Mkuu, KII, Garissa, 23 Aprili 2011.

53 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Nakuru, 28 Aprili 2011.

54 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Nakuru, 28 Aprili 2011.

55 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Nakuru, 28 Aprili 2011; Trans-Nzoia, 4 Juni 2011.

56 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Maralal, 27 Julai 2011.

57 Mtoa Habari Mkuu na ofisi ya utoaji leseni za bunduki; Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Mandera, 19 Julai 2011; Trans-Nzoia, 4 Juni 2011.

58 Maeneo yaliyotajwa ni yale yaliyoathiriwa kwa viwango vya juu-, kadiri- na chini.

59 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Mandera, 19 Julai 2011.

60 Kisa kimoja kilisimuliwa huko Kapedo, ambako mhojiwa mmoja wa kundi la mjadala FGD9 alisimulia jinsi mwanamke mmoja Mturkana alivyopigwa risasi na Mpokot. Alipoulizwa, alisema bunduki yake ni mpya na alitaka kujaribu kuona kama inafanya kazi (Small Arms Survey FGD, Kapedo, 27 Julai 2011).

61 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Marsabit, 19 Julai 2011.

62 Kwa mfano, mwezi Juni 2011 kulikuwa na uvamizi huko Kawap, Samburu Kaskazini (Obwocha, 2011).

63 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Maralal, 27 Julai 2011.

64 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Tot, 27 Julai 2011.

65 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Lokichoggio, 20 Julai 2011; Mandera, 19 Julai 2011.

66 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Mandera, 19 Julai 2011.

67 Matokeo haya yanathibitisha uchunguzi ulionukuliwa awali na Bevan (2008) kuhusu tatizo la risasi haramu huko Turkana, na pia Kamenju, Singo, na Wairagu (2003) kuhusu usalama huko North Rift.

68 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Lokichoggio, 20 Julai 2011; Mandera, 19 Julai 2011; Migori, 14 Julai 2011.

69 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Maralal, 27 Julai 2011; Marsabit, 19 Julai 2011; Trans-Nzoia, 4 Juni 2011.

70 Mtoa Habari Mkuu, KII, Garissa, 23 Aprili 2011.

71 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Garissa, 23 Aprili 2011.

72 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Maralal, 27 Julai 2011.

73 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

74 Mahojiano katika makao makuu ya KFS, Nairobi, 23 Agosti 2011.

75 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Marsabit, 19 Julai 2011.

76 Hii ni kawaida katika maeneo ambako polisi wa akiba, KPRs wamepelekwa.

77 Maoni yasiyo rasmi ya mshiriki wa kundi la mjadala, FGD, la Small Arms Survey, Marsabit, 19 Julai 2011.

78 Mtoa Habari Mkuu, KII, Maralal, 17 Julai 2011.

79 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Lokichoggio, 20 Julai 2011; Maralal, 27 Julai 2011; Mandera, 19 Julai 2011; Marsabit, 19 Julai 2011; Kapedo, 27 Julai 2011; Tot, 27 Julai 2011.

80 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Lokichoggio, 20 Julai 2011.

81 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Nakuru, 28 Aprili 2011.

82 Kwa mfano, washiriki wa FGD walisema kwamba walikuwa na wasiwasi sana kuhusu utumizi wa silaha butu au zenye bapa kwenye ghasia, kuliko utumiaji wa bunduki (Small Arms Survey FGD, Kimeu, 25 April 2011).

83 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Nakuru, 28 Aprili 2011; Trans-Nzoia, 4 Juni 2011; Garissa, 23 Aprili 2011.

84 Kwa mfano, udhaifu huu ulizusha madai kwamba kushindwa kwa wadumishaji sheria kuchukua hatua wakati dalili za mapema zilipoonekana ni mojawapo ya sababu zilizochangia kuongezeka kwa ghasia za baada ya uchaguzi za 2007/08 (CIPEV, 2008, uk. ix).

85 Kundi la FGD la Small Arms Survey, Maralal, 27 Julai 2011.

86 Makundi ya FGDs ya Small Arms Survey: Lokichoggio, 20 Julai 2011; Mandera, 19 Julai 2011; Kapedo, 27 Julai 2011.

87 Ingawaje serikali imetekeleza mazoezi kadhaa ya upokonyaji silaha, kwa mfano, Operation Dumisha Amani za 2005 na 2010, Operation Chunga Mpaka na Operation Okoa Maisha za mwaka 2008, miongoni mwa mengine, kumekuwa na mazoezi yaliyohusisha makundi ya kutetea haki za jamii, kama vile Mradi wa Upunguzaji Ghasia Zinakotumika Silaha, huko Garissa, uliofadhiliwa na UNDP.

88 Kwa mfano, Chopra (2008a, uk. 15–16) anaonyesha jinsi mifumo ya amani ya maeneo husika hatimaye inavyosababisha kuibuka kwa makubaliano ya amani kama Azimio la Modogashe-Garissa.

89 Kwenye uchambuzi huu kuhusu mafanikio ya ufanisi Wajir, Menkhaus (2008, uk. 25–29) anasema kwamba kamati ya WPDC imesaidia kudhibiti uhusiano baina ya koo za Ajuraan na Degodia tangu 1994, na kuanzisha mfumo mahuluti wa ujenzi wa maeneo katika majimbo dhaifu ambao ni tofauti na ule wa kielelezo cha Ulaya.

90 Kwa mfano, katika kisa cha hivi majuzi, watu sita walifariki kutokana na mashambulizi ya guruneti (Hussein, 2011).

91 Kwa mfano, NSC (2011, uk. 126–33) iliorodhesha sababu muundo na zinazokaribiana karibiana zinazosababisha mizozo katika sehemu tofauti za nchi.

92 Kwa mujibu wa  Mtoa Habari Mkuu, KII.

93 Kwa mujibu wa Mtoa Habari Mkuu, KII.

94 Asilimia hamsini imejikita kwenye msingi wa nafasi sawa ya majibu ya maswali yaliyogawanywa katika sehemu mbili. Hii yamaanisha kwamba majibu hayatarajiwi kuwa yana utaratibu maalumu, na kwamba majibu yote yana uwezekano sawa wa kuchaguliwa.

95 Hesabu halali inaashiria ubora, mwambatano, na kufaa kwa majibu kwenye hojaji, kama inavyonakiliwa na karani. Hivyo basi, majibu pekee yanayoweza kusomeka, kueleweka, na kuambatana na vigezo vya swali yanachukuliwa kuwa halali. Hesabu ya kutegemewa, au takwimu za kutegemewa katika jambo hili, inamaanisha takwimu zilizokusanywa ambazo hazijakumbwa na ukosefu wa utaratibu wa kimantiki. Hii inamaanisha kwamba, sawa na ushahidi au usemi wa wazi wazi, majibu hayapaswi kukinzana au kuhitilafiana. Hatimaye, hesabu yenye maadili inamaanisha kwamba karani amemsomea mhojiwa fomu ya kibali kabla ya kuendesha au kuandaa mahojiano, kwamba kuna ishara dhahiri kwenye hojaji kuonyesha nia ya mhojiwa kushiriki kwenye uchunguzi, na kwamba haki ya mhojiwa ya kukataa kujibu swali wakati wowote iliheshimiwa wakati wote.

96 Visa tisa havikuonyesha jinsia ya mhojiwa.

# Bibliografia

ACORD (Agency for Cooperation and Research in Development). 2010. *Pursuing Justice for Sexual and Gender-based Violence in Kenya: Options for Protecting and Compensating Survivors of Sexual and Gender-based Violence*. Nairobi: ACORD.

Adan, Mohamud na Ruto Pkalya. 2005. *Closed to Progress: An Assessment of the Socio-economic Impacts of Conflict on Pastoral and Semi-pastoral Economies in Kenya and Uganda*. Nairobi: ITDG.

Astariko, Steve. 2011. 'Garissa Boasts the Biggest Livestock Market in East and Central Africa.' *The Star* (Nairobi). Makala ya Mtandao, Mei18. <http://www.nairobistar.com/lifestyle/128-lifestyle/24787-garissa-boasts-the-biggest-livestock-market-in-east-and-central-africa>

Berman, Eric. 2007. 'Illicit Trafficking of Small Arms in Africa: Increasingly a Home-grown Problem.' Makala yaliyowasilishwa kwenye kikao cha GTZ-OECD-UNECA Expert Consultation of the Africa Partnership Forum Support Unit. Addis Ababa, Machi 14.

Bevan, James. 2007. *Between a Rock and Hard Place: Armed Violence in African Pastoral Communities*. Geneva: Small Arms Survey na UNDP.

——. 2008. *Blowback: Kenya's Illicit Ammunition Problem in Turkana North District*. Geneva: Small Arms Survey.

CART (Continental Advisory Research Team – Kundi la Ushauri wa Utafiti Barani). 2010. *State of the Union Kenya Report 2010*. Nairobi: George Bensons.

Chopra, Tanja. 2008a. *Building Informal Justice in Northern Kenya*. Ripoti ya Utafiti. Nairobi: Legal Resources Foundation Trust.

——. 2008b. *Reconciling Society and the Judiciary in Northern Kenya*. Ripoti ya Utafiti. Nairobi: Legal Resources Foundation Trust.

CIPEV (Commission of Inquiry into Post-election Violence – Tume ya Uchunguzi wa Ghasia za Baada ya Uchaguzi mkuu). 2008. *Ripoti ya Matokeo ya Uchunguzi wa Ghasia za baada ya Uchaguzi mkuu, CIPEV*. Nairobi: Government Printers.

Citizen TV. 2010. 'Narok Arms Cache Mystery.' Makala ya video ya YouTube. Februari 2. <http://www.youtube.com/watch?v=MOiZBfCTpN4>

Cock, Jacklyn. 2000. 'Weaponry and the Culture of Violence in South Africa.' In Virginia Gamba, ed. *Society under Siege: Managing Arms in South Africa*. Pretoria: Institute for Security Studies, uk 75–95.

Collins, O. R. 2006. 'The Turkana Patrol of 1918 Reconsidered.' *Ethnohistory*, Vol. 53, No. 1. Winter, uk. 95–120. <http://www.history.ucsb.edu/faculty/Collinsmaterial/articles/TurkanaRecon.pdf>

*Daily Nation* (Nairobi). 2010a. 'Police Seize Second Arms Cache in Narok.' Makala ya mtandao, Februari 1. <http://allafrica.com/stories/201002011607.html>

——. 2010b. '26 Quizzed over Narok Arms Cache.' Makala ya mtandao, February 4. <http://allafrica.com/stories/201002040952.html>

EAC (East African Community). n.d.a. 'Welcome to the EAC.' Ulifunguliwa 9 Januari 2012. <http://www.eac.int/about-eac.html>

——. n.d.b. 'Admission to the Community.' Ulifunguliwa 9 Januari 2012. <http://www.eac.int/about-eac/admission-to-the-eac.html>

Eavis, Paul. 2002. 'SALW in the Horn of Africa and the Great Lakes Region: Challenges and Ways Forward.' *Brown Journal of World Affairs*, Vol. 9, No. 1, uk. 251–60. Providence: Brown University.

Ekuam, Daudi. 2008. *An Overview of the Status of Small Arms and Light Weapons in Areas Affected by Post-election Violence in Rift Valley Province*. Ripoti ya utafiti ya UNDP/OCHA ambayo haijachapishwa.

Farah, Ibrahim, Ahmad Aisha, na Omar Daud. 2005. *Small Arms and Border Controls in the Horn of Africa: The Case of Malkasufta, Ethiopia; Mandera, Kenya; and Bula Hawa Somalia*. Nairobi: African Peace Forum and Project Ploughshares.

Hartford, Mark. n.d. *From Africa to Africa: Traffic in Arms*. <http://www.misna.org/uploads/trafficoarmi-en.pdf>

HRW (Human Rights Watch). 2002. *Playing with Fire: Weapons Proliferation, Political Violence, and Human Rights in Kenya*. New York: HRW.

——. 2008. *'All the Men Have Gone': War Crimes in Kenya's Mt. Elgon Conflict*. New York: HRW.

——. 2009. *Bring the Gun or You'll Die: Torture, Rape and Other Serious Human Rights Violations by Kenyan Security Forces in the Mandera Triangle*. New York: HRW.

Hussein, Issa. 2011. 'Six Dead in Garissa Grenade Attack.' *Daily Nation* (Nairobi). Makala ya mtandao, Novemba 25. <http://www.nation.co.ke/News/Six+dead+in+Garissa+grenade+attack/-/1056/1279074/-/jbf92d/-/index.html>

IDMC (Internal Displacement Monitoring Centre – Kituo cha kuchunguza wanaoachwa bila makao nchini). 2008. *Kenya: No Durable Solutions for Internally Displaced Yet: A Profile of the Internal Displacement Situation*. Geneva: IDMC.

Kamenju, Jacob Alex Nderitu, Mwachofi Singo, na Francis Wairagu. 2003. *Terrorized Citizens: Profiling Proliferation of Small Arms and Insecurity in the North Rift Region of Kenya*. Nairobi: Kituo cha Utafiti wa Usalama na Habari, SRIC.

Katumanga, Musambayi na Lionel Cliffe. 2005. *Nairobi – A City Besieged: The Impact of Armed Violence on Poverty and Development*. Bradford: Kituo cha Ushirikiano wa Kimataifa na Usalama, Centre for International Cooperation and Security.

Kenya. 1954. Kifungu cha sheria kuhusu bunduki, Firearms Act (rev. 2009, cap. 114). Kiliidhinishwa Januari 1. Nairobi: Government Printers.

Kenya Police. 2007a. *Takwimu linganishi za uhalifu kwa miaka 2005, 2006, na 2007*. Nairobi: Kenya Police. <http://www.kenyapolice.go.ke/resources/COMPARATIVE%20FIGURES%20 2005,2006AND%202007.pdf>

——. 2007b. *Takwimu za uhalifu*. Nairobi: Kenya Police. <http://www.kenyapolice.go.ke/resources/CRIME%20STATISTICS%202007.pdf>

——. 2008. *Takwimu za uhalifu*. Nairobi: Kenya Police. <http://www.kenyapolice.go.ke/resources/CRIME%20STATI2008.pdf>

——. 2010. *Ripoti ya mwaka ya uhalifu*. Nairobi: Kenya Police. <http://www.kenyapolice.go.ke/resources/Crime%20report%202010.pdf>

KHRC (Tume ya Haki za Binadamu nchini Kenya, Kenya Human Rights Commission). 2011. *Justice Delayed …: A Status Report on Historical Injustices in Kenya*. Nairobi: KHRC. Aprili.

Kimaiyo, David na Eliud Nthiga. 2009. *Mapping of the Disarmament Effort in Karamajong Triangle*. Ripoti ambayo haijachapishwa iliyotayarishiwa Taasisi ya Mafunzo ya Usalama, Institute for Security Studies, Nairobi. Novemba. <http://www.nscpeace.go.ke/nsc/index.php/resource-library/downloads/reports/80-mapping-of-the-disarmament-effort-in-karamojong-triangle>

KNFP (Kenya National Focal Point on Small Arms and Light Weapons). 2003. *Kenya Country Report to the UN Biennial Conference on the Implementation of the UN Programme of Action*. Nairobi: KNFP. 1 Julai.

——. 2006. *Kenya National Action Plan for Arms Control and Management*. Nairobi: KNFP.

——. 2010a. 'Disarmament in Kenya.' Makala yaliyowasilishwa kwenye warsha ya kuthibitisha upunguzaji silaha za vita iliyoandaliwa na Kituo cha Kanda kuhusu silaha ndogo (RECSA). Mombasa, Kenya, 30–31 Agosti.

——. 2010b. *Kenya Country Report to the Fourth UN Biennial Meeting of States on the Status of Implementation of the UN Programme of Action on Small Arms and Light Weapons and the Implementation of International Tracing Instrument*. Nairobi: KNFP

——. 2011. 'Consideration of Key Implementation Challenges and Opportunities Relating to the International Tracing Instrument, Including International Cooperation and Assistance.' Taarifa ya Bw D. M. Kimaiyo, CBS, mkurugenzi KNFP wakati wa mkutano wazi wa Wataalamu wa serikali wa Mpango wa Utekelezaji. New York, 9–13 Mei.

——. n.d. 'KNFP.' Mtandao. Ulifunguliwa 20 Machi 2012. <http://www.nscpeace.go.ke/nsc/index.php/knfp>

—— na Small Arms Survey. 2011. *Assessment of Small Arms and Perceptions of Security in Kenya*. Mkondodata yaani Database. Nairobi: KNFP.

KOFC (Kenya Ordnance Factories Corporation – Shirika la Kiwanda cha Silaha nchini Kenya). n.d. Mtandao wa kampuni. Ulifunguliwa Novemba 2011. <http://www.kofc.co.ke/>

Lewis, Mike. 2009. *Supply and Demand: Arms Flows and Holdings in Sudan*. Toleo la ukadiriaji wa usalama wa binadamu, Sudan Human Security Baseline Assessment Issue Brief No. 15. Geneva: Small Arms Survey.

Mburu, Nene. 2002. *The Proliferation of Guns and Rustling in Karamoja and Turkana Districts: The Case for Appropriate Disarmament Strategies*. <http://www.peacestudiesjournal.org.uk/dl/guns.pdf>

Menkhaus, Ken. 2008. 'The Rise of a Mediated State in Northern Kenya: The Wajir Story and Its Implications for State-building.' *Afrika Focus*, Vol. 21, No. 2, uk. 23–38. Ghent: Ghent Africa Platform and Afrika Brug.

Mkutu, Agade Kennedy. 2007. 'Small Arms and Light Weapons among Pastoral Groups in the Kenya–Uganda Border Area.' *African Affairs*, Vol. 106, No. 422. Januari, uk. 47–70. <http://www.ssrnetwork.net/uploaded_files/4346.pdf>

——. 2008. *Guns and Governance in the Rift Valley: Pastoralist Conflict and Small Arms*. Oxford: James Currey.

Muchai, Augusta. 2005. 'Insecurity: A Case Study of Northern Kenya.' In Micha Hollestelle and Simon Simonse, eds. *Security When the State Fails: Community Responses to Armed Violence*, Vol. 5. The Hague: Pax Christi, uk. 113–29.

Murunga, Godwin Rapando. 2005. 'Conflict in Somalia and Crime in Kenya: Understanding the Trans-territoriality of Crime.' *African and Asian Studies*, Vol. 4, Nos. 1–2. Leiden: Brill.

Mwaniki, Mike. 2000. 'Kenya: 5,000 Guns Unlicensed in Nairobi.' *Daily Nation* (Nairobi). Makala ya mtandao, 18 Disemba. <http://allafrica.com/stories/200012180426.html>

Nairobi Protocol (Mwafaka wa Nairobi wa uzuiaji,udhibiti na upunguzaji silaha ndogo na silaha nyepesi katika eneo la maziwa makuu, upembe wa Afrika na mataifa jirani). 2004. Nairobi, 21 Aprili. <www.recsasec.org/pdf/Nairobi%20Protocol.pdf>

Nation TV. 2010. 'Security Agencies Involved in Narok Arms Saga.' Makala ya video yaYouTube. Yalitangazwa 2 Februari. Yalifunguliwa 19 Septemba 2011. <http://www.youtube.com/watch?v=Oa-fQUFwptg&feature=related>

Ndung'u, James. 2010. *A Reserve Force in Decline: Dilemmas of Supporting Community Security through Auxilliary Police in Greater Marsabit*. Ripoti haijachapishwa. Marsabit: Tume ya kanisa Katoliki ya Haki na Amani, Catholic Justice and Peace Commission.

Nguli, Mutuku. 2008. *Small Arms and Light Weapons' Proliferation in Parts of Kenya*. Nairobi: PEACENET Kenya.

NSC (National Steering Committee on Peacebuilding and Conflict Management – Kamati Kuu ya Kitaifa ya Uongozi kuhusu Uimarishaji Amani na Usimamizi wa Mizozo). 2011. *National Conflict Mapping and Analysis: Peace and Conflict Trends in Kenya*. Ripoti haijachapishwa. Nairobi: NSC.

NTA (National Taxpayers Association – Chama cha Kitaifa cha Walipakodi). 2009. *Scoping Study: Public Security Services in Kenya*. Nairobi: NTA.

Obwocha, Beatrice. 2011. 'Raiders Kill Two as They Steal 136 Animals.' *The Standard* (Nairobi). Makala ya mtandao, 21 Juni. <http://www.standardmedia.co.ke/InsidePage.php?id=2000037611&cid=159&story=Raiders%20kill%20two%20as%20they%20steal%20136%20animals>

Oparanya, Wycliffe Ambetsa. 2010. *2009 Population & Housing Census Results*. Ripoti ambayo haijachapishwa ya waziri wa mipango, maendeleo ya kitaifa na ruwaza ya 2030. 31 Agosti.

Otieno, Alex. 2008. 'Improving Kenya's Response to Internal Displacement.' *Forced Migration Review*, Vol. 30. Aprili, uk. 55. <http://www.fmreview.org/FMRpdfs/FMR30/55.pdf>

Oxfam GB. 2003. *Oxfam GB-funded Peacebuilding Initiatives in the Arid Districts of Kenya*. Nairobi: Oxfam GB.

PAIS (Wizara ya Kenya ya Utawala wa Mikoa na Usalama wa Ndani). n.d. 'Background.' Mtandao. Ulifunguliwa 20 Machi 2012. <http://www.provincialadministration.go.ke/index.php?option=com_content&view=article&id=1:background&catid=12:about-us&Itemid=2>

Pkalya, Ruto, Mohamud Adan, na Isabella Masinde. 2003. *Conflict in Northern Kenya: A Focus on the Internally Displaced Conflict Victims in Northern Kenya*. Nairobi: Intermediate Technology Development Group.

Sabala, Kizito. 2002. 'The Proliferation, Circulation and Use of Illegal Firearms in Urban Centers: The Case of Nairobi, Kenya.' In Bonn International Center for Conversion (BICC). *Small Arms in the Horn of Africa: Challenges, Issues and Perspectives*. Brief No. 23. Bonn: BICC, uk. 36–41.

Saferworld. 2011. *Controlling Small Arms and Light Weapons in Kenya and Uganda: Progress so Far*. Nairobi: Saferworld.

SIKOM PeaceNetwork for Development. 2010. *Progress Report and In-depth Analysis of the On-going Military Disarmament in North Rift, Particularly in Pokot Region*. Ripoti ambayo haijachapishwa iliyotayarishwa na SIKOM kwa wadau.

Small Arms Survey. 2003. *Small Arms Survey 2003: Development Denied*. Geneva: Small Arms Survey.

SRIC (Security Research and Information Centre – Kituo cha Utafiti wa Usalama na Habari). 2003. *Kenya Crime Survey*. Nairobi: SRIC.

Stavrou, Aki. 2002. *Crime in Nairobi: Results of a Citywide Victim Survey*. Nairobi: UN-Habitat.

TI (Transparency International). 2010. *Corruption Perceptions Index 2010*. Berlin: TI. <http://www.transparency.org/policy_research/surveys_indices/cpi/2010/in_detail#6>

TI-Kenya (Transparency International-Kenya). 2011. *The East African Bribery Index 2011*. Nairobi: TI-Kenya.

UNDP/UNOCHA (United Nations Development Programme/United Nations Office for the Coordination of Humanitarian Affairs). 2008. *Humanitarian Update*, Vol. 21. 21–27 Mei. <http://reliefweb.int/node/268256>

UNGA (United Nations General Assembly). 1997. *Report of the Panel of Governmental Experts on Small Arms*. A/52/298 of 27 Agosti 1997. <http://www.un.org/depts/ddar/Firstcom/SGreport52/a52298.html>

UNODC (United Nations Office on Drugs and Crime). 2010. *Victimization Survey in Kenya: Executive Summary.* Nairobi: UNODC.

Wabala, Dominic. 2011. 'Al-Shabaab Landmine Kills One KDF Soldier.' *The Star* (Nairobi). Makala ya mtandao, 25 Novemba. <http://www.the-star.co.ke/national/national/50963-kenyan-soldier-killed-by-an-improvised-explosive-device-in-madera>

Wachira, Kiragu, Barrack Muluka, na Manasseh Wepundi. 2010. 'The Mt. Elgon Conflict: A Rapid Assessment of the Socio-economic, Governance and Security Factors.' *Amani Papers*, Vol. 1, No. 1, uk. 1–41.

Wairagu, Francis na James Ndung'u. 2003. 'The Problem of Small Arms and Initiatives for Combating Their Proliferation, Circulation and Trafficking.' In Intermediate Technology Development Group East Africa (ITDG EA). *Peace Bulletin*, No. 2. Nairobi: ITDG EA.


Wepundi, Manasseh. 2010. *Study on Practical Disarmament for the RECSA Region*. Ripoti haijachapishwa. Nairobi: Regional Centre on Small Arms/Institute for Security Studies.

——. 2011. *Context, Intervention and Impact: A Conflict Sensitivity Assessment of the Diocese of Maralal's CSA Pilot*. Ripoti haijachapishwa. Maralal: Catholic Justice and Peace Commission.

——, James Ndung'u, na Simon Rynn. 2011. *Lessons from the Frontiers: Civilian Disarmament in Kenya and Uganda*. Nairobi: Saferworld.

World Bank. 2010. *Aggregate Indicators of Governance 1996–2010*. Washington, DC: Mradi wa viashiria vya uongozi wa dunia, World Governance Indicators project. <info.worldbank.org/governance/wgi/pdf/wgidataset.xls>

Kuchapishwa katika Juni 2012
ISBN 978-2-9700771-8-3 ISSN 1661-4453



**Small Arms Survey**
Graduate Institute of International
and Development Studies
47 Avenue Blanc, 1202
Geneva, Switzerland

**p** +41 22 908 5777
**f** +41 22 732 2738
**e** sas@smallarmssurvey.org
**w** www.smallarmssurvey.org